# Nipashe

Jumatatu Mei 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579922

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Machinga wasalimu amri upanuzi wa barabara Dar

UKURASA 3







UKURASA 13

# Viongozi wa kanisa katika tuhuma nzito

**WATUHUMIWA** kutumia vibaya misamaha ya kodi kuingiza magari ya kifahari...*Endelea Ukurasa 2*



Wafanyabiashara wadogo wakihamisha vibanda vyao eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam jana, kupisha upanuzi wa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi yenye urefu wa kilomita tano kuanzia Morocco hadi Mwenge. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Lugola awageuzia kibao trafiki

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**NYUMBA 84 ZA WAKOPA BENKI KUPIGWA MNADA**

ZAIDI ya nyumba 84 zinatarajiwa kupigwa mnada, baada ya...

UKURASA WA 5

**ASKOFU GWAJIMA SASA AZIDI KUTETEWA**

MSANII maarufu wa vichekesho nchini, Emmanuel Mgaya, almaarufu Masanja Mkandamizaji...

UKURASA WA 26

**JPM APONGEZA TAASISI MASHINDANO QUR'AAN**

RAIS John Magufuli ameipongeza Taasisi ya Al-Hikma kwa kuandaa mashindano ya Qur'aan Tukufu yaliyojumuisha...

## Korosho, Masele kutikisa Bunge

UKURASA 3

**MICHEZO** SERIKALI, TFF SASA KUMTUZA SAMATTA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Viongozi wa kanisa wakumbwa tuhuma nzito

**Na Mwandishi Wetu**

MADAI kuhusu matumizi mabaya ya misamaha ya kodi yameibuka katika Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT), huku baadhi ya viongozi wa juu wa taasisi hiyo wakihusishwa kuingiza nchini magari ya aina mbalimbali yakiwamo ya kifahari.

Imebainika kanisa hilo lina namba ya mlipa kodi (TIN number) ambazo zote zimetumika katika kuingiza vitu mbalimbali kwa msamaha ikiwamo magari kwa miaka kadhaa kabla ya kugundulika.

Kutokana na hali hiyo, jumla ya wachungaji 546 wa kanisa hilo wanajiandaa kufungua kesi dhidi ya wadhamini wa taasisi hiyo kudai mali za kanisa hilo.

Hata hivyo, inaonyesha kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa EAGT, Heny Semfuko, alishachukua hatua za awali za kuiandikia barua TRA Desemba 12, mwaka 2017 na nakala kuituma kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Katika barua hiyo ambayo Nipashe imeona nakala yake, aliiomba kuchunguzwa kwa mali za kanisa na uingizwaji wa magari 50 kwa jina la taasisi hiyo, pamoja na kutengenezwa kwa TIN namba nyingine kadhaa zilizoonyesha kuhusika na jina la taasisi hiyo.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliandika barua kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Januari 4, mwaka 2018, ambayo ilisainiwa na Benjamin Mashauri kwa niaba ya CAG, ikimwomba kukagua mali, mapato na matumizi ya EAGT.

Katika barua hiyo ambayo gazeti hili imeona nakala yake, ilielezwa kuwa CAG anaomba kufanya ukaguzi huo baada ya kupokea barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Wadhamini wa EAGT Desemba 18, mwaka 2017 aliyeomba kufanyike ukagu

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola (kulia), akizungumza na waandishi wa habari mjini Morogoro, baada ya kukutana na madereva wa vyombo vya moto waliotaka kugoma kutokana na kutopewa mikataba ya kazi, matumizi mabaya ya tochi pamoja na ulipaji wa faini na kusimamishwa ovyo na matrafiki barabarani jana. Akiwa pamoja na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa. **PICHA: MAMBO YA NDAN**

# Nyumba 84 za wakopaji benki kupigwa mnada

**Na Romana Mallya**

ZAIDI ya nyumba 84 zinatarajiwa kupigwa mnada, baada ya wakopaji wa mikopo benki kuzitumia kama dhamana na kushindwa kurejesha fedha kwenye taasisi za fedha kwa muda uliopangwa.

Kwa mujibu wa tangazo lililotoka Jumanne ya wiki iliyopita kwenye moja ya magazeti ya wiki, nyumba hizo zitapigwa mnada kwa awamu tofauti kuanzia mwezi huu hadi Julai baada ya wahusika kushindwa kurejesha mikopo waliyochukua kwenye benki ya NMB.

Tangazo hilo ambalo lilitolewa na kampuni ya udalali ya Nsombo & Company (NC), limeainisha majina ya wadaiwa, mali ilipo na tarehe ya mnada utakapofanyika.

"Kwa idhini tuliyopewa na Benki ya NMB Makao Makuu tutauza nyumba za wadaiwa katika mikoa mbalimbali," lilieleza tangazo hilo.

Pia tangazo hilo lilisema mnada huo utafanyika mahali zilizopo mali hizo kwa tarehe na muda kama ulivyoainishwa kwenye tangazo hilo kati ya Jumapili ya mwezi huu hadi Julai 13.

Tangazo hilo limeweka hadharani majina ya wakopaji hao na dhamana walizoziweka wakati wa ukopaji.

Katika kipindi cha mwaka jana kampuni mbalimbali za udalali kwa nyakati tofauti zilitangaza uuzaji wa nyumba za wakopaji kwenye benki tofauti ambao walishindwa kurejesha mikopo wanayodaiwa.

Mwezi Aprili Benki ya EFC ya jijini Dar es Salaam, ilitangaza mnada wa nyumba 43, viwanja na magari yaliyowekwa rehani na watu waliochukua mikopo kwenye benki hiyo na kushindwa kuirejesha.

Kwa mujibu wa matangazo yaliyochapishwa Aprili 20, mwaka huu kwenye magazeti mawili tofauti, mnada huo ulijumuisha mali hizo ambazo zilinunuliwa au kuwekwa dhamana kama mkopo kwa wananchi hao.

Benki hiyo ilitoa kazi ya kuendesha mnada huo kwa kampuni za udalali ambazo hata hivyo, zilipopigiwa simu ili kutoa ufafanuzi wa mnada utakavyoendeshwa, hazikuwa tayari kueleza.

Katika tangazo lililochapishwa kwenye moja ya magazeti hayo, lilionyesha wateja 24 walikopa fedha kati ya Sh. milioni 30 hadi milioni 343 na kuweka rehani hati za nyumba na kadi za magari.

Tangazo hilo lilibainisha kuwa nyumba hizo ziko maeneo ya Kunduchi, Mbweni, Ukonga, Manzese, Temeke, Mivumoni, Buza, Mbagala, Kiwalani na Segerea.

Katika tangazo lingine, jumla ya wadaiwa 19 wenye mikopo kati ya Sh. milioni 25 hadi 120, walioweka dhamana ya nyumba, zilitangazwa kuuzwa kwa mnada wa hadhara.

Novemba 2, kampuni ya udalali ilitangaza uuzaji wa nyumba 21 baada ya wahusika kushindwa kurejesha mikopo waliyochukua kwenye benki ya NBC.

Mwaka jana, Mwenyekiti wa Kampuni ya udalali ya Yono Auction Mart, Stanley Kevela, alisema wamekuwa wakiuza nyumba za wateja walioshindwa kulipa mikopo ya benki kadhaa, kukusanya madeni ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

INAENDELEA UK. 8

## Lugola sasa awageuzia kibao trafiki

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewatangazia kiama askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini wanaowabambikia madereva makosa ya picha za mwendokasi (Speed rader) zisizo na uhalisia kwa nia ya kujipatia mapato wakibainika watawajibika kuzilipa wao wenyewe faini hizo na kuondolewa katika kitengo hicho.

Alitoa agizo hilo mjini hapa wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu maafikiano kati ya vyama vya watoa huduma za usafirishaji nchini kuhusu kusitisha kusudio la madereva wa mabasi ya abiria kufanya mgomo wakishinikiza kutimiziwa madai yao mbalimbali ikiwamo ya mikataba ya kazi.

Alisema maamuzi hayo yametokana na makubaliano ya pamoja baina viongozi wa vyama hivyo vya usafirishaji pamoja na wizara mtambuka za serikali kwa nia ya kutatua changamoto walizowasilisha katika kikao hicho kuhusu kubambikiwa makosa na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani.

Waziri Lugola, alisema moja ya makosa yanayolalamikiwa na madereva hao ni pamoja tochi zinazopiga picha mabasi na kurushwa kwenye simu za maaskari zinakosa uhalisia wa tukio ikiwamo kutoonekana kwa namba za usajili pamoja na vibao vya kuzuia makatazo mbalimbali na kusababisha utata na mivutano yenye nia ya kujenga mazingira ya rushwa.

Alisema kuanzia sasa askari hao wanapaswa kupiga picha katazo mbalimbali za barabara mbele ya gari ikionyesha mwonekano usio na mashaka, namba ya usajili pamoja na eneo la alama iliyokiukwa na dereva ili kuwapo na ushahidi halali vinginevyo dereva huyo asichukuliwe hatua yoyote.

"Dereva anapokuwa na mashaka na picha iliyopigwa dhidi ya gari lake kama haionyeshi usajili wa namba za gari na eneo la kibao cha zuio asikubali kuadhibiwa na badala yake amweleze huyo askari azitume picha hizo kwa msimamizi wa kikosi cha usalama barabarani na aende huko," alifafanua Waziri Lugola. Pia alisema tabia ya baadhi ya askari kukamata mabasi yenye abiria na kuyafikisha kituo cha polisi kwa nia ya kumuadhibu dereva aliyetenda makosa, jambo hilo liachwe mara moja na badala yake dereva aliyetenda kosa anapaswa kukamatwa katika kituo cha mwisho cha safari yake.

"Sheria ya Mamlaka ya Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), inaeleza wazi kila basi linalofanya safari za masafa marefu lazima liwe na madereva wawili, hivyo ukimkamata dereva na kumweka ndani tayari unaenda kinyume na sheria za Sumatra na kulifanya basi kushindwa kuendelea na safari yake," alisema.

Aidha, aliliagiza Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuendelea kuwanyang'anya leseni madereva wanaofanya makosa ya kujirudia pamoja na kukamata magari yanayofanya shughuli za usafirishaji bila kuwa na leseni kwa kushirikiana na Sumatra. Akielezea kuhusu maafikiano ya mgomo wa madereva wa mabasi, alisema wameshafikia makubaliano na kuagiza wamiliki wote wa mabasi na vyombo vingine vya usafirishaji kuwapa mikataba ya kazi mara moja kabla ya mkono wa serikali kuwafikia.

Waziri Lugola alisema pamoja na hatua hizo serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kufanyia kazi changamoto mbalimbali za sekta ya usafirishaji kupitia wizara mtambuka kwa kuwa miongoni mwake kuna mambo ya kisheria ili iweze kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

## HABARI KITAIFA

# Sababu za Zimamoto kuwatangaza 8 kuichafua

**Na Romana Mallya**

JESHI la Zimamoto na Ukoaji limewatangaza watu wanane kuwa siyo watumishi wao na hawatahusika na utapeli wanaodai kuuendeleza kwa kuchukua fedha kwa wananchi na kughushi vyeti vya ukaguzi.

Ofisa Habari, Mawasiliano, Uhusiano na Elimu kwa Umma wa jeshi hilo, Godfrey Peter, aliliambia Nipashe jana kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limelazimika kutoa tangazo la watu hao kutokana na vitendo vyao wanavyovifanya kwa wateja licha ya kufukuzwa kazi miaka miwili na wengine mmoja uliopita.

Tangazo la jeshi hilo lililotolewa jana kwa umma liliambatanisha picha na majina ya wahusika ambao ni Noely Byamungu, Abdul Mpondomoka, Rahim Pazi, Joseph Chale, Duncan Mwakajinga, Hashim Kapamba, Ahmed Nassoro na Weston Kaziyalele.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halitahusika kwa kutambua shughuli zozote zitakazofanywa na watu hao.

"Tunawashukuru wananchi kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa kwa jeshi. Tunawataka wananchi watoe taarifa haraka kwa jeshi pindi wanapotilia shaka mtu yeyote anayejihusisha na kazi za ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto," alisema.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, Peter alisema watu hao walifukuzwa kwa vipindi tofauti ambapo wapo walioondolewa mwaka mmoja uliopita na

**INAENDELEA UK. 8**



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akiongozana na Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dodoma, Dk. Dickson Chilongani, baada ya kuweka shada ya maua katika kaburi la aliyekuwa Mtemi Mkuu wa Ugogo Paramount, Chief Daudi Solomon Mazengo Chalula, jana katika kijiji cha Mvumi Makulu mkoani Dodoma. **PICHA: BUNGE**

# Polisi, machinga hapatoshi

**Na Gwamaka Alipipi**

POLISI na wafanyabiashara ndogondogo (machinga) katika eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam, jana waliingia kwenye mvutano baada ya kuambiwa waondoke katika eneo hilo ili kupisha ujenzi wa barabara ya njia nne.

Vurugu hizo zilidumu kwa dakika kadhaa baada ya polisi waliokuwa wamevalia sare kufika aneo hilo majira ya saa sita mchana wakiwa wamebeba silaha, huku gari maalum kwa ajili ya kubomoa vibanda vya machinga ho likiwa limeegeshwa pembeni tayari kwa kuanza kazi ya kuvunja.

Wafanyabiashara hao wanatakiwa kuhama eneo hilo na kutengewa eneo barabara inayoelekea kiwanda cha Cocacola.

Nipashe lilishuhudia baadhi ya wamachinga hao wakiimba nyimbo zilizoashiria kupinga agizo la polisi hao kuondoka eneo hilo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Rashidi Juma, aliiambia Nipashe kuwa eneo wanalotakiwa kwenda kufanya kazi halina idadi kubwa ya wateja kama ilivyo eneo hilo la Mwenge.

Alisema jambo la kushangaza serikali iliwapatia vitambulisho vya kufanyia kazi katika eneo hilo, lakini wanashangaa kuona Jeshi la Polisi linakuja kuwaondoa.

"Hili soko limebomolewa zaidi ya mara tano, tatizo kubwa siasa zimejaa kwa sababu huyu anatuambia tuondoke mwingine anasema tusiondoke, na huko wanakotaka kutupeleka biashara zetu zinakwenda kudoda," alisema Juma.

Mkuu wa Wilaya ya Konondoni, Daniel Chongolo, alifika katika eneo hilo na kuwashawishi wafanyabiashara hao, ambao walianza kuvunja wenyewe vibanda vyao.

Akizungumza na waandishi wa habari, Chongolo alisema serikali inawahamisha wafanyabiashara katika eneo hilo ili kupisha ujenzi wa barabara wa njia nne kutoka Morocco hadi Mwenge.

Alisema wafanyabiashara hao wanahamishiwa eneo lingine ambalo siyo mbali na walipo kwa sasa.

"Tumewaandalia eneo lingine la kufanya biashara, ni barabara iendayo kiwanda cha Cocacola, mkandarasi yupo eneo hilo na anamalizia kulikarabati, kilichobaki kwa sasa ni wao kuhamia tu," alisema Chongolo.

**INAENDELEA UK. 8**

# Korosho, Masele kutikisa Bunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

HOJA ya upinzani kuwataka baadhi ya mawaziri kuwajibika kutokana na sakata la mauzo ya korosho inatarajiwa kuendelea kutikisa wakati Bunge la Bajeti likiingia katika wiki la nane leo.

Vilevile, kusimamishwa kwa uwakilishi wa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele (CCM), katika Bunge la Afrika (PAP), kunatarajiwa kuendelea kuteka mijadala ya Bunge hilo baada ya Spika Job Ndugai, kuagiza ahojiwe na Kamati ya Maadili akimtuhumu kwa utovu wa nidhamu.

Pia Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe (Chadema), anatarajiwa kuwasilisha bungeni leo ushahidi kuhusu tuhuma zake dhidi ya Stella Manyanya, kwamba Naibu Waziri

**INAENDELEA UK. 8**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA 51YA 2019**
**ACESS BANK TANZANIA LIMITED....................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**IBRAHIM ABDI MAHD.............................. MJIBU MAOMBI**
**HABIBU ZAHARA .................................... MJIBU MAOMBI**
**RASHID MAKAM .................................. MJIBU MAOMBI**

**Kwa,**
**IBRAHIM ABDI MAHD**
**HABIBU ZAHARA**
**RASHID MAKAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Ijumaa, Tarehe 7 Mwezi 6 mwaka 2019 Saa 2:00 Asubuhi**Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.**ANGALIZO:**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 05 Mwaka 2019.**

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215237202



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA 50 YA 2019**
**ACESS BANK TANZANIA LIMITED....................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**NDEANA KANZA.................................. MJIBU MAOMBI**

**Kwa,**
**NDEANA KANZA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Ijumaa, Tarehe 7 Mwezi 6 mwaka 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 05 Mwaka 2019.**

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215237202

# Lugola amtaka RCO kuonyesha jalada kesi TLTC

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemtaka Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Morogoro (RCO) kuonyesha lilipo jalada la kesi inayokikabili Kiwanda cha Tumbaku (TLTC) mkoani hapa, ili kuwezesha kesi hiyo kuisha kwa wakati na kuondoa ukakasi wa unyanyasaji kwa kiwanda hicho.

Waziri Lugola alitoa agizo hilo jana wakati akiongea na waandishi wa habari mkoani hapa kuwa, wakati Tanzania ikitaka kupiga hatua katika uchumi wa kati, haoni sababu ya kuwasumbua wawekezaji hao.

Alisema, pia hata katika vifungu vya ndani ya Ilani ya CCM inaelekeza uwekezaji katika kukuza Pato la Taifa na kuwa wawekezaji wanapaswa kupewa nafasi ikiwa wanazingatia sheria na kanuni zilizopo.

Alisema, malalamiko yaliyopo kwa sasa ya polisi kuvamia ofisi za kiwanda hicho, wakidai kuwachunguza watuhumiwa bila kuwa na karatasi ya ukaguzi wala jalada la kesi yanampa wasiwasi wa kusumbua wawekezaji kama ikiwa hawana hatia.

Waziri Lugola alisema, anapenda kujua hilo kwa maslahi ya taifa na alipohoji aliambiwa kuwa polisi ilipata malalamiko ya mfanyakazi mmoja kutishiwa na wawekezaji wa kiwanda hicho na ndipo alifungua jalada polisi na kuanza uchunguzi kwa kwenda kwenye ofisi hizo.

Lugola alisema, toka apate taarifa hiyo siku nne zimekwisha bila kupewa jalada hilo huku akiwa hamuoni hata RCO mwenyewe ili aonyeshe jalada hilo licha ya kuliomba jambo ambalo alisema haridhishwi na mwenendo wa RCO wake.

"Huyo RCO akiitwa ao

INAENDELEA UK.26



Rashid Salum, mkazi wa Shehia ya Miembeni ambaye ni mwathirika wa mvua za masika akiwa amebeba chakula ukiwa ni msaada kutoka serikali kwa wananchi ambao nyumba zao zimeathiriwa na mvua za masika. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jaji Mkuu awafunda viongozi wa dini

**Na Mary Geofrey**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amewataka viongozi wa dini kushirikiana bila kuangalia tofauti za madhehebu yao ili kuzidi kuimarisha amani na upendo kwa Watanzania kwa sababu wao ni kinga muhimu ya nchi.

Alimtolea mfano, Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, kwa kufanya ziara katika nchi za Uarabuni kwamba kitendo hicho kilichobadili baadhi ya misimamo ya dini na kukaribishwa vizuri.

Prof. Juma alitoa rai hiyo juzi wakati wa hafla ya futari, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Shia kwa kushirikiana na Baraza la Waislam Tanzania (Bakwata) kwa lengo la kujenga mshikamano kati ya jamii na dini mbalimbali nchini.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa dini ya Kikristo, viongozi wa serikali, wanasiasa na wafanyabiashara mbalimbali.

Prof. Juma, alisema viongozi wa dini ni msingi mzuri wa kuendeleza amani ya nchi na kwamba kupitia wao nchini itazidi kuwa na mshikamano na maendeleo.

"Viongozi wetu wa dini wana dhamana kubwa ya kuzidi kuendeleza amani ya nchi kwa kupitia mafunzo ya elimu ya dini

INAENDELEA UK.26




# Tuhuma za ubadhirifu zatumbua watendaji 11

**Na Dege Masoli,** TANGA

WATUMISHI 12 wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wamefukuzwa kazi, akiwamo mmoja kushushwa mshahara wake kutokana na kujihusisha na tuhuma mbalimbali zikiwamo udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma kupitia mfumo wa Tehama.

Akitangaza maamuzi ya kuwafukuza watumishi hao kwenye Baraza la Madiwani wa Halmashauri lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini hapa, Meya wa Jiji la Tanga, Muhina Mustaph, alieleza kuwa watumishi hao walikuwa katika idara mbalimbali na kuwa maamuzi hayo yamefikiwa baada ya kujigeuza kama kamati na

kujiridhisha na mapendekezo ya Kamati ya Maadili ya Utumishi wa Umma ya kuwachukulia hatua.

Alisema watumishi 11 wameondolewa kazini na mmoja kushushwa mshahara kutokana na kuhusishwa na makosa mbalimbali ya kinidhamu kama utoro kazini, udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma.

Kwa mujibu wa Meya huyo, watumishi 11 wakiofukuzwa sita ni

watendaji wa mitaa na mmoja wa kata, watumishi wanne ni wa sekta ya afya na idara ya fedha na mtendaji wa mtaa wa Kwanjeka Nyota, Abd Kalua aliyeshushwa mshahara.

"Waliofukuzwa ni Chikila Gamba, Salum

Malick, Shaban Dosa, Fredrick Hiza, Michael Mhina na Abogasti

Komba na watumishi wa idara ya afya waliofukuzwa kazi ni

Bonivenja Laurence, Chikulute Subira, Mkunde Shaban na Shaban Kijonjoo ambaye alikuwa mhasibu msaidizi idara ya afya katika kituo cha afya Ngamiani," alieleza meya huyo.

Alisema aliyekuwa Mtendaji Kata ya Ngamiani Kusini alifukuzwa

kazi kutokana na kosa la udanganyifu na kufanya ubadhirifu wa fedha katika mfumo wa Tehama pamoja na kupokea fedha kutoka kwa wananchi kinyume cha utaratibu.

Mwingine ni Joachim Mabula aliyekuwa mtumishi wa idara ya afya ambaye alikuwa akikabiliwa na makosa ya utoro kazini kwa kuondoka eneo lake la kazi bila ya kutoa taarifa katika ngazi husika.



Mwananchi akitupa taka kwenye kontena maalumu la kukusanyia taka ndani ya Soko la Sabasaba jijini Dodoma kama alivyokutwa jana, Jiji hilo limeweka vifaa hivyo ili kuimarisha hali ya usafi katika maeneo mbalimbali hasa kwenye masoko. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu Gwajima azidi kutetewa

**Na Enock Charles**

MSANII maarufu wa vichekesho nchini, Emmanuel Mgaya, almaarufu Masanja Mkandamizaji, amesema video ya ngono inayodaiwa kurekodiwa ikimwonyesha Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, akiwa na mwanamke imetengenezwa na wasomi na kuwa haamini kuwa mchungaji huyo anaweza kufanya hivyo.

Akijibu swali katika kipindi maalum cha chombo kimoja cha habari nchini kuhusu kusambaa kwa video ya ngono ya mchungaji huyo ambaye ameonekana katika wimbo wake wa Kemea Pepo katika kipindi maalum cha chombo mojawapo cha habari nchini, msanii huyo alidai kuwa kwa sasa teknolojia imekuwa na hivyo upo uwezekano wa kutengenezwa video ya uongo kwa malengo mabaya dhidi ya mtu.

"Sio tu kuamini nina uhakika wa asilimia mia moja kwamba Askofu (Gwajima) hawezi kufanya kitu kama hicho yaani askofu hawezi kujirekodi akifanya vitu vya namna hii ingelikuwa mtu mwingine wa mtaani mimi ningeanzia hapo kuelewa," Masanja alisema.

Takriban wiki mbili zilizopita ilisambaa video ya ngono katika mitandao ya kijamii ikimwonyesha mtu mwenye sura kama ya Askofu Gwajima akiwa faragha na mwanamke ambaye hajafahamika mpaka sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari Mei 8, mwaka huu baada ya kusambaa video hiyo, Askofu Gwajima alisema video hiyo sio yake akibainisha imetengenezwa kwa lengo la kumchafua na kumnyamazisha akihusianisha na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Najua kuna watu wanajaribu kunichafua na kuninyamazisha kuelekea Uchaguzi Mkuu 2020 sasa nawaambia mdomo huu haunyamazishwi," Gwajima alisema.

Wakati polisi wakidai kuendelea na uchunguzi wa tukio hilo tayari askofu huyo amepata watetezi mbalimbali akiwamo Askofu wa Kanisa na Full Gospel Bible Fellowship, Zachary Kakobe, ambae Jumapili ya Mei 12, mwaka huu alikwenda katika kanisa la Gwajima na kumsafisha, akisema kwamba ni mipango ya shetani kuleta mgogoro baada ya watu kupatana.

# Mufti Mkuu aitabiria mema NMB kwa kujali jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MUFTI Mkuu wa Tanzania, Sheikh Aboubakar Zubeir, ameitabiria Benki ya NMB kufanikiwa katika kuhudumia jamii kutokana na utamaduni wa kuijali, kuithamini na kuipa kipaumbele chini ya mwamvuli wa kaulimbiu yao ya Karibu Yako.

Mufti Zubeir alisema hayo wakati akizungumza na waalikwa wa hafla ya benki hiyo ya kufuturisha waumini wa dini ya Kiislamu tangu kuanza kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani mwaka huu 2019.

Hafla hiyo iliyoshirikisha waumini wa Kiislamu, wateja na waalikwa wengine, ilihudhuriwa pia na Sheikh Mkuu wa Mkoa, Alhad Mussa Salum na Meya wa Jiji, Issaya Mwita.

"Niwapongeze kwa uamuzi huu wa NMB kufuturisha waumini wa Kiislamu, hasa ukizingatia mnahudumia makundi mbalimbali wakiwamo Wakristo na wasio na dini. Hii inatoa tafsiri moja tu kuwa NMB inajali makundi na kada mbalimbali za jamii, jambo ambalo litawapa mafanikio.

Alisema walichokifanya benki hiyo ni jambo kubwa, linalojenga uhusiano mkubwa baina ya Waislamu na wasio Waislamu, na kila mmoja kuitazama kama taasisi inayojali makundi yote ya watu na kwa namna hiyo wanazivuta nyoyo za wengi kuona inafanya kazi kwa weledi.

"Mtu akiwa mwema kiasi hicho ama hata taasisi, Mwenyezi Mungu humlipa ama huilipa, hii maana yake ni kuwa kwa utamaduni huu, NMB itapata mafanikio makubwa kutokana na namna mnavyojali makundi mbalimbali ya jamii," alisema Mufti Zubeir.

INAENDELEA UK.26

# Serikali kupanga maeneo itakayopita reli ya kisasa

**Na Munir Shemweta,** KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza kupangwa kwa maeneo itakapopita reli ya kisasa (SGR) ili shughuli zitakazofanyika katika wilaya na vijiji inapopita reli hiyo kuendana na shughuli za kiuchumi za mradi wa reli hiyo.

Waziri Lukuvi alisema wakati wa kupanga maeneo hayo hakuna mwananchi yeyote atakayenyang'anywa eneo lake bali yatapangwa kimji na kuainishwa matumizi yake kama ujenzi wa viwanda na hoteli na kuwataka wananchi wanaotaka kufanya uendelezaji mdogo kusubiri mpango huo.

Alisema hayo juzi katika vijiji vya Kwala na Soga vilivyopo Kibaha mkoa wa Pwani alipozungumza na wananchi wa maeneo hayo kuwaelezea mpango wa wizara yake kupanga na kupima maeneo yote inapopita reli ya SGR ili kuendana

INAENDELEA UK.26

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 52 YA 2019
ACESS BANK TANZANIA LIMITED....................MLETA MAOMBI
DHIDI YA
NASSOR HAMOUD MOHAMED.................................. MJIBU MAOMBI
RACHEL MATHIAS MSANGI..........................................MJIBU MAOMBI

Kwa,
NASSOR HAMOUD MOHAMED
RACHEL MATHIAS MSANGI

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Ijumaa, Tarehe 7 Mwezi 6 mwaka 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

ANGALIZO:
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 05 Mwaka 2019**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

215237202

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 67 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LTD .....................WALETA MADAI
DHIDI YA
MASERO JOHANES VISENT......................MJIBU MADAI
RAMADHANI MSANGI SHADA..................................MJIBU MADAI

Kwa,
1. MASERO JOHANES VISENT
2. RAMADHANI MSANGI SHADA

Dar es Salaam

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatano, Tarehe 5 Mwezi 6 mwaka 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

ANGALIZO:
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **16 Mwezi 05 Mwaka 2019**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

215237202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Watanzania itumieni vema fursa ya Sevilla nchini

**WAPENZI** wa soka nchini Alhamisi wiki hii watapata fursa ya kipekee kwa mara ya kwanza katika historia ya soka Tanzania, kuishuhudia mubashara timu inayoshiriki Ligi Kuu Hispania, La Liga, Sevilla ikitandaza kabumbu Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Sevilla yenye historia kubwa La Liga na barani Ulaya kwa ujumla, itashuka Uwanja wa Taifa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji wao, Simba, mchezo huo ukiwezeshwa kwa ushirikiano mkubwa na Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni, SportPesa na La Liga.

Aidha, SportPesa ambao ni wadhamini wakuu wa Klabu ya Simba, wamesema ujio wa Sevilla ni moja ya mipango yao ya kuhakikisha wanakuza soka nchini na kuzipa mazoezi ya kutosha klabu wanazozidhamini kwa kupata uzoefu wa kupima uwezo na klabu kubwa duniani.

Na kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), wameeleza maandalizi kwa ajili ya mechi hiyo yapo tayari wakati huu Sevilla ikitarajiwa kuwasili nchini kesho.

Hata hivyo, katika kuhakikisha mashabiki wa soka na Watanzania kwa ujumla hawaipotezi fursa ya kuishuhudia mubashara mechi hiyo, TFF imetangaza viingilio rafiki kabisa katika mchezo huo.

Kiingilio cha chini katika mchezo huo ni Sh. 5,000 wakati cha juu (VIP) ambacho kitajumuisha vinywani na usafiri kutoka Hoteli ya Serena iliyopo Posta jijini na kurudi, kikiwa ni Sh. 100,000.

Hakika hii si mechi ya kukosa kwani historia inakwenda kuandikwa kwa Simba kucheza na mabingwa hao wa kihistoria [mara tano] wa michuano ya Uefa Europa League.

Pamoja na yote hayo, wachezaji wa Simba hawana budi kuitumia mechi hiyo kuonyesha ubora wao kwani hiyo inaweza kuwa fursa ya kipekee kwao kupiga hatua moja zaidi kisoka.

Nipashe tunaamini mchezo huo utakuwa ukimulikwa na wapenzi wa soka dunia nzima, hivyo wachezaji wa Simba ni fursa kwao kuonyesha kiwango cha hali ya juu ili kujitangaza kisoka.

Mbwana Samatta anaweza kuwa mfano wa kuigwa katika hili, kwani ni mmoja wa wachezaji aliyetumia fursa ya kucheza mechi mbili tu kati ya Simba na TP Mazembe kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kuweza kutangaza uwezo wake kabla ya kununuliwa na klabu hiyo ya DR Congo na hatimaye KRC Genk ya Ubelgiji.

Hivyo, tunaamini kupitia mchezo huo, wachezaji wa Simba wana fursa pana ya kujifungulia milango ya kucheza soka nje ya Tanzania kwa kuonyesha kiwango cha hali ya juu Alhamisi.

Kadhalika, fursa hiyo haipo kwa wachezaji tu, bali tunaamini hata benchi la ufundi linaweza kumulikwa na klabu kubwa kama Simba itaonyesha soka la kuvutia kwa kucheza kwa kiwango cha juu.


Lakini pia, huu ni wakati mwafaka kwa wafanyabiashara kutumia fursa hii kuweza kujiingizia kipato kwa ujio wa timu hiyo kwa kuwa tunaamini wageni wengi watamiminika kutoka ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya mchezo huo.

Hatutarajii kuona Watanzania wakizubaa na kujikuta wakipigwa bao na wafanyabiashara kutoka nje kama ambavyo mfanyabiashara kutoka Uganda alivyoweza kujiingizia kipato kikubwa kupitia msiba wa Mwenyekiti wa IPP, Regnald Mengi, na kuwaacha wakishangaa.

Mwisho tunaomba amani, utulivu na ustaarabu utawale katika kipindi chote wageni hao wakiwa nchini ili kuendelea kuitangaza nchi yetu kama kisiwa cha amani duniani kama ambavyo imekuwa ikifahamika. Kila kheri Simba katika mechi hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Lipuli ina cha kujifunza kutoka kwa Watford

Na Adam Fungamwango

**JUMAMOSI** iliyopita dunia ilishuhudia fainali ya Kombe la FA nchini England, wakati Manchester City ikiisulubu bila huruma Watford kwa mabao 6-0 kwenye Uwanja wa Wembley. Ni mechi ambayo iliwaacha hoi watu walioikuwa wanaitazama, maana ilifika wakati ikaonekana kana kwamba Man City inacheza mazoezi na si mechi ya fainali.

Kwenye vibanda umiza nako hakuishiwi maneno, watu wakaanza kuulizana timu ile iliingiaje kwenye fainali, hali ya kuwa imeonekana ni dhaifu sana. Wengine wakazikumbuka timu kadhaa za England ambazo tayari zimeshatolewa kuwa kama zingetinga fainali basi zingeipa kazi sana Man City.

Wengine wakasema Watford ilipata bahati ya kutokutana na timu ngumu, lakini baadhi wakapinga na kusema England timu zote ni ngumu, ila ilikuwa ikikomaa na kuzikamia baadhi ya timu na kufika hapo ilipofika.

Vyovyote itakavyokuwa, lakini ni fainali iliyoboa, ambayo wengi hawakuitarajia kuwa itaisha kama ilivyoisha. Ni kweli England kwa sasa Man City ni timu ya kuogopesha ukikutana nayo, lakini kwa hali ilivyokuwa ilisikitisha. Man City, ilicheza inavyotaka. Ikatawala mpira ilivyotaka, wachezaji wakacheza wanavyojisikia, wakafunga mabao wanavyotaka, huku Watford wakionekana kukimbikiakimbia tu kama swala wanaokimbia mwituni wakisalimisha maisha yao yaliyokuwa hatarini dhidi ya mnyama Simba.

Nikaanza kuwaza fainali ya Kombe la FA la Tanzania ambayo inatarajiwa kupigwa Juni Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi kati ya Azam na Lipuli.

Wengi wanauchukulia kama utakuwa ni mchezo mgumu kutokana na njia ngumu aliyopitia Lipuli hadi kufikia fainali.

Moja kati ya njia ngumu ni kukutana na Yanga ambayo tayari uelekeo wake wa ubingwa wa Tanzania Bara ulikuwa tayari umeshapotea, hivyo njia pekee iliyobaki kwao ni kutwaa Kombe la FA kwa ajili ya kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao.

Hilo halikufanyika kwani Lipuli, kwa namna ambayo haikutegemewa na wengi iliichapa Yanga mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Samora na kuzima ndoto zao, huku yenyewe ikiweka rekodi ya kutinga hatua hiyo kwa mara ya kwanza kwenye historia ya klabu hiyo.

Lakini wakati kila mmoja anauchukulia kuwa utakuwa mchezo mgumu, Lipuli ikifanya masihara inaweza ikajikuta ikiwa kama Watford na fainali ikawa nyepesi kwa Azam.

Ni kwamba wachezaji wa timu hizi huwa wanacheza kwa bidii na juhudi kubwa wakicheza na klabu zenye wachezaji wenye majina makubwa na mashabiki wengi, lakini zinapokwenda kucheza na klabu zingine viwango vyao vinabadilika kabisa. Wachezaji wengi wa Kitanzania hawaichukulii Azam kama ni klabu yenye uwezo mkubwa na viwango vya hali ya juu kama ilivyo Simba au Yanga, badala yake huichukulia poa tu kwa sababu tu haina mashabiki wengi. Hicho ndicho kinaweza kuigharimu kabisa Lipuli. Makocha wa Lipuli wakiongozwa na Selemani Matola wanapaswa wawe makini na wachezaji wao si kwenye ufundi tu, bali kuwatia morali na kuifanya mechi hiyo kuwa kali ya kusisimua kama inavyotarajiwa kuwa.

Vinginevyo tunaweza kushuhudia fainali kama ile ya England ikawa rahisi mno kwa Azam na baadhi wakaanza kujiuliza Lipuli ilifikaje fainali.

Ikumbukwe kuwa Azam kwa muda sasa haijawakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa na haina nafasi yoyote kwenye ubingwa wa Ligi Kuu, hivyo bahati kama hii ya kufika fainali haiwezi kuja mara mbili, hivyo watakwenda wakiwa wamejizatiti ili kurudisha heshima yao, hivyo Lipuli inabidi iende kwa tahadhari na isije kukipata kichapo kama kilichomtokea kwa Watford.

# BARUA/MJADALA

## *Tuzingatie tahadhari tunazopewa, tuhame mabondeni*

**Ndugu Mhariri**

*NIMEJITOKEZA kama raia mwema wa taifa hili kutoa mchango wangu katika eneo ambalo ni la msingi katika ustawi wa Watanzania, kwa sababu linagusa shughuli zao za kila siku kwa njia moja au nyingine.*

*Ninasikitika kwamba ni eneo ambalo miaka nenda rudi, limekuwa likipigiwa kelele na watu wengi wenye mapenzi mema na hasa nyakati za masika ama za vipindi vya mvua nyingi kama vinavyoendelea katika Jiji la Dar es Salaam.*

*Lakini si kwa Jiji tu la Dar es Salaam, pia kwa maeneo karibu yote ya ukanda wa Pwani kwa maana ya Tanga, mkoa wa Pwani wenyewe, Lindi na Mtwara na kwa mujibu wa vyombo vya habari, ni karibu nchi nzima.*

*Nimejitokeza kuzungumzia tatizo moja ambalo linagusa mambo mawili kwa maana ya usalama wa watu lakini pia afya zao.*

*Tatizo hili linawahusu watu wanaoendelea kuishi maeneo ya mabondeni ambao ndio waathirika wakuu. Ni waathirika wakuu wa madhara yatokanayo na wingi wa mvua za masika ama zinazoletwa na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyojitokeza sasa kufuatia mvua ambayo imenyesha kwa takribani siku ya nane sasa.*

*Mhariri kwa miaka mingi kwa mfano katika Jiji la Dar es Salaam, watu wanaoishi katika Bonde la Mto Msimbazi, yale ya Magomeni, Jangwani, Mkwajuni, na Kigogo wameaswa kuyahama maeneo hayo.*

*Wameaswa kuhama maeneo hayo kutokana na ukweli kuwa mafuriko ambayo yamekuwa yakijitokeza si kwamba yameleta athari za vifo kwa wanaong'ang'ania kuendelea kuishi katika maeneo hayo, bali pia athari za kiafya na mali zao. Mbali na vifo, baadhi ya watu wamepoteza vifaa vya ndani, lakini mwishowe wamekumbwa na magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, pamoja na malaria.*

*Magonjwa ya kupindupindu kwa sehemu kubwa huyakumba maeneo haya kutokana na tatizo lingine la wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, ambao baadhi yao hutumia kipindi hiki kufungulia maji ya vyooni wakiyaelekeza kwenye bonde hilo.*

*Wakati umefika sasa Mhariri kwa Watanzania na hasa wanaoishi maeneo ya mabondeni kurejesha fahamu zao katika mstari na hivyo kuhama kwenye maeneo hayo kama ambavyo serikali ikielekeza kwa muda mrefu na wapenda maendeleo wengine. Hiyo ni kwa ustawi si wa waathirika peke yao, bali pia kuokoa rasilimali za nchi zinazotumika kuwahudumia wanapokumbwa na majanga hayo.*

**Raia Mwema, Dar**


**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz


# Si Mafisango tu, Tindwa pia akumbukwe Simba




**Na Adam Fungamwango**

ITAKUWA ni Mei 30, klabu ya Simba itakapofanya hafla ya utoaji tuzo kwa wachezaji, viongozi, wanachama na mashabiki wake kwenye Hoteli ya Hyatt Regency iliyopo jijini Dar es Salaam.

Huu utakuwa ni msimu wa pili kwa tuzo hizo zinazojulikana kama Tuzo za Mo, zilizoanza kufanyika mwaka jana.

Zilianzishwa kwa lengo moja la klabu kutambua mchango wa watu wote wa familia ya soka kwenye klabu hiyo kongwe ya Simba.

Kwa upande wa wachezaji wanaowania ni James Kotei, Mzamiru Yassin na Jonas Mkude kwa kipengele cha kiungo bora wa mwaka 2019, John Bocco, Meddie Kagere na Emmanuel Okwi wao wakishindana kwenye kipengele cha Mshambuliaji Bora wa Mwaka, pia kwenye kipengele cha Mchezaji Bora wa Mwaka wamo John Bocco, Meddie Kagere na Clatous Chama.

Upande wa makipa, Aishi Manula anashindana na msaidizi wake Deogratius Munishi 'Dida', wanaoshindana kwenye Beki Bora wa Mwaka ni Erasto Nyoni, majeruhi Shomari Kapombe na Paschal Wawa na kwenye kipengele cha Mchezaji Chipukizi wameshindanishwa Rashid Juma, Adam Salamba na Paul Bukaba.

Kuna wachezaji pia wanaowania tuzo la Goli Bora la Mwaka, ambao ni Claotus Chama, Meddie Kagere na John Bocco.

Tuzo zikitoka huko zinahamia kwa viongozi wa klabu pamoja na wadau wengine, hizo zinaitwa tuzo za heshima.

Hizo hupatiwa watu walioifanyia makubwa klabu hiyo huko nyuma, waliojitolea jasho, nguvu na hata uhai wao kwa ajili ya klabu. Tuzo hizi zinawajumuisha wachezaji, viongozi, wanachama au mashabiki, wawe hai au wamefariki dunia. Mwaka jana tuliona tuzo ya shabiki bora wa mwaka ikienda kwa shabiki mwanamama marehemu Fihi Salehe Kambi ambayo ilichukuliwa na mwakilishi wake.

Wakati zimebaki siku chache kabla ya tuzo hizo kutolewa, klabu ya Simba inapaswa iwe na kumbukumbu ya baadhi ya wachezaji na mashabiki wake wa nyuma ambao wameshawahi kufanya mambo makubwa kiasi cha kupoteza uhai wao kwa sababu ya klabu hiyo.

Ni kwa sababu tu Watanzania, hasa kwenye tasnia ya michezo, si Shirikisho la Soka nchini (TFF), wala klabu zenye tabia ya kutunza kumbukumbu za wachezaji au matukio ya miaka ya nyuma ili kuwa kama kielelezo au funzo kwa kizazi kijacho.

Mfano kwa sasa wengi wanasema kuwa aliyekuwa kiungo mahiri wa klabu hiyo marehemu Patrick Mafisango apewe tuzo maalum ya heshima, lakini Simba wanapaswa warudi nyuma wakumbuke kuwa kulikuwa na mchezaji aliyeitwa Hussein Tindwa aliyefia uwanjani akiwa amevaa jezi ya klabu hiyo.

Mafisango alifariki Mei 17, mwaka 2012 jijini Dar es Salaam kwa ajali ya gari akiwa mchezaji wa Simba, Tindwa alianguka akiwa uwanjani mwaka 1979 wakati Simba ikicheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Racca Rovers ya Nigeria jijini Dar es Salaam, akafariki dunia akiwa na jezi ya Simba mwilini.

Hawa ndiyo mashujaa wa kukumbukwa ambao hawasemwi wala habari zao kutajwa na naishauri Kamati ya Tuzo angalau ingalie ni jinsi gani na kufanya ili Tindwa naye apate tuzo yake kwa sababu afadhali Mafisango anazungumzwa na kizazi cha sasa, lakini beki huyo wa kati aliyekuwa akiinukia ni kama historia na Simba yenye kama vile haimtendei haki.

Kwenye upande wa shabiki bora, pamoja na kuwa na shabiki bora wa mwaka, lakini tuzo nyingine maalum ingekwenda kwa shabiki ambaye, ingawa wenye Simba huwa hawaielezei, sana, lakini mitaani inazungumzwa sana na mashabiki wa soka hasa wa miaka ya nyuma.

Mwaka 1974, baada ya Simba kufungwa mabao 2-1 na Yanga, Uwanja wa Nyamagana, mechi ambayo ilikuwa inaelekea Simba kupata ushindi, lakini mahasimu wao walisawazisha dakika ya majeruhi na baadaye kupata bao la pili, simulizi zinadai kuwa kuna shabiki mmoja huko Mwanza alijirusha kwenye pipa la maji na kufariki.

Viongozi wa Simba walipaswa wawe wanafanya utafiti na kujua alikuwa ni nani na familia yake au ndugu zake wako wapi kwa sasa.

Simba ikitoa tuzo kwa shabiki kama huyu, itakuwa ni faraja hata kwa familia au ndugu zake na kuona kuwa alichofanya ndugu yao enzi zile ni kitu cha kishujaa kwani amekumbukwa na kuenziwa.

Kwa haya yote, ni kwamba kuanzia sasa klabu zetu zianze kukusanya rekodi na historia ya matukio yote yaliyotokea huko nyuma na kuyaweka kwenye maandishi na pia ziwe na maktaba ya kuonyesha matukio na watu muhimu waliofanya makubwa na kusababisha klabu hizi zisimame hadi leo hii kuwa kubwa na kupendwa na watu wengi nchini.

## KABWELA — NA FADHIL MOHAMMED



# Viongozi wa kanisa wakumbwa tuhuma nzito

INATOKA UK. 2

zi wa mali, mapato na matumizi ya kanisa hilo.

"Kati ya maeneo yanayotuhumiwa kwa ubadhirifu ni viongozi wa EAGT kuingiza magari kwa jina la EAGT wakati magari hayo yanatumiwa na watu binafsi, hivyo kuikosesha serikali mapato," ilieleza sehemu ya barua hiyo.

**WANACHOTAKA WACHUNGAJI**

Wachungaji hao pia wameiomba Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru), TRA, Jeshi la Polisi, taasisi nyingine husika za serikali zichukue hatua za kuchunguza ili kuweka mambo bayana na kuwezesha hatua kali kuchukuliwa ili iwe fundisho kwa wanaofanya ufisadi makanisani.

Wakiongozwa na Makamu wa Askofu Mkuu wa EAGT, Dk. John Mahene, wanajipanga kufungua kesi wakisimamiwa na kampuni ya uwakili ya Giraffe Attorneys.

Wakili Sylivester Sebastian, mmoja wa mawakili wa kampuni hiyo anayeshughulikia hatua za ufunguaji wa kesi hiyo, ameliambia gazeti hili kuwa wachungaji hao wamepata fedheha baada ya kubaini taasisi yao imekuwa ikitumiwa vibaya na baadhi ya viongozi.

Sebastian alisema kwa sasa wachungaji watatu ambao aliwataja kuwa ni Yared Lesilwa wa Dodoma, Mchungaji Paul Alphonce Kapama na Mchungaji Francis Weja, wote wa Dar es Salaam, wameshapeleka maombi yao Na. 54/2019 Mahakama Kuu ya Tanzania.

Alisema lengo ni kuomba idhini ya Mahakama kufungua kesi hiyo kwa niaba yao na kwa niaba ya wenzao 543.

"Maombi hayo, yapo mbele ya Jaji Leila Mgonya na yatatajwa Juni 3, mwaka huu, kwa ajili ya kusikiliza mapingamizi ya wajibu maombi," alisema Sebastian.

Wakili huyo alibainisha kuwa awali wachungaji hao waliomba na kupewa idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo ilitolewa Oktoba 22, 2018 ili waweze kufungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania dhidi ya wadhamini wa EAGT kwa mujibu wa kifungu Na. 67 cha Sheria ya Mienendo ya Masuala ya Madai Sura Na. 33. Marejeo ya 2002.

Wachungaji na waumini wa EAGT, wanalalamika kutokuwapo na mkaguzi wa ndani wa fedha za EAGT kama Katiba yao ya 2011 inavyotaka.

Alisema kwa mujibu wa Katiba, viongozi walitakiwa kila baada ya miaka miwili waitishe mkutano mkuu wa kawaida na watoe taarifa kuhusu fedha za EAGT, pamoja na miradi, lakini hawafanyi hivyo.

"Vikao vinavyoitishwa na viongozi hao ni vya dharura pekee ambavyo vyote vimekuwa havina tija, bali vikiwa na malengo ya kupitisha mambo wanayotaka viongozi na si vinginevyo," alisema. Wakili huyo alibainisha kuwa aidha wachungaji wanalalamika kuhusu taarifa za miradi ya EAGT kutokuwa wazi ikiwa taasisi hiyo ni ya dini na lengo lake ni ustawi wa jamii na si kufanya biashara au kutafuta faida kwa viongozi.

Wachungaji na waumini wa EAGT, wanategemea kuiomba Mahakama kutoa fasiri kuhusu taasisi hiyo kutokuwa na ofisi zake kwa mujibu wa sheria.

"Wanadai hadi sasa ukitaka kumuona Askofu Mkuu unamkuta Dodoma, Makamu Askofu Mkuu yupo Mwanza, Katibu Mkuu yupo Arusha na Mhazini Mkuu yupo Dar es Salaam.

Mchungaji Lesilwa alibainisha kuwa kama Mahakama Kuu itakubaliana na maombi yao, basi watafungua kesi na kudai mambo kadhaa ambayo wadhamini pamoja na viongozi waandamizi wa EAGT walishindwa kutolea ufafanuzi kwa wachungaji kwa mujibu wa Katiba ya EAGT, 2011.

Aliyataja baadhi ya mambo wanayohitaji kupata ufafanuzi ni uwapo wa TIN namba tano kwa kutumia jina la EAGT au majina yanayofanana/kuelekeana na taasisi hiyo.

"TIN hizo zote zimekuwa zikiingiza magari na pikipiki nchini kwa kutumia taasisi ya EAGT, na kwa msamaha wa ushuru wa forodha, lakini ukweli ni kuwa magari hayo na pikipiki hizo hazipo ndani ya umiliki wa EAGT hadi sasa na hazijulikani ziko wapi," alidai.

TIN namba hizo zilizosajiliwa TRA zimetajwa ni No. 1000932326 ambayo inasomeka kwa jina la Temeke Evangelistic Assembiles of God.

Nyingine ni 103600766 kwa jina la Evangelistic Assemblies of God (T) na Tin No. 114558796 kwa jina la Evangelistic Assemblies of God Tanzania.

Mchungaji Lesilwa alitaja TIN namba nyingine ni 101060063 inayosomeka kwa jina la Evangelistic Assemblies of God CD na namba nyingine ni 103957200 kwa jina la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT).

Alisema wamelazimika kuomba ufafanuzi kutoka TRA wa TIN kwa kuwa wanatambua taasisi moja inapaswa kumiliki TIN namba moja, pia hakuna taarifa zinazoonyesha jinsi TIN hizo zilivyopatikana.

"Kinachowashangaza waumini na wachungaji wa EAGT ni kwa vipi EAGT imeonekana ikimiliki TIN zote hizo na ikiwa magari na pikipiki zilizoingizwa hazipo chini ya umiliki wa taasisi na wadhamini hawatoi maelezo yoyote juu ya jambo hili," alidai.

## Sababu za Zimamoto

INATOKA UK. 3

mmoja miaka miwili iliyopita.

"Watu hawa walifukuzwa kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya kufanya ukaguzi kwa wananchi na kisha kuwatoza tozo za juu tofauti na viwango vilivyowekwa," alisema.

Alisema licha ya watu hao kufukuzwa lakini wamekuwa wakiendelea kufanya kazi hiyo huku wakijitambulisha kuwa ni wafanyakazi wa jeshi hilo.

"Wanapokwenda kwa wananchi wanajifanya ni wafanyakazi wa Zimamoto. Mfano wanakwenda kwenye duka wanafanya ukaguzi, kama mhusika alitakiwa kulipa Sh. 30,000 wanamlipisha Sh. 100,000. Mbali na hili wamekuwa wakighushi vyeti na kuwapa wateja visivyo na muhuri wala sahihi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji," alisema.

Alisema jeshi limeamua kuwatangaza kutokana na kuwa na kasi kubwa ya kuwaendea wateja na wamekuwa wakifanya hivyo kwa kwenda wawili au watatu.

"Imefikia hatua watu hawa ili kujiaminisha kwa wananchi bado ni wafanyakazi wa jeshi wametengeneza vitambulisho vya kughushi, tunaomba wananchi wawe makini," alisema.

## Nyumba kupigwa mnada

INATOKA UK. 2

"Tuna kazi ya kukusanya madeni na kuuza nyumba za wateja walioshindwa kulipa mikopo benki zaidi ya 10, kama NBC, KCB, Barclays na CRDB. Tunauza nyumba Mwanza, Morogoro, Zanzibar na maeneo mengine.

Nyumba ya aliyewahi kuwa Waziri wa serikali ya awamu ya tatu na nne, Dk. Batilda Burian, iliwekwa sokoni baada ya kudaiwa kushindwa kurejesha mkopo anaodaiwa benki.

Nyumba hiyo ilikuwa ipigwe mnada Juni 9, mwaka jana, kwa niaba ya Benki ya Equity Tanzania baada ya Dk. Batilda aliyekuwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kushindwa kulipa deni.

Lakini baadaye Kampuni ya udalali ya Magwembe iliyotangaza kuuza nyumba hiyo ilisema haikuuzwa kwa sababu mwenyewe amejitokeza na kuikomboa.

"Mmiliki aliongea na benki akalipa kiasi cha fedha na wakakubaliana kuongezewa muda zaidi wa kulipa deni ili nyumba hiyo isipigwe mnada kama tulivyokuwa tumepewa kazi na benki," alisema ofisa mmoja wa kampuni ya udalali.

Juni mwaka jana, nyumba 85 na magari zaidi ya 10 ya wakopaji wa benki nne nchini, ziliwekwa katika mnada wa hadhara baada ya wakopaji kushindwa kurejesha mikopo waliochukua kwa dhamana ya mali hizo.

Kwa mujibu wa matangazo ya kampuni za udalali ndani ya siku 57 tangu Aprili 20, mwaka huu, na kampuni zilizopewa kazi ya kuendesha mnada kwa niaba ya benki hizo, wakopaji hao walipewa muda wa siku saba kulipa madeni yao vinginevyo mali zao zitauzwa kwa mnada wa hadhara.

Katika tangazo la Mei 23, mwaka jana nyumba 21 na magari sita yalitangazwa kupigwa mnada na nyumba nyingine 20 na magari manne zilitangazwa kwenye tangazo lingine.

## Korosho, Masele kutikisa Bunge

INATOKA UK. 3

huyo wa Viwanda na Biashara amekuwa akiomba rushwa kwa wawekezaji.

Wiki iliyopita, wabunge mbalimbali wa upinzani waliwataka mawaziri walioshiriki mchakato wa serikali kuingia mkataba na Kampuni ya Indo Power Solutions ya Kenya kununua korosho nchini, kujiuzulu kutokana na kile walichoeleza kuisababishia serikali hasara ya Sh. trilioni 1.18.

Awali, upinzani ulimtaka Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki, Prof. Palamagamba Kabudi, kuwajibika kwa kile ulichodai alikuwa kinara katika mchakato wa serikali kuingia mkataba na kampuni hiyo ya Kenya.

Hata hivyo, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alilieleza Bunge kuwa mawaziri wanawajibika kwa pamoja, hivyo kama kuna dosari ilitokea mahali ni kwa mawaziri wote.

Kutokana na kauli hiyo ya Dk. Mwakyembe, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche (Chadema), alisema bungeni Ijumaa iliyopita kuwa serikali nzima inapaswa kuwajibika kwa kile alichokiita kulitia aibu taifa kwa kuingia mkataba na kampuni ambayo haina uwezo wa kununua kiasi hicho kikubwa cha korosho nchini (tani 100,000).

Leo wakati wa kuhitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha, serikali inatarajiwa kujibu hoja hiyo ya upinzani bungeni.

Hata hivyo, hoja ya kumtaka Prof. Kabudi kuwajibika inatarajiwa kuibuka tena Jumatatu ijayo wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha. Upinzani umekuwa ukimtuhuma mtaalamu huyo wa sheria kwamba ameishauri vibaya serikali katika mambo mbalimbali ya kisheria likiwamo sakata la makinikia na utungaji wa sheria mbalimbali.

**HATIMA YA MASELE**

Wiki iiyopita, Spika Ndugai aliagiza Masele kurejea nchini akitokea Afrika Kusini alikokuwa anashiriki vikao vya PAP ili ahojiwe na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge huku akiweka wazi kuwa hata Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) pia inamsubiri mbunge huyo ambaye mwaka 2010 alishinda ubunge kwa tofauti ya kura moja.

Spika Ndugai alitangaza uamuzi wa kusimamisha uwakilishi wa mbunge huyo PAP akimtuhumu kupeleka maneno ya uongo kwenye mhimili wa juu serikalini na kukaidi wito wa Spika.

Tayari kiongozi huyo wa Bunge la Tanzania ameshaweka wazi kuwa iwapo Masele hataitikia wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maadili leo saa tano asubuhi, atafikishwa bungeni kwa pingu.

**TUHUMA RUSHWA KWA WAZIRI**

Ijumaa jioni, wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mbunge wa Ndanda, Mwambe, alisema anatamani awe Naibu wa Viwanda na Biashara akidai anayeshika nafasi hiyo kwa sasa (Manyanya) ameshindwa kazi.

Mwambe alimtuhuma naibu waziri huyo kuwa amekuwa akilalamikiwa na baadhi ya wawekezaji kwamba anawaomba rushwa.

Kauli hiyo baadaye ilimwinua kitini Manyanya ambaye alikiomba Kiti cha Spika kumtaka Mwambe ama afute maneno au athibitishe ukweli wa tuhuma dhidi yake kwamba ni naibu waziri anayewaomba rushwa wawekezaji.

Baada ya kutakiwa na Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, kufuta maneno yake kama hana ushahidi, Mwambe alidai ushahidi anao na yuko tayari kukithibitishia chombo hicho cha kutunga sheria.

Baada ya Mwambe kudai kuwa na ushahidi wa kadhia hiyo, Chenge alimtaka mbunge huyo kuuwasilisha bungeni Jumatatu, yaani leo.

## Polisi, machinga hapatoshi

INATOKA UK. 3

Chongolo alisema mbali na kujenga barabara nne, eneo la Mwenge pia kutajengwa kituo cha daladala kitakachohudumia wakazi wa maeneo mbalimbali wa Jiji la Dar es Salaam.

Februari 28, mwaka huu Serikali ya Tanzania na Japan zilitiliana saini mkataba wa kuanza kwa ujenzi wa mradi wa upanuzi wa barabara ya New Bagamoyo awamu ya pili kuanzia eneo la Morocco hadi Mwenge, itakayokuwa na urefu wa kilomita 4.3, kwa gharama ya Sh. bilioni 73.6.

Utiajia saini wa upanuzi huo ulihusisha Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) na Kampuni ya International Division Dai Nippon Construction ya Japan, ambayo itajenga barabara hiyo kwa muda wa miezi 24.

Wakati wa makubaliano hayo, Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Mhandisi Patrick Mfugale, alisema mchakato wa upanuzi wa barabara hiyo ulianza mwaka 2008 ukihusisha ujenzi wa kilomita 17 za barabara kutoka MorAocco hadi Tegeta.

Alisema awali barabara hiyo ilijengwa urefu wa kilomita 12.7 kutoka eneo la Mwenge hadi Tegeta, hivyo kusainiwa kwa mkataba huo tena watamalizia sehemu ya mradi ambayo ni kilomita 4.3.

# Onyo wanaochezea pampu za mafuta

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

WAMILIKI wa vituo vya kuuzia mafuta mkoani Rukwa wameonywa kutojihusisha na kuchezea pampu za mafuta kwa lengo la kuwaibia wateja na atakayebainika kufanya hivyo atafikishwa mahakamani.

Onyo hilo lilitolewa jana na Kaimu Meneja wa Wakala wa Vipimo mkoani humo, Hassan Mrisho, wakati akikagua vituo vya mafuta vya mjini Sumbawanga katika maadhimisho ya Wiki ya Vipimo Duniani.

Alisema wapo wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta ambao wana tabia ya kuzichezea pampu za mashine za kuuzia mafuta ili zitoe mafuta kwa kiasi kidogo kwa lengo la kuwaibia wateja wao, na kwamba kitendo hicho ni kosa la jinai na atakayebainika atafikishwa mahakamani.

Mrisho alisema wakala wa vipimo mkoani humo umekuwa na utaratibu wa kufanya ukaguzi mara kwa mara katika pampu hizo ili kubaini muuzaji ambaye ana mchezo huo kwa lengo la kuwalinda wanunuzi wa mafuta ili waweze kupata kiasi cha mafuta kwa thamani ya fedha waliyotoa.

Alisema hivi sasa wapo katika ukaguzi maalumu kwa kuwa wanaadhimisha Wiki ya Vipimo Duniani na kilele chake kitakuwa leo, hivyo watahakikisha wanawafikia wamiliki wote wa mafuta ili kuzikagua pampu hizo na kujua ubora wake.

Alisema wanawasaidia kwa kuhakikisha wateja hawawakimbii kwa kuwa mteja anapokwenda kupata huduma na akiridhika itasaidia kurudi mara kwa mara kwa kuwa atakuwa na uhakika na mafuta anayonunua.

Naye Meneja wa kituo cha kuuzia mafuta cha Munio Filling Station, Hassan Miraj, alisema kuwa wao wanaufurahia ukaguzi huo kwa kuwa pia wakala wa vipimo wanaweka stika maalumu ambayo inamtambulisha mteja kuwa wamekaguliwa na wako salama.



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Yamungu Kayandabila, akizindua kanuni za kutoa huduma za bima kupitia benki jijini Dar es Salaam, huku wageni wengine wakishuhudia. Uzinduzi huo uliandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA) kwa kushirikiana na BoT. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIRA yazindua kanuni za bima kupitia benki

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA) kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), zimezindua kanuni za kutoa huduma za bima kupitia benki.

Akizindua rasmi kanuni hizo jijini Dar es Salaam, Naibu Gavana wa BoT, Dk. Yamungu Kayandabila, alizitaka taasisi za fedha na benki nchini kuzingatia katika kutoa huduma zao ili kuongeza ufanisi wa shughuli zao.

Alisema kanuni hizo zitasaidia kusambaza huduma ya bima nchini kwani watu wengi bado hawajafikiwa.

"Ujio wa kanuni za kutoa huduma za bima kupitia benki nchini umechelewa kidogo, hivyo wadau wana kila sababu ya kuzingatia kwa manufaa ya pande zote watoa huduma na wanufaika," alisema.

Alisema endapo wadau watazizingatia kanuni hizo, mapato katika sekta hiyo kiujumla yataongezeka kwa taifa, watoa huduma na watu wengi zaidi watafikiwa na huduma za bima.

Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alisema licha ya manufaa lukuki ya uzinduzi wa kanuni hizo, pia unalenga kuendeleza ajenda ya TIRA ya kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima nchini yaani bima kwa wote.

"Tunahitaji kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za Bima (access) nchini kwa kuongeza aina mbalimbali za bima kwa mahitaji mbalimbali, mfano mbadala wa uuzaji na usambazaji wa huduma za bima ikiwamo kutumia benki," alisema.

Kamishna huyo aliongeza kuwa inahitajika teknolojia rahisi na rafiki kwa ajili ya kusambaza bima, kununua bima, kuuza bima, kulipa mafao/madai ya bima, kusikiliza maoni na mahitaji ya wananchi, kuchakata na kuandikisha maombi ya bima," alisema Dk. Saqware.

Aliongeza kuwa kuanzishwa kwa kanuni hizo ni muhimu katika kuendeleza sekta ya kifedha nchini na kusisitiza kuwa pato la taifa, hasa ukizingatia faida nyingi ambazo zitapatikana kwa benki zenyewe na watumiaji wa huduma za bima.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali serikalini, kampuni za bima, taasisi za kifedha, mawakala mbalimbali na wadau wa sekta ya bima na kudhaminiwa na BoT, Reliance Insurance, Heritage Insurance, Zanzibar Insurance, Chama cha Watoa Huduma za Bima (ATI), NMB, CRDB Insurance, Metropolitan Life Tanzania, Jubilee Insurance, FSDT, Stanbic Bank, Smart Policy, Alliance Insurance, TPB Bank na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

# Wateja Vodacom wapewa unafuu wa usajili simu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA zoezi linaloendelea la usajili wa simu kwa alama za vidole, wateja wa kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania Plc, sasa wanaweza kusajili sehemu yeyote waliyopo nchini.

Uamuzi huo unatokana na kampuni hiyo kugawa mashine za usajili 8,000 kwa wakala huru wanaozunguka mitaani.

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni hiyo, Jacquiline Materu, alisema jana kuwa pamoja na kuwa na maduka yapatayo 100 na madawati ya huduma kwa mteja 350 yanayofanya usajili kwa kutumia alama za vidole, kampuni hiyo imewapa vifaa watoa huduma wengine zaidi.

"Tumetoa mafunzo na vifaa kwa mawakala huru (Freelancers) ili kuongeza juhudi za uandikishaji kwa wateja wetu popote pale walipo," alisema Materu akiongeza kwamba hii ni katika kuendana na kasi ya serikali katika kutekeleza agizo la kusajili wateja wote wa huduma za simu za mkononi.

"Tunawathamini wateja wetu na muda wao na ndio maana sambamba na kuongeza vifaa na wafanyakazi madukani kwetu, tumeamua pia kuwatumia mawakala huru wanaozunguka ili kuwasogezea huduma za usajili wateja wetu ambao hawataweza kufika madukani kwa sababu za kikazi, kiafya au nyinginezo," alisema.

Akizungumzia zoezi la usajili linaloendelea, Mkuu wa Kanda ya Kati wa kampuni ya Vodacom, Grace Chambua, aliwashauri wateja wa kampuni hiyo hasa walioko katika mji wa serikali wa Mtumba jijini Dodoma kujitokeza ili kupata huduma ya usajili kwa wakati.

Mteja wa kampuni hiyo aliyemaliza usajili huu mpya, Mohamed Amiri, alisema: "Sikukuta foleni na huduma ilikuwa ya haraka mno, ndani ya dakika tatu nilikuwa nimeshamaliza usajili wangu mpya, nimefurahi sana kwa huduma hii."

Kwa mujibu wa maagizo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), wananchi wote wenye simu za mkononi wanatakiwa kufanyiwa usajili mpya kwa kutumia alama za vidole.

# Watia nia uchaguzi wa 2019/20 wapewa angalizo

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

WATIA nia ya kugombea nafasi mbalimbali kwenye chaguzi wa 2019/2020 wametahadharishwa na fedha chafu kwenye kampeni.

Wameonywa kwa matumizi ya aina hiyo licha ya kuwaingiza katika kashfa, pia zitawafanya washindwe kutimiza wajibu na majukumu yao ya kuwatumikiwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana na mwezeshaji, Dk. Ally Fungo, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake na vijana katika kushiriki shughuli za kisiasa ikiwamo kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi zaliyofanyika mjini Korogwe.

Katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Tanzania Youth Coalition (TYC) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), Dk. Fungo, aliwataka washiriki hao wanapogombea nafasi za uongozi watumie mbinu za ushawishi uliyo halali na kuepuka vikwazo vikiwamo kutumia fedha chafu kwenye kampeni zao.

"Mambo mengine ya kuzingatia wakati wa kuomba ridhaa kwa wananchi ni kuwa na takwimu sahihi, uhakika kwa unachokizungumza ili kuepuka ubabaishaji, utengaji muda wa kutosha wa kujieleza na kujibu maswali pamoja na kujiridhisha na fedha utakazozitumia kwenye kampeni zako," alisema Dk. Fungo.

Alitoa angalizo kwa wagombea kufanya kampeni kwa fedha za mikopo ili kuepuka fedheha pindi wanapokosa nafasi wanazoomba na kusisitiza umuhimu wa mgombea kuweka mpangilio mzuri katika kuzungumza.

Alisema lazima mgombea awe mkweli na muwazi, na kutumia lugha nyepesi wanapofanya mikutano ya kampeni ili kueleweka vema na wananchi.

Awali mratibu wa mradi huo, Yahaya Kitogo, alieleza lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kutengeneza ujumbe unaowashawishi wapigakura, kuelewa njia bora za kufikisha ujumbe kwa jamii, kuelewa jinsi ya kufanya kampeni yenye mafanikio, kujifunza mbinu za ushawishi na kujifunza namna ya kupata msaada wa hali na mali.

Kitogo alieleza kuwa mradi wa Women Youth Political Representation (WYPRE) unaendesha mafunzo hayo katika wilaya nne za Mkoa wa Tanga ambazo ni Lushoto, Muheza, Handeni na Korogwe na kwamba kuna zaidi ya washiriki 60 kutoka kwenye wilaya hizo.




Baadhi ya wateja wakinunua bidhaa katika duka la GSM Pugu Mall jijini Dar es Salaam, kwa ofa maalum ya msimu huu wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani yaani 'Danube Ramadhani Special offer'. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Madereva wa malori walia foleni bandari Dar

**Na Enock Chaulema**

MADEREVA wa malori wamelalamikia foleni ndefu katika bandari ya Dar es Salaam iliyodaiwa kutokana na mfumo wa uendeshaji wa bandari hiyo, kutoka kwa uongozi wa bandari wanapofanyiwa ukaguzi katika mashine za kukagua mizigo inayotoka ama kuingia ili kubaini kama ina taarifa sahihi ama la.

Kwa mujibu wa madereva hao, ukaguzi huo umekuwa ukichukua muda mrefu jambo linalosababisha kuwe na foleni ndefu bandarini hapo na hivyo kupoteza muda ambao ungeweza kutumika katika shughuli zingine.

Akizungumza na gazeti hili mmoja ya madereva hao aliyejitambulisha kwa jina la Hamisi Dongo, alisema wamekuwa wakilazimika kukaa kwa muda mrefu katika foleni kutokana na ukaguzi mbalimbali unaofanyika bandarini hapo na hivyo ameiomba serikali kuangalia upya namna bora ya kufanya ukaguzi ili kurahisisha na kuokoa muda.

"Kwa kweli muda tunaopoteza hapa hata serikali ingetufikiria, ukiangalia muda unaotumika kukagua gari moja kuanzia kule kwenye mzani dakika 40 hadi 50, ukija hapa sasa ndio shida zaidi mara nyingine tunaambiwa mashine hazisomi sasa tunaiomba serikali itufikirie," Dongo alisema.

Naye dereva mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Dafa, alidai kuwa mzani uliopo katika geti namba 12 bandarini hapo ni chanzo kikubwa cha foleni na hivyo ameishauri serikali kuangalia mahali pengine pakuweka mzani huo, ili kupunguza foleni kwa kuwa barabara hiyo licha ya kutumiwa na magari yanayoingia na kutoka bandarini pia hutumiwa na magari mengine yakiwamo ya abiria na yale ya watu binafsi.

"Huo mzani hapo ni chanzo cha foleni ukizingatia hii barabara inatakiwa kutumika na watu wengi kuna magari ya abiria hapa na magari ya watu binafsi mie naona pangetafutwa mahali pengine pakuwekwa huu mzani badala ya kuuweka hapo," Dafa alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko, alipotafutwa kuzungumzia hali hiyo hakupokea simu na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi haukujibiwa.

# Sheria ndoa yamkwaza mtendaji kata

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHERIA ya Ndoa ya mwaka 1971 imedaiwa kuwa kikwazo katika kutokomeza tatizo la mimba na ndoa za utotoni wilayani Kishapu Mkoa wa Shinyanga kutokana na kuwa moja ya kinga dhidi ya watuhumiwa ambao wamekuwa wakikamatwa kuhusika na matukio hayo kushindwa kufungwa jela.

Hayo yalibainishwa juzi na Mtendaji wa Kata ya Kishapu wilayani humo, Nunya Chege, kwenye kikao cha Shirika la Agape cha kuunganisha nguvu ya pamoja ya kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kilichohusisha watedaji wa kata, maofisa maendeleo ya jamii, dawati la jinsia polisi, wanasheria, na mahakimu.

Alisema pale wanapokuwa wakiwakamata watuhumiwa wakifunga ndoa na watoto wadogo walio chini ya umri wa miaka 18, sheria hiyo ya ndoa inakuwa kinga kwao kwa kutoa tafsiri kuwa mtoto mwenye umri wa miaka 14-15, anaweza kuolewa kwa ruhusa ya wazazi au mahakama, hivyo kushindwa kuwatia hatiani.

"Naomba Sheria hii ya Ndoa ya mwaka 1971 ifanyiwe marekebisho ya haraka tofauti na hapo suala la kumaliza tatizo la mimba na ndoa za utotoni litakuwa ndoto... mimi binafsi inanikwaza, nimeshakamata watuhumiwa wengi tu, lakini kesi zao zote zinaishia njiani bila kutolewa hukumu sababu ya hii sheria," alisema Chege.

"Sasa hivi nikiletewa kesi inayohusu masuala ya mimba na ndoa za utotoni si shughuliki nayo hadi pale sheria hii ya ndoa itakapofanyiwa marekebisho," alisema na kuongeza:

"Sababu unajikuta unahaghaika, lakini hakuna mafanikio, mwisho wa siku unaanza kuingia uhasama na wananchi kwa kuonekana umekula rushwa."

Naye Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Octavian Kiwone, aliwataka viongozi wote wa serikali kuanzia ngazi ya kijiji kutokatishwa tamaa na sheria ya ndoa, bali waendelee kupiga vita vitendo hivyo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuacha kutongoza watoto wadogo na kuwaozesha.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Itilima wilayani Kishapu, Athumani Kitundu, naye alikiri sheria ya ndoa kuwa tatizo katika uendeshaji wa kesi zinazohusu mimba na ndoa za utotoni, kwa kuwa inakinzana na sheria zingine za ulinzi wa mtoto.

Ofisa Mradi wa Sauti ya Mwanamke na Mtoto kutoka Shirika la Agape, Felix Ngaiza, alisema mradi huo umelenga kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Kishapu, ambapo utatekelezwa katika kata tatu za Itilima, Bunambiyu na Kishapu kwa miezi sita.

# Mkakati watakiwa kudhibiti ukatili dhidi ya watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imetakiwa kuweka mikakati thabiti ya kupambana na ukatili wa watoto, ndoa na ajira za utotoni, ili kujenga taifa lenye kujali utu, maadili na ustawi kwa mtoto na taifa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Azimio la Arusha, Constantine Nyamabondo, kwenye maadhimisho ya Siku ya Makumbusho Duniani yanayoadhimishwa Mei 18 kila mwaka.

Alisema siku hiyo inaadhimishwa kwa mada mbalimbali na mwaka huu wamejadili ukatili dhidi ya watoto na ndoa za utotoni kwa mtoto wa kike, ili kuweka mikakati ya kukomesha tatizo hilo.

"Lakini tunaiomba serikali iweke mikakati kabambe kukomesha haya ili tuwe na taifa lenye kujaa maadili mema," alisema.

Alisema kimsingi mada hizo ni sehemu ya kupeleka ujumbe kwa jamii ya Watanzania na watu wote ulimwenguni kukumbuka na kujifunza ili watu warudi kwenye kujenga jamii yenye maadili na kuondokana na ukatili dhidi ya watoto.

Maadhimisho hayo wamefanya kwa kushirikiana na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati.

"Tunafahamu tunapojadili katika maadhimisho haya tunasaidia jamii kubadilika na hatimaye kumwezesha mtoto wa kike kupata elimu anayostahili badala ya kukimbizwa kuozwa," alisema.

"Maadhimisho haya kila mwaka huwa tunajadili masuala mbalimbali yanayozunguka jamii, baada ya kualika wananchi kutembelea makumbusho kujifunza historia, tunapata fursa ya kujadili kwa pamoja changamoto za kijamii kuweza kupaza sauti na kuzitokomeza," alisema Nyamabondo.

Awali akizungumza kwenye maadhimisho ya siku hiyo Mkurugenzi wa Wanawake na Watoto KKKT, Faustina Millan, alisema jamii hususani wazazi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha watoto wanapata malezi sahihi, sambamba na elimu ya afya itakayowasaidia kufikia ndoto zao.

Millan alisema matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto yanatokana na tofauti baina ya wazazi, hivyo kuwataka wazazi kuondoa changamoto zao kabla hazijawakumba watoto, ili kuondokana na uvunjifu wa maadili kwenye jamii na malezi salama kwa watoto.

"Najua msingi wa maadili katika jamii hususani ya kiroho yanachangia kuwapo kwa hofu katika jamii na maadili kukua ila panapokosekana na kupungua kwa maadili, ndio tunaona changamoto za ukatili kwa watoto ikichagizwa na mila potofu kwa jamii zetu," alisisitiza Millan.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza wakati akitoa taarifa yake ya mwaka 2018 katika Mkutano Mkuu wa 24 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB, uliomalizika jana kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa AICC, jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbulu wapata ukombozi Baraza la Ardhi, Nyumba

**Na Cynthia Mwilolezi**
MANYARA

WANANCHI wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, waliokuwa wanafuata huduma ya Baraza la Ardhi na Nyumba wilayani Babati, wataondokana na tatizo hilo baada ya viongozi wa wilaya hiyo kupanga mikakati ya kuanzisha katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Joseph Mandoo, aliyasema hayo jana, wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo.

Mandoo alisema wameshapata jengo litakalokuwa linatumika katika mashauri mbalimbali ya baraza hilo litakalokuwa kwenye Kata ya Dongobesh.

Alisema baada ya jengo hilo kupatikana sasa wanajipanga ili lianze kutumika na wananchi waliokuwa wanakwenda mbali hadi Wilaya ya Babati kufuata huduma hiyo, sasa itakuwa karibu tofauti na mwanzo.

"Tutawachukua wazee wa baraza hilo kutoka kwenye kata mbalimbali za jirani ikiwamo Dongobesh, Tumati na nyinginezo kuliko kuwachukulia walio mbali na eneo ofisi ilipo," alisema Mandoo.

Hata hivyo, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Flatei Massay, alisema changamoto kubwa inayosababisha kutoanzishwa kwa baraza hilo ni watumishi hasa wapigachapa.

"Kama mkurugenzi angeweza kufanikisha tupate hata wapigachapa wa halmashauri, mashauri yangeanza kusikilizwa, ila muda siyo mrefu shughuli ya baraza hilo itaanza," alisema Massay.

Awali Diwani wa Viti Maalum wa Tarafa ya Dongobesh, Ester Joel (CCM), aliuliza swali juu ya jambo linalokwamisha uanzishaji wa shughuli za Baraza la Ardhi na Nyumba kwenye halmashauri hiyo.

Joel alisema hivi karibuni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliwateua wenyeviti wa wilaya wa mabaraza ya ardhi na nyumba wa wilaya, hivyo ofisi ya Mbulu nayo ianze kazi.

Mkazi wa kijiji cha Dongobesh, John Matle, alipongeza serikali kwa kufanikisha uanzishwaji wa baraza hilo, akisema wengi wanaofuata huduma hiyo mjini Babati wanalazimika kutumia gharama kubwa.

"Wengine walikuwa wanalazimika kulala Babati ili kusikiliza mashauri yao na gharama za kupeleka mashahidi nazo ni kubwa, ila kuwapo hapa Dongobesh itapunguza muda na gharama," alisema Matle.

# W'biashara waagizwa kulipa kodi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa Halmashauri ya Meru wilayani Arumeru, wametakiwa kulipa ada ya ushuru wa hudumu (Service Levy) ili kuleta maendeleo katika halmashauri hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, wakati akiongea na baadhi ya wafanyabiashara waliopo wilayani humo.

"Nataka wafanyabiashara wote mtoe kodi za huduma ili kuleta maendeleo katika halmashauri hii na nawasihi msijaribu kukwepa," alisema.

Muro alisema serikali inakusanya kodi ili kuzirejesha kwa wananchi kupitia mikopo ya asilimia kumi sambamba na kuwaletea wananchi miradi ya maendeleo.

Aidha, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Emmanuel Mkongo, kuhakikisha kila mfanyabiashara anayetoa huduma ya uuzaji mafuta (sheli), maduka makubwa na wengine wanalipa ushuru wa huduma.

"Unajua mnapolipa fedha hizi zinasaidia kufanya shughuli za kimaendeleo katika halmashauri zetu, pia napenda kuwaambia wale ambao wana madeni ya muda mrefu yaani waliolimbikiza madeni wakalipe mara moja ndani ya mwezi huu," alisema Muro.

Alisema katika hilo wanatoa muda wa mwezi mmoja kwa wafanyabiashara wa maduka makubwa, sheli, mahotel pamoja na wawekezaji kwenda katika ofisi ya mkurugenzi kuzungumza na kulipa fedha wanazodaiwa.

Muro alisema baada ya mwezi kwa yeyote ambaye hajalipa hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Kwa upande wake mmoja wa wafanyabiashara aliyejitambulisha kwa jina la Anna Shayo, alisema wamesikia agizo hilo na watakwenda kulipa kodi hiyo, ili wilaya hiyo iweze kufanya shughuli za kimaendeleo.

"Sisi nasi hatutaki kukwamisha shughuli za maendeleo, bali wote tunapenda kuona halmashauri yetu na taifa vinasonga mbele," alisema.

# Chuo cha Ualimu Moshi chalilia umeme

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKATI ulimwengu wa sasa wa utandawazi ukiwa unazilazimisha nchi zinazoendelea duniani kujikita katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), wanafunzi wa kozi ya ualimu katika Chuo cha Ualimu Moshi, kwao mambo ni tofauti.

Hayo yamo katika risala ya wanafunzi wa chuo hicho, waliyoikabidhi juzi kwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba-Moshi, James Silas, wakati wa mahafali ya tatu ya ualimu, ngazi ya cheti ya 'Grade IIIA yaliyowashirikisha walimu 175.

Katika risala yao iliyosomwa na Eliagape Godfrey, wanafunzi hao wameeleza masikitiko yao kuwa, licha ya chuo hicho kujitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kununua kompyuta za kutosha ili kufundisha walimu hao somo hilo, tatizo kubwa linalojitokeza na limekosa ufumbuzi ni kuunganishwa kwa nishati ya umeme.

"Changamoto kubwa tunayolia nayo na inatufanya tuachwe mbali na teknolojia katika utekelezaji wa majukumu yetu tutakapopangiwa shule za kufundisha katika nchi yetu ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Ukosefu wa umeme hapa chuoni umesababisha somo la Tehama kwa vitendo lisifanikiwe kutokana na kuwapo kwa kompyuta, lakini hazitumiki," alisema.

Ishara muhimu ya utandawazi ni ule uwezo wake wa kuyagusa maisha ya wanajamii wengi kwenye jamii anuwai katika nyanja za elimu, uchumi, siasa na utamaduni kwa jumla ambamo lugha hupata nafasi ya pekee.

Tehama ni somo lililoanzishwa katika mtaala wa Elimu ya Msingi (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2005). Somo hili linampa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari, vyombo vya mawasiliano na maktaba.

Akizungumza na walimu hao, Mwenyekiti huyo wa Baraza la Ardhi na Nyumba-Moshi, (James) aliwataka wahitimu hao kwenda kufanya kazi ya kufundisha kwa weledi na nidhamu."Msingi wa utumishi wa umma umejikita katika uadilifu, hivyo mtumishi wa umma ni lazima afanye kazi kwa weledi na nidhamu ya hali ya juu. Ualimu ni fani yenye heshima, wahusika wanatakiwa kwanza kujiheshimu wenyewe, hatutegemei atokee mtu kati yenu akajihusisha na ulevi wa kupindukia na kisha kufukuzwa kazi kwa aibu, haipendezi," alionya.

Kwa upande wake, Mkuu wa chuo hicho, Fredy Akyoo, aliishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa maelekezo wanayoyatoa na kusimamia utekelezaji wake pamoja na hasa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ambaye amekuwa akifuatilia mara kwa mara maendeleo ya chuo hicho na kutoa ushauri wa kukiboresha.



Waziri wa Nishati, Medard Kalemani, akiwahutubia wananchi wa kijiji cha Mpakani wilayani Muheza juzi, alipotembelea kukagua mradi wa umeme. Kushoto ni Mbunge wa Jimbo la Muheza, Adadi Rajabu na kulia ni Katibu wa CCM wilaya hiyo, Mohamed Moyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM MUHEZA**

# Atetea uamuzi wa JPM ujenzi wa reli ya kisasa

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ametetea uamuzi wa serikali ya Rais Dk. John Magufuli kuelekeza nguvu zake zaidi katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi mkubwa wa reli ya kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR), akisema maono hayo yangeweza kuichukua Tanzania hata miaka 50 mbele kufikia uwekezaji huo.

Kwa siku kadhaa sasa, kumekuwapo na minong'ono kutoka kwa baadhi ya wanasiasa na watumiaji wa mitandao ya kijamii, wakijadili na kuhoji ujenzi huo, badala ya kutekelezwa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Mkuu huyo wa wilaya ametetea uamuzi huo wa serikali akisema: "Faida zake kwa taifa letu kuanzia za kiuchumi ni kuwapo kwa gharama nafuu za usafiri, kuokoa muda, kuokoa barabara na kuongeza pato la taifa, lakini faida za kijamii ni pamoja na ajira, huduma kwa jamii na fahari kwa nchi na kisiasa ni kuonyesha nguvu ya hoja.

Hapa ndipo napozidi kuamini kuwa Rais wetu Dk. John Magufuli, si mtu wa kawaida. Ni kati ya watu wachache sana unaoweza kuwapata duniani."

Kwa maono yake, uamuzi wa serikali ni uamuzi wenye hoja, ujasiri wa kuthubutu, uzalendo usio na chenga na uamuzi usiosita, kwa jambo lenye maslahi kwa nchi yetu.

Alisema Rais Magufuli ni tunu ya pekee ambayo Watanzania hakika wanapaswa kumuenzi kutokana na maono yake.

Kwa mujibu wa Senyamule, anaamini bila yeye (Magufuli) kuanza mradi huo, ungeweza kuchukua hata miaka 50 mbele kuanza kuujenga kwa kungoja fedha ambazo zipo humu humu nchini.

Ujenzi wa reli hiyo unaanzia Bandari ya Dar es Salaam hadi mji mkuu wa Dodoma na baadaye hadi nchi za jirani za Rwanda, Burundi na DR Congo.

Mradi huo umeelezwa kuwa mkubwa zaidi katika miundombinu kufanyika miaka ya hivi karibuni na manufaa yake kiuchumi kuwa makubwa si kwa Tanzania tu, bali hata nchi za jirani.

# Miaka 30 jela kwa kumbaka binti wa miaka 12

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKAZI wa West Kilimanjaro, wilayani Siha, Joseph Nkea (24), amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela, kwa kosa la kumbaka binti wa miaka 12 aliyekuwa ametumwa kununua mboga.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Jasmine Abdul, akisoma hukumu hiyo mwishoni mwa wiki, amesema mahakama hiyo imemtia hatiani mshtakiwa huyo baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na mashahidi watano wa upande wa mashtaka.

Alisema hukumu hiyo iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Mshtakiwa huyo alitiwa hatiani kwa kutenda kosa hilo, Oktoba 3, 2018, majira ya saa 12 jioni nyumbani kwa wazazi wa binti huyo.

Hakimu Jasmine wakati anasoma hukumu hiyo, alieleza kuwa baada ya kuridhika na ushahidi wa watu watano uliotolewa mahakamani hapo na ambao haukuacha shaka, mahakama imemtia hatiani kwa kosa la kubaka na hivyo atalazimika kuanza maisha mapya gerezani ya kutumikia kifungo cha miaka 30.

Alieleza kuwa pamoja na juhudi za serikali na taasisi mbalimbali yakiwamo mashirika binafsi ya kiraia kujitahidi kumaliza tatizo hilo, mambo hayo bado yanaongezeka siku hadi siku.

Mapema Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Simon Feo, alidai mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alitenda kosa la kumbaka binti huyo ambaye ni mwanafunzi, huku akijua kwamba kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Katika hati ya mashtaka, mazingira ya tukio hilo yanaeleza kuwa mwanafunzi huyo wakati anabakwa, alikuwa ametoka kuchukua mboga gengeni kwa mama yake mzazi.

Ilielezwa na upande wa mashtaka kuwa, wakati mwanafunzi huyo alipokuwa anarejea nyumbani akiwa peke yake na alipofika nyumbani na kufungua mlango wa nyumba yao, ndipo mshtakiwa alipopata fursa ya kumbaka hapo hapo.

Mwendesha mashtaka huyo alidai mahakamani hapo kuwa, kitendo hicho ni kinyume na kifungu 130 (1) (2) na kifungu 131 (1) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 cha Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Katika utetezi wake, mshtakiwa huyo alieleza mahakama hiyo kwamba yeye ni yatima na ana familia inayomtegemea, hivyo anaiomba mahakama imuonee huruma.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Jasmine alitupilia mbali ombi hilo na kumhukumu kwenda kutumikia adhabu ya miaka 30 gerezani.

Nipashe
# Spotika
JUMATATU MEI 20, 2019




TISHA KWA KUCHEZA KLABU MOJA TU UK. 20




# KWA HERI KAMANDA...

Rafinha, akiagwa kwa kurushwa juu na wachezaji wenzake wa Bayern Munich baada ya kushinda mechi yao ya kufunga msimu dhidi ya Eintracht Frankfurt na kutwaa ubingwa wa Bundesliga. Rafinha ambaye ameitumikia klabu hiyo kwa miaka nane, anaungana na Arjen Robben na Franck Ribery ambao juzi waliichezea klabu hiyo, huku wakishinda 5-1, hiyo ikiwa ni mechi yao ya mwisho kuitumikia Bayern kwani wanaachana nayo msimu huu.
**PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

PEP Guardiola ni kocha wa nane kuweza kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, EFL Cup na FA Cup, baada ya Bill Nicholson, Don Revie, Joe Mercer, Kenny Dalglish, George Graham, Alex Ferguson na Jose Mourinho.



# NJIA 5 ZA KUISUKA BARCA MSIMU UJAO

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeshinda mechi zake nane kati ya 11 za mwisho za Ligi Kuu ya Hispania, La Liga kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Eibar, na wanatarajia kushinda taji la tano mfululizo la Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey']. Lakini mara ya pili mfululizo wametolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa wanahitaji kuimarisha kikosi chao. Na hapa tunaangalia njia tano ambazo Barcelona inaweza kuimarika msimu ujao...

**5. Kumuuza Philip Coutinho**

Januari 6, mwaka jana, Liverpool ilithibitisha kwamba ilifikia makubaliano na Barcelona kwa usajili wa Coutinho. Ada yake ya uhamisho iliripotiwa kuwa pauni milioni 105, ambayo ingeweza kupanda hadi pauni milioni 142. Katika msimu wake wa kwanza, Coutinho hakuweza kuichezea klabu yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Coutinho alichangia mabao 13 kwenye La Liga na mabao matatu kwenye Copa Del Rey.

Lakini msimu huu mambo yanaonekana kuwa magumu kwa Coutinho. Amefunga mabao matano tu na kutoa pasi za mwisho mbili kwenye La Liga. Hajawa kwenye kiwango kizuri, hali inayofanya hata mashabiki kuna wakati humzomea. Hivyo kama kuna sehemu ambayo Barcelona inahitaji kufanyia marekebisho ni kumuuza Coutinho ambaye nafasi yake imekuwa ikichukuliwa na Dembele kwenye kikosi cha kwanza.

**4. Kununua beki wa kushoto**

Wakati Jordi Alba alipojiunga na Barcelona kutoka Valencia kwa euro milioni 14 mwaka 2012, hakuna aliyemtarajia kuwa mmoja wa mabeki bora wa kushoto. Msimu huu peke yake alitoa pasi za mwisho 13 na kufunga mabao matatu katika mashindano yote. Kiulinzi Alba amekuwa ukuta mgumu. Lakini kwa sasa anahitaji kuwa na msaidizi pale kwenye benchi ambaye atatimiza majukumu yake yeye akiwa majeruhi.

Hivyo, wakati Lucas Digne alipoondoka kwenda Everton mwanzoni mwa msimu huu, ilikuwa wazi kwamba Barcelona inahitaji beki. Lakini kocha Ernesto Valverde aliamua kuwaamini vijana kutoka akademi ya La Masia, Juan Miranda na Cucurella. Bahati mbaya Cucurella aliondoka na kwenda Eibar kwa mkopo na Miranda hajawa kwenye kiwango kizuri. Hivyo wakati ambao Valverde aliamua kumpumzisha Alba, alimtumia Roberto au Semedo kucheza beki wa kushoto. Lakini sasa Barcelona inahitaji beki wa kushoto. Nyota wa Real Betis, Junior Firpo, Philipe Luiz wa Athletico na Alaba wa Bayern au Grimaldo wa Benfica wanaweza kuwa msaada kwao.

**3. Kuuza wachezaji wenye mishahara mikubwa**

Mabingwa hawa wa La Liga, Barcelona wamekuwa timu ya kwanza kutumia mabilioni ya euro kwenye mishahara ya wachezaji, baada ya stafu wake kutumia asilimia 42 kwa kipindi kilichopita.

Miamba hao wa Catalunya ambao walimsajili Philippe Coutinho kutoka Liverpool Januari mwaka jana kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya euro milioni 160, analipwa kiasi kikubwa. Ujio wa Ousmane Dembele na kuongeza mikataba kwa wachezaji wengine kama Lionel Messi na Jordi Alba, kumeongeza matumizi makubwa ya mishahara.

Kitu pekee cha kupunguza matumizi ya fedha nyingi ni kuwauza wachezaji wanaolipwa fedha nyingi.

**2. Kumfukuza Ernesto Valverde**

Baada ya kutolewa mara mbili mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kocha Valverde anapaswa kufukuzwa.

Klabu kama Barcelona haiwezi kuendelea kuwa na kocha ambaye misimu miwili mfululizo ameshindwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Valverde anaweza kuwa kocha mzuri, lakini hapaswi kuendelea kuwa na miamba hao wa Catalunya.

Kumfukuza Valverde linaweza kuwa suluhisho rahisi zaidi ili Barcelona ipate kocha mwenye njaa ya mafanikio ya taji hilo la Ulaya.

**1. Kuongeza wigo wa mawinga**

Wakati Neymar alipoondoka Barcelona kwenda PSG mwanzoni mwa msimu wa 2017-18, Barcelona ilimpoteza mtu ambaye alikuwa akitumia mipira kutoka kwenye winga. Kuziba pengo hilo, Barcelona ilimsajili Ousmane Dembele kutoka Dortmund kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 120.

Lakini kuumia kwake kukaifanya Barcelona kukosa huduma yake. Na sasa inatakiwa kununua mawinga wapya kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji.

Julian Brandt wa Bayer Leverkusen na Hudson Odoi wa Chelsea wote wanaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kama wakiamua kuwasajili ili kumsaidia Dembele.




Coutinho

## JE, WAJUA?

Manchester City ni timu ya nne kutwaa makombe yote makubwa ya kimashindano ya ndani kwa msimu mmoja baada ya Arsenal msimu wa 1992-93, Liverpool msimu wa 2000-01 na Chelsea msimu wa 2006-07.

MICHEZO

# MAPRO WALIOKALIA KUTI KAVU SIMBA SC

Na Adam Fungamwango

ITAKAPOMALIZIKA Ligi Kuu, Simba inataka kufanya usajili kabambe kwa ajili ya kushiriki michuano ya kimataifa mwakani.

Viongozi wa Simba wana uhakika kuwa msimu ujao watakuwamo kwenye michuano ya kimataifa, hivyo akili yao imelenga kufanya usajili wa wachezaji wa kimataifa kutoka nje ya nchi na wachache tu wa ndani.

Simba ina wachezaji 10 wa kigeni ambao wapo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Soka Tanzania. Lakini kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa iliyomalizika, kuna baadhi ya wachezaji wa kigeni wa timu hiyo hawakuonyesha kiwango ambacho wengi walitegemea wakionyeshe, ikizingatiwa kuwa wao ni wachezaji wa kulipwa kutoka nje ya nchi.

Ni kwamba baadhi ya wachezaji hao viwango vyao vingeweza kuzidiwa hata na wachezaji wa Kitanzania kama wangesajiliwa na timu hiyo na kuwekwa kwenye kikosi hicho.

Ndiyo maana hata Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu hiyo, Mohamed "MO" Dewji alisema kuwa anataka kusajili wachezaji wageni wa viwango vya juu, wenye uwezo na uzoefu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na si wale ambao wanakuja nchini kufanya majaribio.

Kwa kauli hiyo, tayari kuna baadhi ya wachezaji lazima wataondoka kuwapisha wenzao watakaosajiliwa baadaye. Hawa ni baadhi ya wachezaji wa kigeni wanaoonekana wataonyeshwa mlango wa kutokea kwenye klabu ya Simba kutokana na wengi kutoridhishwa na viwango vyao...

**1. Asante Kwasi**

Mwanachama au shabiki yeyote yule wa Simba ukimuuliza wachezaji wa nje ambao waondoke, jina la Asante Kwasi litakuwamo. Ni kwa sababu ameshindwa kumnyang'anya namba hata Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambaye pia naye ana makosa mengi upande wake.

Kwasi raia wa Ghana, anamaliza msimu wa pili Simba na wakati anaingia alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu, na si tu kwamba alikuwa akifanya vema kazi yake kama beki wa kushoto, lakini pia alikuwa na kasi na uwezo mkubwa wa kupeleka mashambulizi mbele na hata kufunga mabao.

Kwa msimu wake wa kwanza Simba, Tshabalala hakuwa na chake. Msimu wa pili hakuwa Kwasi yule. Majeraha yalimwandama na hata alipopona, hadi leo hajarudi kwenye kiwango chake cha kawaida. Simba haiwezi tena kwenda kwenye Ligi ya Mabingwa ikiwa na beki kama Kwasi. Ana asilimia kubwa ya kutemwa.

**2. Paschal Wawa**

Ni beki mzuri, mzoefu kwenye Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati na ni mzuri katika kuanzisha mashambulizi. Kama Simba ingekuwa kama Yanga, yaani yenyewe inataka kucheza Ligi Kuu tu, Wawa angefaa kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

Lakini akili ya Simba kwa sasa ni kwenye mechi za kimataifa na tayari imeshaonja ladha na imeshajua ni wachezaji wa aina gani wanatakiwa kuwamo. Ndiyo maana wao hata Paschal Wawa wanamuona hafai. Malengo yao ni makubwa. Kwanza kabisa wanadai umri wake umekuwa mkubwa, wengine wamekuwa hawakubaliani na aina ya ukabaji wake, hasa anapokutana na mastraika hatari kutoka nje ya nchi. Pia naye majeraha yameshaanza kumwandama. Huenda naye akawa mmoja wa watakaotemwa, raia huyo wa Ivory Coast.

**3. Juuko Murshid**

Tangu msimu uliopita, ni kama Simba ilikuwa inatafutia sababu ya kumtema. Na ingeweza kumtema kama si tetesi za kutaka kusajiliwa na Yanga. Kwa sasa inaonekana Simba haina tena wasiwasi huo, labda kutokana na uchumi wa mahasimu wao kuwa wa kubabaisha.

Juuko, raia wa Uganda amekuwa ni kama vile hana bahati na timu hiyo, kwani akiwa na klabu yake ya Uganda hufanya vema, lakini akiwa Simba amekuwa akifanya makosa mengi yanayoigharimu timu ikiwamo kucheza kibabe.

Kama Simba kwa sasa ina uwezo wa kuchezesha mabeki wa kati Wabongo watupu, yaani Yusuph Mlipili na Erasto Nyoni, basi safari ndiyo imemkumba kwa sababu nafasi hiyo wenyewe wanaitaka kusajili beki mwenye viwango vya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika na si vinginevyo.

**4. Zana Coulibaly**

BEKI huyu wa kulia alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo. Ni raia wa nchi mbili za Burkina Faso na Ivory Coast. Awali hakukubalika kabisa na mashabiki wa soka nchini.



.Paschal Wawa

Baadaye akabadilika na kufanya vitu vya uhakika, kiasi cha kuwa kipenzi cha mashabiki wa Simba.

Haijajulikana ni kulewa sifa, au vipi, ameonekana kurejea kwenye hali yake ile ile ya awali. Kwa sasa anafanya makosa mengi uwanjani. Akipanda anachelewa kurudi. Kuna baadhi ya makocha wa timu wameshajua jinsi gani ya kucheza na Simba kama Zana yupo. Ni kwamba wanaponyang'anya mpira wanaupiga upande ambao ametoka na wote wanakimbia huko, hivyo inakuwa ni hatari kwa timu hiyo. Ameigharimu Simba kufungwa mabao mengi kwenye mechi ya TP Mazembe kwa makosa yake binafsi. Sidhani kama anaweza kusalia kwenye kikosi hicho kinachojipambanua kufanya usajili wa kufa mtu.

**5. Nicolaus Gyan**

Kitakachomgharimu mchezaji huyu raia wa Ghana ni mahitaji makubwa ya klabu na si uwezo.

Wakati Zana akisajiliwa, Gyan alikuwa ameshuka kiwango na kutoaminika tena. Wakati Zana kiwango kimeshuka, Gyan amerejea kwenye kiwango cha hali ya juu na hata akicheza kwenye nafasi ya beki wa kulia kunakuwa ni kugumu kupitika kuliko hata kwa Tshabalala.

Gyan ambaye kwa asili ni straika, aligeuzwa kuwa beki wa kulia na hadi ligi inaelekea mwishoni amekuwa mhimili kwa Simba.

Hata hivyo, kutokana na kwamba Simba inahitaji idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni wenye uwezo mkubwa zaidi ya hawa waliopo, huenda akaondoka kwenye klabu hiyo, au akatolewa kwa mkopo ili baadaye aweze kurejea kutokana na kwanza ana umri mdogo, lakini pia anakubalika na mashabiki na viongozi wa klabu hiyo.

NJE YA UWANJA

## STERLING APORWA BAO LA HAT-TRICK

BAO la pili lililokuwa likimfanya Raheem Sterling kukamilisha hat-trick yake kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA wakati Manchester City ikiichapa Watford 6-0, amezawadiwa Gabriel Jesus.

Baada ya mpira wa Jesus kutua katika mstari wa goli, Sterling aliuzamisha kimyani katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi, Jumamosi na kuifanya City kuwa mbele kwa mabao 2-0 dhidi ya Watford.

Utata wa bao hilo, na mabao mawili Sterling aliyofunga kipindi cha pili unamwondolea sifa ya kuwa mchezaji wa nne kufunga hat-trick kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA, na wa kwanza tangu Stan Mortensen alipofanya hivyo mwaka 1953.

Hata hivyo, baada ya uamuzi huo kuchelewa kutolewa, bao hilo sasa limetolewa rasmi kwa mchezaji mwenza, Jesus, ambaye pia alifunga lingine na hivyo sasa kuwa ametupia mawili wakati City ikishinda 6-0, na kukamilisha taji lao la tatu msimu huu.

Sterling, 24, kupitia mtandao wa Twitter, alilalamikia uamuzi huo akidai bao hilo lilikuwa lake, na hata akaenda mbali zaidi kwa kumshukuru Jesus kwa pasi yake ya mwisho.



Extra Time

# TIMU 5 EPL NA MASHIMO WANAYOTAKIWA KUFUKIA




**LONDON, England**

MSIMU wa Ligi Kuu England wa 2018/2019, umemalizika na Manchester City wametawazwa kuwa mabingwa. Vijana hao wa Pep Guardiola walifanya kazi ya ziada kuhakikisha wanalitwaa taji hilo mbele ya Liverpool.

Baada ya kuongeza wachezaji wachache kwenye kikosi chake, Jurgen Klopp aliwapa wakati mgumu Man City kwenye mbio za ubingwa huo. Licha ya kuwa kwenye wakati mgumu, Chelsea chini ya Maurizio Sarri wameweza kutinga fainali ya Ligi ya Europa.

Tottenham na Arsenal pia walikuwa wakikabiliwa na presha ya kumaliza kwenye nne bora. Licha ya kutonunua wachezaji wapya, Spurs walifanikiwa kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao na pia wametinga fainali ya michuano hiyo.

Chini ya kocha mpya, Unai Emery, Arsenal hawakuwa na kiwango kizuri. Lakini wametinga fainali ya Ligi ya Europa ambapo watacheza na Chelsea mjini Baku.

Klabu zote hizo baada ya kumalizika kwa msimu huu zinahitaji kuingia sokoni wakati huu wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto na hapa tunaangalia idara ambazo wanatakiwa kuziimarisha...

**1. Arsenal (Mawinga)**

Msimu wa kwanza wa Emery kama kocha wa Arsenal unaweza kumalizika kwa kubeba Kombe la Ligi ya Europa mjini Baku nchini Azerbaijan Mei 29, mwaka huu. Hata hivyo, kikosi hicho kina mapungufu kadhaa ambayo wanatakiwa kuyafanyia kazi. Kiukweli kwenye safu ya ulinzi hasa beki wa kati ni jambo ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi.

Hata hivyo, Arsenal msimu huu ilikuwa na tatizo kubwa mno la mawinga, hivyo kipindi hiki cha majira ya joto wanatakiwa kufanyia kazi idara hiyo.

Mabeki wa pembeni, Hector Bellerin, Nacho Monreal, Sead Kolasinac na Maitland-Niles ndio walitumika kama mawinga wa kupanda na kushuka.

Hata hivyo, kunahitajika mawinga ambao wataweza kusukumiza mashambulizi ya Arsenal mbele na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata mabao.

Majina kama Nicolas Pepe (Lille OSC), Ryan Fraser (Bournemouth) na Leonardo Trossard (KRC Genk) yamekuwa yakihusishwa na mpango wa kusajiliwa kwa 'Washika Bunduki' hao.

**2. Tottenham Hotspur (Kiungo ya Kati)**

Kama Spurs watashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye fainali ya Juni Mosi, mwaka huu, kocha Mauricio Pochettino atatatakiwa kujengewa sanamu kwenye uwanja wao mpya. Hii ni kwa sababu ametumia nguvu ya ziada kuhakikisha kikosi hicho kinafanya vizuri msimu huu.

Ameweza kumaliza kwenye nafasi ya nne katika Ligi Kuu akizipiku timu kubwa kama Arsenal na Manchester United. Chochote kitakachotokea kwenye fainali ya mjini Madrid, lakini klabu hiyo inatakiwa kutumia fedha kwa ajili ya usajili.

Nafasi ya kiungo wa kati kwa timu hiyo haikuwa vizuri kwa kipindi chote cha ligi hiyo msimu huu. Harry Winks, Eric Dier, Victor Wanyama na Dele Alli waliumia na wakaifanya timu hiyo kuwa kwenye wakati mgumu. Moussa Sissoko alionekana kujaribu kuziba pengo lao, lakini bado kulionekana kuna pengo. Endapo Christian Eriksen atatimkia Real Madrid kama uvumi unavyosambaa ni lazima wahakikishe wanasajili viungo wapya.

Majina kama Andre Gomes (Barcelona) na Youri Tielemans (AS Monaco) yanahusishwa kwenye usajili huo.

**3. Chelsea (Mshambuliaji)**

Umekuwa msimu mgumu pale Stamford Bridge, kwa kuwa licha ya ujio wa Maurizio Sarri katika kikosi hicho, lakini bado haijawa na mshambuliaji wa kumtegemea.

Mabao mengi ya Chelsea msimu huu yametoka kwa viungo na hasa Eden Hazard ambaye ndiye alikuwa kama nguzo ya kikosi hicho na kuweza kumaliza ligi ikiwa nafasi ya tatu.

Hata hivyo, safu ya ushambuliaji imekuwa butu kwa kukosa mchezaji pale mbele. Ujio wa Gonzalo Higuain aliyetua hapo kwa mkopo ulionekana kama ungekuwa na msaada, lakini ameshindwa kufikia kile ambacho wengi walikitarajia kutoka kwake.

Olivier Giroud amekuwa kwenye kiwango kibovu zaidi tangu atue hapo akitokea kule Arsenal, lakini alikuwa na wakati mzuri kwenye Ligi ya Europa akiwa na mabao 10. Hivyo, kwa vyovyote, Chelsea inahitaji mshambuliaji.

**4. Liverpool (Kiungo Mchezeshaji)**

Walikaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu wa 2018/2019 na hiyo ni baada ya kuijenga vizuri timu yao wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka jana.

Wana golikipa mzuri na safu imara ya beki na wametinga kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya pili mfululizo.

Lakini katika safu ya kiungo mchezeshaji kunaonekana kuna tatizo kubwa. Kuondoka kwa Philippe Coutinho aliyetimkia Barcelona kunaonekana kuwa tatizo kubwa kwako na hivyo wanahitaji kiungo mwingine kwa ajili ya msimu ujao. Naby Keita alitarajiwa angekuwa msaada mkubwa akicheza nyuma ya kina Mo Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino, lakini hakufikia kwenye kiwango kikubwa. Nabil Fekir linabakia kuwa jina linalotajwa zaidi hapo Anfield kwamba anahitajika, lakini pia Youri Tielemans (AS Monaco) na Ruben Neves (Wolves) wamekuwa wakihusishwa.

**5. Manchester City (Kiungo wa kati)**

Licha ya Fernandinho kuumia, lakini amekuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kwenye safu ya kiungo wa kati. Lakini katika umri wake wa miaka 34, raia huyo wa Brazil anahitaji mtu wa kumsaidia, kwani pale alipokosekana uwanjani ilionekana kuwa mambo magumu kwao. Man City kwa namna yoyote kwa sasa wanahitaji kiungo wa kati. Majina kama Douglas Luiz amekuwa na msimu mzuri pale Girona ambako anacheza kwa mkopo kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga. Anaweza kuwa msaada mkubwa kama akirudi kwenye kikosi hicho. Ingawa kuna majina kama Rodri (Atletico Madrid) na Tanguy Ndombele (Olympique Lyonnais) ambao wanatajwa kuwaniwa na klabu hiyo.


## NUKUU



"Nimebakiza miaka miwili kwenye mkataba wangu, sielewi kitakachotokea baada ya hapo, lakini kwa wakati huu siendi kokote," alisema **Mesut Ozil akieleza dhamira yake ya kuendelea kuitumikia Arsenal hadi mkataba wake utakapofika tamati mwaka 2021.**



"Nilitaka kuwaambia mashabiki ambao mara zote wamekuwa wakionyesha mapenzi, kwamba nimechukua uamuzi wa kuondoka, kuona mambo mengine, kupata changamoto nyingine, ukweli imekuwa ni vigumu kuchukua njia hii, lakini ndicho ninahisi, ninakihitaji na ningependa kuwashukuru wote kwa mapenzi mlionionyesha katika kipindi cha miaka mitano," **Antoine Griezmann, 28, akiaga rasmi Atletico Madrid.**



"Ni heshima kupata tuzo hii. Nataka kuisherehekea tuzo hii na wachezaji wangu kwa sababu wao ndio kila kitu kwa benchi la ufundi kwa sababu tulipigana pamoja na makocha wote wa Ligi Kuu, hasa Jurgen Klopp, ambaye nilipambana naye hadi mwisho, ni fahari kwetu kucheza dhidi yao, wote tulikuwa katika ushindani mkubwa dhidi yao katika mbio za kuwania ubingwa**,"** **Pep Guardiola baada ya kutangazwa kocha bora wa msimu.**

Michezo

# 11 WAKUIRUDISHIA YANGA MAKALI

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Yanga kinahitaji mabadiliko makubwa msimu ujao ili kuendana na ushindani ambao tayari umeanza kuonekana kwenye soka la Tanzania msimu huu.

Kuna dalili zote za klabu hiyo kongwe kukosa michuano ya kimataifa msimu ujao baada ya kutolewa kwenye Kombe la FA kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Lipuli na pia haina uhakika wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaoonekana utaelekea mtaa wa Msimbazi kwa mara ya pili mfululizo.

Kutokana na hali hiyo, Yanga inabidi ijipange vizuri kwa msimu ujao kwa kusajili wachezaji wa ndani na wa nje, wenye uwezo mkubwa ambao wamefanya vizuri msimu unaomalizika wakiwa na timu mbalimbali.

Kwa wachezaji wa ndani Yanga ina faida moja kuwa washindani wao wakubwa Simba hawana mpango wa kusajili wachezaji wengi wa ndani, badala yao macho yao yameelekezwa zaidi nje ya nchi, hivyo soko la usajili la wachezaji wa ndani linaweza kuwa zuri kwao na kupata wachezaji wengi wazuri, wenye uwezo na wanaoweza kuwasaidia msimu ujao kwa ajili ya kurejesha makali. Wafuatao ni wachezaji 11 wa Kitanzania ambao kama Yanga itafanikiwa kuwasajili, basi inaweza kurejea kwenye kiwango chake kilichozoeleka...

**1. Aron Kalambo-Prisons**

Ni kipa wa Prisons ambaye Yanga ilikuwa inamwania tangu msimu uliopita na hata kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu huu, lakini pesa ikawa tatizo. Kalambo ni mmoja wa makipa mahiri kwa sasa kiasi cha kuitwa kwenye timu ya taifa, Taifa Stars.

Kama Yanga itafanikiwa kumsajili kipa huyu itakuwa imetibu tatizo la golini kwa kuwa mpaka sasa, bado mashabiki na wanachama wa timu hiyo hawana imani sana na uwezo wa makipa wao waliopo.

**2. Said Kipao - Kagera Sugar**

Kwa sasa anaidakia Kagera Sugar. Ni kipa wa zamani wa JKT Ruvu. Kwenye mechi mbili ambazo Kagera Sugar imecheza dhidi ya Simba, Kipao amecheza kwa kiwango cha hali ya juu na kuwa kikwazo kwa mastraika hatari wa Simba, kina John Bocco, Emmanuel Okwi na Meddie Kagere.

Dawa ya kufungwa mara kwa mara na Simba inaweza kutoweka kwa kumsajili kipa huyu ambaye anaonekana kuwajulia mastraika hao.

**3. Kenny Ally- Singida United**

Huu ni msimu wa tatu Yanga inapigania kumsajili kiungo huyu mkabaji. Tangu alipokuwa Mbeya City, Yanga ilionekana kuvutiwa na kiungo huyo, lakini baadaye ikapigwa bao na Singida United.

Kwa Yanga haitokuwa na kazi kubwa kumpata Kenny kutoka Singida United kwa msimu ujao kutokana na urafiki baina ya timu hizo uliofikia mpaka kupeana wachezaji.

Kama ikifanikiwa kumtia mikononi, basi nafasi ya kiungo mkabaji ambayo nayo pia ni tatizo, inaweza kuimarika.

**4. Aron Lulambo - KMC**

Kuna taarifa kuwa beki wa kushoto wa Yanga, Gadiel Michael anamaliza mkataba wake Yanga na huenda asisaini tena, badala yake akatimkia Afrika Kusini au akaenda Simba.

Kama Wanajangwani wanamsainisha beki tatu huyu anayeichezea KMC wanaweza kuwa wamelamba dume, kwani ni beki wa kupanda na kushuka, ambaye anaendana sana na staili ya uchezaji wa timu hiyo.



Kabunda

**5. Ahmad Waziri - Kagera Sugar**

Wakati mwingine Yanga huyumba kwenye safu ya nyuma anapokosekana Kelvin Yondani.

Ni kwa sababu Yondani hutumia nguvu na akili, tofauti na mabeki wengine wa timu hiyo wa kati ambao hata sehemu wanayopaswa kutumia akili tena ndogo tu, inatumika nguvu kubwa kupita kiasi.

Ahmad Waziri ni beki wa kati wa Kagera Sugar ambaye anatumia nguvu inapobidi na akili zaidi katika kutekeleza majukumu yake. Kama Yanga ikimsajili atakuwa mbadala wa Yondani inapotokea tatizo la kadi, majeruhi, au kutumika wote wawili.

**6. Idd Suleiman 'Nado'- Mbeya City**

Ni mchezaji ambaye msimu unaomalizika ameweka rekodi ya kuzifunga Simba na Yanga, ingawa timu yake imekuwa ikipoteza mechi kwenye michezo hiyo.

Nado, mchezaji wa Mbeya City aliyechukuliwa kutoka michuano ya Ndondo Cup misimu miwili iliyopita, akiwa anaichezea Manzese United, anamaliza mkataba wake na timu hiyo, hivyo yuko huru kwenda kokote kule.

Yanga itakuwa imelamba dume kumsajili mchezaji huyu mwenye uwezo wa kucheza winga zote mbili, tisa na kumi, akiwa na uwezo wa kupiga miguu yote miwili, pia kufunga kwa kichwa.

**7. George Sangija- KMC**

Huyu ni aina ya winga ambao Yanga huwa inawahitaji. Ana kasi, chenga za maudhi na krosi za hatari.

Ni winga wa kulia wa KMC ambaye ameifanya timu hiyo kuwa ya kutisha msimu huu licha ya kwamba ni msimu wake wa kwanza.

Yanga inahitaji winga wa aina hii kutokana na staili yake ya uchezaji ya enzi na enzi, kwani kwa sasa inakosa aina hiyo ya wachezaji kufuatia winga kama Mrisho Ngassa umri kuanza kumtupa mkono na kasi kupungua.

**8.Hassan Kabunda- KMC**

Ni mtoto wa zamani wa beki wa Yanga, Salum Kabunda 'Ninja'. Hivyo kama Yanga ikimsajili haitokuwa imepotea, itakuwa tu imemkaribisha mtoto wa nyumbani.

Kabunda, mwenye uwezo wa kucheza winga ya kushoto, au straika msaidizi, yaani namba kumi, kwa msimu miwili sasa amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu kiasi hata Simba ilikuwa na mpango wa kumsajili, lakini baadaye ikasitisha.

Spidi yake, uwezo wake wa kupiga chenga na umahiri na kupachika mabao, utawafanya Yanga kurudi tena kwenye chati iliyozoeleka.

**8. Kassin Khamis- Kagera Sugar**

Ni mmoja wa mastaika bora chipukizi kwa sasa. Naye ameitwa kwenye kikosi cha Taifa Stars. Ameshapachika mabao tisa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, mengine akiyafunga kwenye mechi alizocheza dhidi ya Simba na Yanga.

Kama Simba ingekuwa inatoa macho kwa wachezaji wazawa, Yanga ingepata tabu kumpata, lakini kwa sasa inaweza kufanya haraka kabla Azam haijafanya hivyo.

Baada ya kuondoka Heritier Makambo, wakati Yanga inatafuta mbadala kutoka nje, Kassim Khamis anaweza kabisa kuvaa viatu hivyo.

**10. Said Dilunga - Ruvu Shooting**

Ana mabao 10 mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Straika huyu wa Ruvu Shooting anaweza kuwa msaada mkubwa kwa Yanga na kuwa mbadala wa Amissi Tambwe ambaye anaonekana hayuko kwenye kiwango chake kilichozoeleka kwa sasa.

**11. Ayoub Lyanga- Coastal Union**

Hapa Yanga inaweza kupata tabu kidogo kwa sababu moja kati ya wachezaji wachache wa Kibongo ambaye ananyemelewa na Simba ni Ayoub Lyanga.

Ni winga wa kulia, lakini pia hucheza kama straika wa kati. Ana uwezo wa hali ya juu wa kumiliki mpira na kupiga chenga huku akikimbia kwa kasi na kupiga mashuti makali.

Ameshaifungia Coastal Union mabao tisa na uhakika ni kwamba mchezaji huyo hatochezea timu hiyo kutokana na kiwango chake cha juu.

Kama Yanga ikiipiga bao Simba na kumpata mchezaji huyu, basi msimu ujao itatisha.

## NAJUA WAJUA

**Manchester City ni klabu ya kwanza Ligi Kuu England kushinda mechi 50 katika mashindano yote kwa msimu mmoja.**






Wachezaji wa Liverpool kutoka kulia juu, Sadio Mane na Roberto Firmino wakiwania kufunga dhidi ya Bayern Munich kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

# KWA NINI EPL MSIMU HUU IMEKUWA BORA?

**NDANI YA 18**

David Silva amekuwa mchezaji wa pili Manchester City kuweza kufunga katika fainali zote; ya Kombe la FA na Kombe la Ligi, baada ya Yaya Toure.



**LONDON, England**

WIKENDI iliyopita, Manchester City iliifunga Brighton mabao 4-1 na kulitwaa taji la Ligi Kuu ya England na kuufanya kuwa moja ya msimu bora zaidi kwenye historia ya soka la Uingereza. Kipindi cha miezi tisa iliyopita kumekuwa na vuta nikuvute nyingi katika mbio za ubingwa huo.

Msimu huu wa 2018/19, umekuwa wenye mafanikio makubwa na hata katika mbio hizo zimekuwa za kuvutia.

Makala haya yanakuchambulia sababu nne kwa nini msimu huu umekuwa bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya England na historia ya soka la Uingereza.

**4. Mwangwi wa Southgate**

Michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2018, ilikuwa ya kuvutia zaidi kwa mashabiki wa soka la Uingereza. Baada ya miongo miwili ya kutofanya vizuri kwenye mashindano hayo makubwa zaidi ya soka, vijana wa England chini ya Gareth Southgate walifanya maajabu. Walitinga nusu fainali katika mashindano hayo yaliyofanyika nchini Urusi na wakafungwa na Croatia.

Kiwango kilichoonyeshwa na timu hiyo katika mashindano hayo kimechangia kwa kiasi kikubwa kuifanya Ligi Kuu ya England kuwa kwenye ubora zaidi.

Kwa sasa England inajiandaa na michuano ya Euro 2020 na kuna uwezekano wakafanya maajabu kama kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

**3. Mafanikio Ulaya**

Kimekuwa kipindi bora zaidi kwa timu za England, kwani sasa fainali ya Ligi a Mabingwa Ulaya itazikutanisha timu za Liverpool na Tottenham. Fainali hiyo itapigwa jijini Madrid nchini Hispania.

Timu zote zimeonyesha kiwango cha kuvutia na hivyo kuwa ni mara ya kwanza kwa kipindi cha muongo mmoja kuzikutanisha timu za Ligi Kuu ya England kwenye fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Kama hiyo haitoshi, Chelsea na Arsenal pia zimetinga fainali ya Kombe la Europa ambapo fainali yake itapigwa mjini Baku, baada ya kuzifunga Frankfurt na Valencia kwenye nusu fainali.

Hii inamaanisha kwamba, ni mara ya kwanza katika historia fainali ya Ligi ya Europa na ile ya Mabingwa Ulaya kuzikutanisha timu zinazotoka nchi moja, kitu ambacho ni mafanikio makubwa zaidi EPL.

Yeyote atakayeshinda fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Madrid na Baku ni kwamba itakuwa timu kutoka England.

**2. Ushindani kwenye ligi tatu**

Wakati mengi yamezungumza kuhusu Ligi Kuu ya England msimu huu, lakini wote wanaofuatilia ligi tatu za Uingereza wanaweza kukuambia kwamba, imekuwa bora kama siyo ya kuvutia.

Ligi ya Championship kumekuwa na vita kati kati ya Norwich, Sheffield United na Leeds. Zote zimekuwa kwenye mbio sawa. Hata ukitazama Ligi Daraja la Pili nako ushindani umekuwa mkubwa mno kwa Lincoln City na Mansfield Town kama ilivyokuwa kwenye Ligi Kuu.

Ushindani wa ligi hiyo msimu huu umekuwa wa kuvutia zaidi kiasi kwamba hadi mechi ya mwisho hakuna timu iliyokuwa na uhakika wa kupata ushindi. Kwa uhakika uwekezaji kwenye soka la Uingereza umekuwa wa kuvutia na kuifanya ligi hiyo kuwa yenye ushindani wa kuvutia zaidi.

**1. Mbio bora zaidi za ubingwa EPL**

Bila shaka zilikuwa mbio za kuvutia zaidi kwa kipindi cha miezi 12, huku Liverpool ya Jurgen Klopp na Pep Guardiola na Manchester City yake zikiwa kwenye mbio bora zaidi.

Man City na Liverpool zilikuwa zinabadilishana nafasi ya uongozi wa msimamo katika mbio za ligi hiyo kila wikendi na hivyo kuufanya ushindani kuwa mgumu mno. Hadi siku ya mechi za mwisho za ligi hiyo, si Man City au Liverpool waliokuwa na uhakika wa kulitwaa taji hilo.

Katika siku ya mwisho, mabingwa Man City waliwafunga Brighton mabao 4-1 na kulibeba taji hilo, huku Liverpool wakiwafunga Wolves 2-0.

Kikosi cha Klopp kilimaliza ligi kikiwa na pointi 97, huku kikiwa imepoteza mchezo mmoja tu msimu mzima, pointi moja tu ndio iliyowanyia ubingwa mbele ya vijana wa Pep ambao wamelitwaa taji hilo kwa mara ya pili mfululizo.

Wakati mashabiki wa Liverpool walikuwa na shauku kubwa ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990, lakini matarajio yao yakaishia kwa Man City kulibeba taji hilo.



MSIMU wa Ligi Kuu England wa 2018/2019, umemalizika na Manchester City wametawazwa kuwa mabingwa. Vijana hao wa Pep Guardiola walifanya kazi ya ziada kuhakikisha wanalitwaa

Uk.16-17




# NYOTA WALIOTISHA KWA KUCHEZA KLABU MOJA TU

**ROME, Italia**

DANIELE De Rossi ataungana na mchezaji mwenzake wa zamani, Francesco Totti kuwa miongoni mwa wachezaji waliocheza timu moja tu hadi kustaafu katika historia ya soka, baada ya AS Roma kuthibitisha kwamba anaondoka.

De Rossi hajawahi kuichezea klabu nyingine zaidi ya 'Giallorossi' hao na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ameonyesha njia ya kutaka kuondoka na kwenda kucheza sehemu nyingine, kabla ya kuhamia kwenye ukocha kama ambavyo amesema.

Kiungo huyo mkabaji, De Rossi alikuwa kwenye kikosi cha Italia kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2006 na anatarajia kuondoka kwenye Ligi ya Serie A na kwenda kumalizia kipindi chake cha uchezaji sehemu nyingine.

Wengi walitarajia kwamba, De Rossi angeweza kumaliza kipindi chake cha uchezaji hapo Roma, lakini yeye ameamua kuondoka. Hapa tunawaangalia wachezaji ambao maisha yao yote ya soka wameichezea klabu moja tu...

**FRANCESCO TOTTI (ROMA)**

De Rossi na Totti walitumia miaka mingi hapo Roma, kabla ya mshambuliaji huyo kutangaza kustaafu msimu uliopita. Totti kwa sasa ni mkurugenzi wa Roma ambaye pia ni balozi wa Euro 2020, ambaye ameshinda taji la Serie A mara moja msimu wa 2000-2001 na kumaliza nafasi ya pili mara tisa. Mchezaji aliyejaliwa kipaji na mfungaji mzuri, Totti pia ameshinda mara mbili taji la Coppa Italia akiwa na klabu hiyo na sasa ameondoka hapo Roma na mwaka 2004 alikataa ofa ya Real Madrid. Totti na De Rossi wote wataingia kwenye historia ya klabu hiyo ya Roma kama magwiji wao.

**RYAN GIGGS, PAUL SCHOLES (MAN UNITED)**

Kocha wa Wales, Ryan Giggs alikuwa mchezaji wa klabu moja akicheza pale Manchester United kwa kipindi chake cha maisha yake ya soka. Giggs alijiimarisha yeye mwenyewe kama winga mwenye kasi na akicheza hadi katika umri wa miaka 40. Giggs ameshinda vitu vingi akiwa pale Old Trafford, yakiwamo mataji 13 ya Ligi Kuu, mataji manne ya FA na taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Giggs amecheza mechi 632 za Ligi Kuu akifunga mabao 109 na alikuwa kocha msaidizi chini ya Louis van Gaal.

Mwingine ni Paul Scholes mchezaji mwenzake na Giggs ambaye ametumia muda wake wote wa kucheza akiwa katika klabu hiyo.

Scholes aliingia hapo pamoja na wakali wengine kama Nicky Butt, David Beckham, Gary Neville na Phil Neville.

**PAOLO MALDINI, FRANCO BARESI (AC MILAN)**

Paolo Maldini alikuwa kama Giggs pale United, akicheza hadi katika umri wa miaka 40. Ameshinda mataji saba ya Ligi Kuu na matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na amecheza pale kwenye dimba la San Siro, kwa kipindi cha miaka 25. Maldini, ni mtoto wa gwiji mwingine wa Milan, Cesare, ambaye ameichezea timu hiyo zaidi ya mechi 1,000 katika michuano yote kwa kipindi chote cha uchezaji wake.

Amefuata nyayo za beki gwiji mwingine wa Italia ambaye aliichezea Italia na Milan, Franco Baresi, ambaye alikuwa nahodha wa Rossoneri katika kipindi chote cha uchezaji wake hapo San Siro. Baresi alishinda mataji sita ya Serie A na matatu ya Ulaya, pamoja na kuisaidia Italia kushinda Kombe la Dunia mwaka 1982. Baresi pia alishika nafasi ya pili kwenye tuzo za Ballon d'Or mwaka 1989 na alijumuishwa kwenye kikosi cha mwaka cha Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa mwaka huo.

**JAMIE CARRAGHER (LIVERPOOL)**

Jamie Carragher alikuwa mmoja wa mabeki mahiri zaidi kwenye Ligi Kuu ya England, akicheza mechi 508 katika mashindano yote kwa Liverpool. Kwa sasa ni mchambuzi wa soka kwenye Televisheni ya Sky Sports. Carragher hakuwahi kushinda taji la Ligi Kuu, lakini aliisaidia timu yake kushinda mataji kadhaa ya FA, pia akicheza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya bora zaidi kwa Liverpool wakati walipotoka nyuma ya 3-0 dhidi ya AC Millan na kutwaa ubingwa huo mwaka 2005 jijini Istanbul nchini Uturuki kwa mikwaju ya penalti. Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England alistaafu kucheza soka mwaka 2013.

## USILO LIJUA

Trent Alexander-Arnold ametoa pasi za mwisho 14 katika mashindano yote msimu huu, ambazo ni zaidi ya mchezaji yeyote yule Liverpool.





# Ubovu wa barabara wawalazimu kusafirisha mizigo kwa kichwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAKAZI wa Kijiji cha Masebe kilichopo Kata ya Mwaya wilayani Kyela, katika Mkoa wa Mbeya, wanalazimika kusafirisha mazao yao kwa kujitishwa kichwani ama kutumia baiskeli kwa zaidi ya kilomita 10 kutokana na barabara kuwa mbovu.

Wananchi hao ambao ni wakulima wa mpunga na kakao, wanadai kuwa barabara inayopita katika kijiji chao ni mbovu hali inasababisha magari kushindwa kupita kwa ajili ya kubeba mazao hayo kwenda sokoni na kuiomba serikali kuwasaidia kuboresha barabara hiyo.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo kuhusu madhara ya mafuriko yaliyosababisha vifo vya watu watano na wengine zaidi ya 2,500 kukosa makazi, wananchi hao walisema mbali na madhara hayo, lakini barabara zimeharibika zaidi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Daraja la Kagera ambalo linajengwa kwa nguvu za wananchi, Michael Mwakalambile, alisema baadhi ya makalafati yameharibika na hivyo barabara kutopitika kabisa.

Alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wananchi wamekuwa wakilazimika kutengeneza kwa nguvu zao maeneo ambayo ni korofi zaidi, lakini bado mafuriko yanasomba miundombinu yote.

"Hata hili daraja tunajenga kwa gharama zetu wenyewe, halmashauri walitusaidia baadhi ya vifaa, lakini kusafirisha kutoka mjini mpaka hapa nilitumia pesa zangu Sh. 300,000, tunatumia mianzi kutengeneza daraja hili kwa sababu ndio vifaa rahisi kupatikana hapa," alisema Mwakalambile.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Saimon Mwakibuje, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakiahidiwa na serikali kuwa watajengewa barabara hiyo, lakini utekelezaji wake umekuwa hafifu.

Alisema baadhi ya wananchi wanashindwa kusafirisha kakao zao kwenda kwenye chama cha msingi cha ushirika na hivyo kulazimika kuuza kwa watu wengine ili angalau wapate fedha za kusafirishia kiasi kinachobaki.

"Tunaomba serikali itusaidie kuboresha miundombinu ya barabara yetu ili ipitike mwaka mzima, kama unavyoona watu wanapambana kuanika kakao zao licha ya hali ya hewa kuwa mbaya, lakini hata zikikauka kwa sasa ni vigumu kusafirisha," alisema Mwakibuje.

Alisema licha ya pikipiki za kubeba abiria kuwa nyingi sasa hivi, hazina kazi kutokana na ubovu wa barabara hiyo ambayo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wake.

Alisema mafuriko ya Mto Mbaka yanayotokana na mvua zinazonyesha katika Wilaya ya Rungwe, yameongezea ubovu wa barabara hiyo kutokana na kusomba madaraja na kuchimba mashimo makubwa ambayo yanahatarisha maisha ya watu.

Baadhi ya wanawake wa kijiji hicho walisema kwa sasa wanapata shida hata kuhudhuria kliniki wanapokuwa wajawazito kwa sababu ya kuogopa mafuriko.



Baadhi ya wanawake wa Kata ya Mwaya, Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, wakihangaika kuvuka katika moja ya maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko kufuatia Mto Mbaka kufurika na maji kuzingira makazi ya watu na barabara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miundombinu yakwamisha huduma majisafi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ZAIDI ya wananchi 30,000 wa vijiji 13 vilivyopo mpakani mwa wilaya za Makete na Mbarali, wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kutokana na miundombinu ya maji iliyopo kushindwa kumudu ongezeko la watu katika eneo hilo.

Kutokana na hali hiyo wananchi hao wanaiomba serikali kuwasaidia kupanua miundombinu ya maji iliyojengwa miaka 28 iliyopita ili iweze kuendana na ongezeko la watu katika eneo hilo.

Wananchi hao wanategemea mradi wa maji wa Nyaugenge ambao umeanzia kwenye maporomoko ya Mto Kimani ndani ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele, ambao miundombinu yake ilijengwa mwaka 1991 na wanadai imechakaa.

Mwenyekiti wa watumia maji wa Nyaugenge, Benedicto Chaula, alisema miundombinu ya mradi huo ilijengwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi 6,000, lakini kwa sasa wananchi wameongezeka na kufikia zaidi ya 30,000 na kusababisha miundombinu kutomudu mahitaji.

Alisema katika chanzo cha maji cha mradi huo kuna maji ya kutosha, lakini wananchi wanashindwa kuyapata ya kutosha kutokana na miundombinu kuchakaa na kuiomba serikali kuwasaidia kuipanua ili iendane na mahitaji halisi ya wananchi. "Kwa sasa wananchi wameongezeka mara tano zaidi ya makadirio ya awali ya wanufaika wa mradi huu, sasa kinachotakiwa ni kuweka miundombinu mipya itakayomudu mahitaji ya wananchi, tunaiomba serikali itusaidie," alisema Chaula.

Vyanzo vya maji ya Mto Kimani vipo katika safu za Mlima Kipengele ndani ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele na kutokana na uhifadhi mzuri wa vyanzo hivyo unaofanywa na Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori (Tawa), inadaiwa yanaweza kuwa maji bora Afrika Mashariki.

Mchungaji Devis Swalo, ambaye ni miongoni mwa wakazi wa Kijiji cha Kimani, alisema wanaishukuru serikali kupitia Tawa kwa uhifadhi uliofanyika katika hifadhi hiyo na kwamba hata wao wananufaika japo changamoto ni ongezeko kubwa ya watu.

Alisema baadhi ya wananchi kutoka maeneo mengine nchini wanahamia katika vijiji hivyo kutokana na uzuri wa maji yanayopatikana kwenye vyanzo vya mto Kimani.

"Haya maji ni bora sana maana wanakuja watu kutoka mataifa mbalimbali wakiwamo wataalamu kutoka GTZ kwa ajili ya kuhakiki maji haya na wamethibitisha kuwa ni maji bora kabisa na yamekuwa yakiwavutia watu wengi kuishi hapa," alisema Mchungaji Swalo.

Maofisa wa Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyama Pori (Tawa) ambao ndio wenye jukumu la kutimiza mpango wa kutunza vyanzo vya Mto Kimani, wanawataka wananchi wa vijiji hivyo kutunza mazingira ili waendelee kufurahia maji mazuri na hali ya hewa nzuri.

Mmoja wa maofisa hao, Suzan Chenya, alisema wanakabiliana na changamoto mbalimbali kwenye uhifadhi wa vyanzo vya mito ikiwamo baadhi ya wananchi kuingia kinyemela ndani ya hifadhi na kukata miti kwa ajili ya kuni za kupikia majumbani.

Alisema hali hiyo inasababisha uharibifu wa mazingira na maji kupungua kwenye baadhi ya vyanzo, hivyo aliwataka wananchi kuacha tabia hiyo.

"Maji wanayotumia yanatoka ndani ya hifadhi, tusingehifadhi vizuri eneo hili pengine wananchi hawa wasingekuwa wanapata maji kabisa kwa hiyo ili waendelee kunufaika ni lazima na wao washiriki katika kutunza mazingira," alisema Suzana.

# Wahoji mil.10/- za ujenzi wa vyoo zilikokwenda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJUMBE wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Iyela jijini Mbeya, wameingiwa na wasiwasi kuhusu matumizi ya Sh. milioni 10 zilizotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya ujenzi wa vyoo katika shule za msingi Nero na Mapambano zilizopo Kata ya Iyela.

Mradi wa ujenzi wa vyoo hivyo ulianzishwa na wadau wa maendeleo akiwamo Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson na Ndele Mwaselela ambao walijenga mpaka usawa wa lenta na kutakiwa kuezekwa ili wanafunzi waanze kuvitumia.

Wasiwasi wa matumizi ya fedha hizo uliibuka mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata hiyo na kudai kuwa ujenzi wa vyoo hivyo bado haujakamilika licha ya fedha kutolewa na hakuna maelezo ya kujitosheleza ya usahihi wa matumizi ya fedha hizo.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Said Mwaituka alisema wananchi wa mitaa ya Nero na Mapambano waliaanza muda mrefu kujenga vyoo hivyo, lakini hawakufanikiwa kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo za kifedha.

Alisema mwaka 2009 walichimba shimo, lakini baadaye walilifukia kutokana na kushindwa kujenga na ndipo mwaka jana wadau wakajitolea na kuendeleza mradi huo ndipo wakaungwa mkono na serikali.

"Baada ya wadau wetu kuanza ujenzi wa mradi huu, mbunge naye alifanya ziara katika shule hizi na kujionea hali ya vyoo ndipo akaahidi kuleta fedha za mfuko wa jimbo na zililetwa, lakini mpaka sasa ujenzi haujakamilika na hatujui kama fedha zimeisha ama zipo," alisema Mwaituka.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mapambano, Asheli Mpetele, alikiri fedha hizo kupokelewa na Ofisi ya Mtendaji wa kata hiyo na kisha kugawanywa kwa shule zote mbili na kwamba taarifa sahihi anazo Ofisa Mtendaji wa Kata.

Alisema fedha hizo ziligawanywa shilingi milioni tano kila shule na kwamba wakati wa manunuzi wao hawakuhusika isipokuwa shughuli zote zilikuwa zinafanywa na ofisa mtendaji ambaye hakuwapo kwenye kikao kwa madai kuwa anaumwa.

"Mimi wakati wa manunuzi sikuwapo nilikuwa nimetoka kidogo, lakini wakati narudi nilikuta tayari bati zimenunuliwa na hivyo sikuwa na sababu ya kuhoji kwa sababu ilikuwa ni utekelezaji na nilitegemea mtendaji ataleta taarifa," alisema Mpetele.

Kwa upande wake mdau wa maendeleo, Mwaselela ambaye ni miongoni mwa walioshiriki kuanzisha mradi huo, alisema fedha hizo zilipelekwa katika kata hiyo tangu mwezi Desemba mwaka jana na ujenzi ulitakiwa ukamilike mwezi Februari.

Alisema baada yeye na Dk. Tulia kuanza ujenzi huo pia Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alichangia mifuko ya saruji ili kuunga mkono juhudi hizo na hivyo akataka maelezo ya uhakika kuhusu matumizi ya fedha.

Alisema walikubaliana kukutana leo ili wapate ufafanuzi kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata hiyo ambaye ndiye aliyepokea fedha hizo kutoka kwa Mkurugenzi wa Jiji.





## Mashine za kisasa upimaji ardhi kuboresha jiji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za upimaji ardhi na urasimishaji wa makazi, Kampuni ya Land Network ya jijini Dodoma kwa kushirikiana na kampuni ya utengenezaji wa vifaa vya upimaji ardhi Kolida ya nchini China, wameleta mashine za kisasa ambazo zitasaidia katika kuboresha jiji hilo kwa haraka. Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Land Network, Samwel Ikwabe, alisema kuwa mashine hizo walizoingiza nchini zitasaidia kufanya upimaji wa Jiji la Dodoma kwa haraka na kwa gharama nafuu.

Alisema kutokana na uwezo wa mashine hizo ambazo zinasambazwa duniani kote na kampuni hiyo, zinaouwezo wa kufanya kazi katika mazingira yote na kuwataka wakazi wa Dodoma kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema kutokana na serikali kuhamia Dodoma changamoto ya suala la upimaji ardhi imekuwa kikwazo, hivyo ujio wa mashine hizo utasaidia kukabiliana nayo. “Maeneo mengi bado hayajapimwa hivyo kuwa moja ya sehemu ya migogoro ya ardhi, lakini pia wananchi wanaomiliki mashamba au ardhi kwa ujumla hawana faidi nazo kutokana na kutopimwa hivyo kupitia mashine hizo watapata fursa ya kupimiwa na kurasimishiwa makazi na kupata hati ya maeneo yao kwa gharama nafuu,” alisema Ikwabe. Aidha, alisema mashine hizo wanaweza kuzikodisha kwa wapimaji ardhi binafsi au wale wa halmashauri ambao zinachangamoto ya vifaa vya upimaji ardhi katika maeneo yao.

“Kupitia mashine hizi Dodoma kila mtu atakuwa na uwezo wa kupimia kipande cha ardhi yake ili kiwe na tija kwa haraka na kwa bei nafuu,” alisema.

Vilevile alisema kutokana na serikali kutaka kwenda katika uchumi wa kati wananchi wakiweza kupimiwa maeneo yao watapata fursa ya kutumia maeneo yao kujipatia mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha.

Alisema upimaji wa ardhi nchini utasaidia kuondoa tatizo la ujenzi holela, uvamizi wa maeneo hivyo kuwa na miji iliyojengwa na katika mpangilio mzuri tofauti na ilivyo sasa katika maeneo mengi. Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa kampuni hiyo, Willson Waitara, alisema mashine hizo zilizoletwa kwa ajili ya upimaji ardhi kwa gharama nafuu pia watazitumia katika kufundishia wanafunzi waliopo katika vyuo mbalimbali.

Alisema wanafunzi katika vyuo vikuu ambao wamekuwa wakisoma masuala ya uhandisi wanapata fursa ya kupata mafunzo ya matumizi ya mashine hizo ili waweze kuendana na teknolojia za kisasa katika nyanja ya upimaji ardhi.

“Kampuni hii ya Kichina ni ya muda mrefu ambayo imeanzishwa toka mwaka 1989, ni takribani miaka 30 sasa hivyo hawa wenzetu teknoljia yao ipo juu hivyo basi vijana wetu watapata fursa ya kujifunza na kupata ujuzi katika mashine hizi,” alisema.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa Kimataifa wa kampuni hiyo, Andy Lau, alisema mashine hizo zimetengenezwa katika ubora wa hali ya juu na zitasaidia kupimia ardhi kubwa kwa muda mfupi na kwa ubora zaidi.

# Ataka timu kusikiliza malalamiko ya wakulima korosho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amemtaka Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kabla ya kuingia msimu mpya wa korosho aunde timu ndogo ya wataalamu itakayozunguka kila wilaya kusikiliza malalamiko ya wakulima.

Akichangia mwishoni mwa wiki, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2019/20 bungeni, Chikota alisema bado kuna malalamiko kwa wakulima hivyo ni vyema waziri huyo akaunda timu ndogo yenye watumishi waadilifu.

“Kwa sababu pale katikati ulishuhudia kuna vijana wako hawakuwa waadilifu, ulichukua hatua za makusudi mapema ili kuzuia dalili za rushwa zisiendelee,” alisema.

Chikota alitoa mfano kuwa kuna mkulima ameuza korosho kilo 500, lakini amelipwa kilo 300 na akienda kwenye uongozi wa chama cha ushirika (Amcos) anaaambiwa hawajahusika, hivyo aunde timu hiyo kushughulikia changamoto kama hizo. Alisema kuna maeneo kama kwenye Amcos kuna akaunti za wakulima 200 zimefungwa hivyo malalamiko ya wakulima kufungiwa akaunti zao na pindi wahusika wanapofuatwa huwapiga danadana. Akizungumzia suala la ubanguaji, Chikota alisema suala la korosho bado ni changamoto kutokana na ubanguaji kupelekwa nje ya nchi licha ya nchi nyingine kufanya vizuri, hivyo sasa ni muda wa kujikita kwenye suala hilo.

Alishauri kuwa kwa kuwa vipo viwanda 12 vya awali vilivyojengwa na havifanyi kazi, ni muda sasa wa kuvifufua na wawekezaji wapya waliojitokeza kujenga wapewe nafasi ili ubanguaji ufanyike hapa nchini.

“Nashauri serikali yangu sikivu iweke vivutio kwa wawekezaji hao na kupunguza kodi kwa mitambo na mashine mpya zitakazoingizwa ili gharama za uwekezaji zipungue na kwa kufanya hivyo korosho itaongeze ajira na ongezeko la thamani hivyo mkulima kuongeza kipato,” alisema.

Aliongeza kuwa tasnia ya korosho ina mambo mengi hivyo inahitaji usimamizi mkubwa.

Alimwomba waziri kuunda bodi mpya ili kusimamia tasnia hiyo kutokana na iliyokuwapo kuvunjwa mwaka jana.

“Ni muda mwafaka sasa kuundwa bodi hiyo kwa kuwa kuna watu wapo waaminifu, hivyo watafutwe ili kusimamia suala la korosho na matatizo yaliyojitokeza yasijitokeze tena,” alisema.

Alisema kuwa vyama vya ushirika vilipaswa kuwa mkombozi kwa wakulima, lakini kilichotokea ni kuwa watumishi wanaumiza wakulima badala ya kuwasaidia.

Alisema kwa kiasi kikubwa changamoto au ubadhirifu mwingi kwenye zao hilo hufanywa na watumishi wa ushirika na kumshauri waziri mwenye dhamana kufuatilia suala hilo kwa kuwahamisha.

“Watumishi wengi wa ushirika wamekaa pale muda mrefu hivyo wahamishwe kwenye korosho wapelekwe wizara nyingine ili wakasimamie mazao mengine au afumue uongozi kutokana na kuwa kuna uozo na mzigo mkubwa kwa wakulima,” alisema.

Alimpongeza Rais John Magufuli kwa maamuzi ya kijasiri aliyochukua ya kuamua kununua korosho baada ya kuona kampuni inayumba.

Alisema sekta ya korosho inahitaji fedha nyingi ndio maana baada ya maamuzi yake aliamua kuvunja bodi ya korosho na kuagiza bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko kusimamia zoezi hilo.

Hata hivyo, alisema bado kuna changamoto kutokana na uwapo wa baadhi ya wakulima ambao bado hawajalipwa wanaodai takribani Sh. bilioni 100.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athumani Masasi, akizungumza na madiwani wa halmashauri hiyo kwenye kikao cha baraza cha taarifa ya utekelezaji kutoka kwenye kata kilichofanyika Chamwino mkoani Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Marufuku kubeba nyama vichwani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Afya wa Jiji la Dodoma, Abdallah Mahia, amepiga marufuku wabeba nyama kubeba vichwani, mgongoni na mabegani kwa kuwa wanahatarisha afya za walaji.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mahia alisema wabebaji hao wanatakiwa kuzingatia kanuni za usafi kwa kubeba kwenye matoroli zikiwa zimefunikwa kwenye mifuko maalum ili kuepuka magonjwa ya kuambukiza.

“Pia hawa wabebaji wanatakiwa kupima afya zao na kuwa na vifaa kama vile sare, koti, kofia na viatu, vyote vyeupe, lakini na hizo nyama hazipaswi kubebwa vichwa, mabegani au mgongoni, inatakiwa wabebe kwenye matoroli maalum tena zikiwa zimefunikwa na mifuko maalum,” alisema.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 na Sheria ya Chakula, Afya, Vipodozi ya mwaka 2003 ambayo inatoa mwongozo wa usafirishaji wa nyama wa mwaka 2006, inakataza ubebaji wa aina hiyo ili kuepuka magonjwa ya kuambukiza.

Alisema watakaokiuka sheria na kanuni hizo watalazimika kuchukuliwa hatua ikiwamo ya faini ya kifungo cha miezi mitatu.

“Watalipa faini ya Sh. 100,000 kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii,” alisema na kuongeza:

“Hizi kanuni na sheria ni muhimu zikazingatiwa kwa wabebaji hao wa nyama na wasafirishaji na hata kwa walaji pia, lengo ni kuhakikisha ulindaji wa afya kwa walaji na wao wenyewe ili kusiwapo na maambukizi yoyote ya magonjwa.”

Aliwataka wamiliki wa maduka ya nyama kuhakikisha kwenye maeneo yao yanazingatia usafi wa mazingira ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko yanayoweza kujitokeza kutokana na uchafu.





Waathirika wa mvua za masika wakimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa Wilaya ya Mjini Magharibi ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Marina Thomas, wakati wa ugawaji wa vyakula kwa waathirika hao vilivyotolewa na serikali kupitia Idara ya Maafa katika eneo la Shule ya Msingi Jang'ombe. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wazazi wahimizwa malezi kwa watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Rizki Pembe Juma, amewataka wazazi kurudisha malezi kwa watoto kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ili kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa watoto.

Akizungumza katika uzinduzi wa vuguvugu la kuhamasisha malezi bora na matunzo ya familia Zanzibar, alisema changamoto kubwa inayowakumba wazazi katika malezi bora Zanzibar ni kuondoa malezi ya pamoja ambayo yangesaidia katika kumlea mtoto kukabiliana na vitendo viovu ikiwamo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema mzazi pekee hawezi kumlinda mtoto pasipokushirikiana na jamii inayomzunguka katika kumlinda. "Zamani wazazi walikuwa wanalea watoto kwa pamoja na ilikuwa rahisi hata kumlinda mtoto, walikuwa wakitumia njia ya mtoto wa mwenzio ni wako, lakini hivi sasa malezi hayo hayapo tena," alisema.

Alilishukuru Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) kwa kuunga mkono jitihada za serikali katika kuhakikisha watoto wanalindwa na kupatiwa haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Mwakilishi wa UNICEF Zanzibar, Maha Damachi, alisema serikali ya Zanzibar imechukua jitihada mbalimbali katika kuwalinda na kuwatunza watoto.

Alisema wazazi wanapaswa kuzingatia vitu vitano katika malezi ya watoto ambavyo vikifanyiwa kazi lengo la malezi bora kwa watoto litatimia.

Akiyataja mambo hayo ni kuwatunza watoto, kuwalinda, kuongea nao, upendo pamoja na kujenga familia ambapo mambo hayo yote jitihada za pamoja zinahitajika katika kufikia malezi bora kwa mtoto. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mwanajuma Majid, alisema talaka ni changamoto katika malezi bora kwa watoto.

Alisema kupitia kitengo cha uhifadhi wa mtoto kwa mwaka 2017/ 2018 walipokea malalamiko 294 kati ya hayo, 175 ni matunzo ya watoto na 119 ya mvutano wa malezi baada ya ndoa kuvunjika.

Aidha, alisema kuwa bado kuna mwamko mdogo katika malezi bora hususani kwa wanaume wanadhani jukumu la kumlea mtoto ni la mwanamke pekee jambo ambalo sio sahihi.

# Mafuriko yaathiri nyumba 2,900

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDARA ya Maafa Zanzibar imesema kuwa jumla ya nyumba 2,911 zimeathiriwa Unguja na Pemba kutokana na athari za mvua za masika zinazoendelea kunyesha.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati akikabidhi msaada wa vyakula kwa waathirika katika shehia 12 za mkoa wa Mjini Magharibi, Mkurugenzi wa idara hiyo, Makame Khatib Makame, alisema nyumba hizo baadhi yake wananchi wake wamesharejea katika makazi na nyingine bado hazikaliki kutokana na kujaa maji.

Alisema serikali haijaweka kambi ya kuwahifadhi waathirika hao badala yake wamekuwa wakitoa msaada wa vyakula. "Leo tumeanza na shehia 12 kuwapatia msaada wa vyakula kama mchele, unga wa ngano, sukari na mafuta kwa wale wote walioathirika na mvua hizi," alisema. Alieleza kuwa familia zilizoathirika ambapo nyumba zao hazikaliki wanaendelea kupatiwa hifadhi kwa ndugu, jamaa na majirani zao.

Alieleza kuwa watu saba wamejeruhiwa kutokana na upepo mkali uliombatana na mvua, ambapo watoto wawili waliangukiwa na kiambaza cha nyumba huko Chuwini. Alisema pia watoto wanne wa familia moja waliangukiwa na mnazi huko Mwera Unguja na mtu mmoja huko Pemba aliangukiwa na mnazi kutokana na upepo mkali.

"Tunashukuru kuwa hakuna kifo kilichoripotiwa kutokana na maafa ya mvua hizi za masika," alisema mkurugenzi huyo.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha hadi Juni.

Waathirika hao walipongeza serikali kutokana na msaada huo wa chakula ambacho kitaweza kuwasaidia hasa katika kipindi hiki cha mfungo wa mwezi wa Ramadhani.

Zaidi ya shilingi milioni 200 zimetumika kwa ajili ya kuwafariji waathirika wa mvua hizo kwa kuwanunulia chakula, ambapo chakula hicho kimeanza kutolewa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na zoezi hilo litaendelea kwa mikoa mingine.

# Wanahabari waaswa amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia kalamu zao vizuri kwa kutoa habari za kweli zilizofanyiwa uchambuzi ili zisiweze kuleta athari kwa jamii.

Akizungumza na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) katika mkutano mkuu wa jumuiya hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kuandika taarifa za ukweli kutaepusha nchi kuingia katika majanga ambayo yatasababisha machafuko kama nchi nyingine duniani.

Ayoub, alisema hakuna sababu ya kutumia kalamu au kamera kuchochea mambo ambayo hayana dhamira njema na nchi.

"Mengi ya majanga yanayojitokeza katika nchi mbalimbali yanatokana na wanasiasa na msingi wake mkubwa unatokana na habari... sasa tujitahidi habari zetu zisipelekee nchi yetu kuingia katika majanga kama hayo," alisema.

Alieleza kuwa tasnia ya habari ni moja ya tasnia muhimu sana kwa mustakabali wa kiuchumi, kijamii, kisiasa pia ni daraja la kuunganisha jamii na jamii.

Alisema, vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa kwa mustakabali wa taifa na nyanja mbalimbali hasa kuchukua jukumu lao kama ni sehemu ya kuelimisha amani na utulivu.

Aliwasisitiza wanahabari kuendelea kulinda uhuru wao kwa kutoa habari zote zilizokuwa na umuhimu na ambazo hazitaleta athari kwa jamii na kutotumia mihemko ya kisiasa kuwa ndio habari ambazo zinaweza kuleta vurugu na machafuko. "Kuna vyombo vingi vya habari duniani havina uhuru mkilinganisha na hapa kwetu na nyinyi mmebainisha hilo, basi endeleeni kulinda uhuru wenu wa habari kwa kuandika habari za kweli," alisema.

Pia aliwaomba viongozi wa serikali na viongozi wa majimbo kutumia vyombo vya habari ili kufikisha taarifa za maendeleo zinazofanywa na serikali ili wananchi waweze kuzijua.

Ayoub alisema tasnia ya habari ina changamoto nyingi hasa waandishi wa vyombo binafsi kutopewa mikataba na kutolipwa mishahara yao, hivyo aliwasihi wamiliki wa vyombo hivyo kuwapa mikataba wafanyakazi wao kwani kutofanya hivyo ni kosa.

Akizungumzia suala la demokrasia Ayoub, alisema ni vyema kwa waandishi wa habari waendelee kuitumia demokrasia iliyopo kwa kuipa jina Zanzibar na kuepusha kuichafua ili mapato yaweze kuongezeka kupitia sekta ya utalii.

Naye Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous, alivitaka vyombo vya habari kuacha kuchochea mambo ambayo yanaweza kuleta taswira mbaya katika nchi.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar, Abdalla Abdul-rahman Mfaume, aliwataka wanahabari kuzingatia amani, usalama na utulivu wa nchi pamoja na usalama wao wenyewe binafsi kwa kufanya mambo yatakayowaepusha na matatizo. Aliuomba uongozi wa mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Habari na Mambo ya Kale na ZEC kuazimia kutoa elimu ya mwongozo kwa wanahabari na vyombo vya dola wakati wa uchaguzi kwa kushirikiana na klabu.

## HABARI MIKOANI

# Viongozi wababe CCM waonywa

**Na Dege Masoli,** TANGA

VIONGOZI wa nafasi mbalimbali wameonywa kuzingatia haki na kutambua kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kuzuia machafuko, na kwamba hayo yatakuwa baraka na mwisho mwema kwa wanaowaongoza.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tanga, Meja mstaafu Hamis Mkoba, alitoa kauli hiyo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kilichokutana mwishoni mwa wiki jijini hapa.

Mkoba alimtaka kila kiongozi awajibike kusimamia haki kwa anaowaongoza ili kudumisha umoja, mshikamano na amani kwa ujumla na kwamba chama hakitakuwa radhi na yeyote atakayekwenda kinyume cha hayo kwa kuwa mtu huyo hana mwisho mwema kwa wananchi.

Alisema kuwa haki ndiyo njia pekee ya kuzuia machafuko mahala popote na kwamba hakuna mbadala wa hilo, hivyo kila aliyepewa dhamana ya uongozi kwa ngazi yoyote kama ni mfia amani wa kweli hanabudi kusimamia haki sawa kwa kila mmoja bila kubagua.

Alieleza kuwa kudumisha umoja na mshikamano uliopo ni kuzingatia mustakabali mzima wa haki sawa kwa kila mtu kwa kutambua kwamba hakuna mwenye thamani zaidi ya mwingine na hiyo ni kwa mujibu wa katiba ya nchi na haki za binadamu.

Alilipongeza Baraza la Madiwani wa Jiji hilo kwa kile alichokieleza kufurahishwa na namna ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo kuzingatia usahihi wa matumizi ya fedha, jambo ambalo alidai limeiwezesha kukamilika kwa wakati na kwa gharama stahiki.

Alieleza kuwa chama kimefarijika kwa maendeleo makubwa yaliofanyika katika sekta ya afya na elimu, ambapo alisema kuwa maendeleo hayo yanaleta faraja kwa chama kwa kuwa huduma zilizosogezwa kwa wananchi ni zenye ubora.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Tobias Mwilapwa,

Seleman Zumo, aliwataka madiwani hao kuongeza udhibiti wa matumizi ya fedha za serikali wanazopewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili kazi hizo ziwe ufumbuzi wa kero za jamii katika wilaya hiyo.




Foleni kubwa ya malori kutoka Bandari ya Dar es Salaam ambayo imelalamikiwa na madereva wa magari hayo ambao wamesema inatokea wanapofanyiwa ukaguzi katika mashine za kukagua mizigo inayotoka ama kuingia. **Habari Uk. 10.** **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tafiri yaomba kusaidiwa vifaa vya maabara

**Na Renatha Msungu,** KIGOMA

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) mkoani Kigoma imeiomba serikali kuwasaidia vifaa vya maabara vya kisasa kwa ajili ya kufanyia utafiti kuepuka kupata madhara ya kemikali zinazotumika katika baadhi ya utafiti wao.

Kemikali ambayo huitumia katika kazi zao ni ya madini tembo ambayo baadaye husababisha kansa, ikiwamo kuzaa watoto wenye ulemavu.

Akizungumza na gazeti hili jana Mtafiti Mwandamizi wa Tafiri Kigoma, Julieth Mosille, alisema kunahitajika vifaa vya kufanyia utafiti vya maabara ili waweze kupata matokeo chanya katika kazi zao. Alisema vifaa hivyo vinawasaidia kukwepa moja kwa moja madhara ya madini tembo (mercury) kutozishika wakiwa na vifaa hivyo.

Julieth alivitaja vifaa hivyo ni Autocleve, Water Bath na Dish Washer ambavyo vinasaidia kutoshika kemikali zenye madhara kwa binadamu. Alifafanua zaidi kuwa wao bado wanatumia njia za kizamani tofauti na nchi za wenzao ambazo wapo juu zaidi katika kufanya utafiti wao.

Naye Ofisa Mtafiti Mwandamizi wa Tafiri Kigoma, Athanasio Bonde, alisema serikali inapaswa kuwasaidia vifaa vya kisasa ili waweze kuboresha zaidi kazi zao za kila siku. Alisema muda mwingine wanashindwa kufanya kazi kwa wakati kutokana na uhaba wa vifaa vya kiutendaji ambavyo vingi ni vya kizamani.

Alisema kutokana na hilo utafiti unashindwa kufanyika, ikiwamo kuangalia upunguaji wa vyakula vya samaki majini, jambo ambalo ni tatizo kubwa kwao.

Alisema wamekuwa wakipata misaada toka kwa wafadhili, lakini wanashindwa kuendelea kutokana na kupungukiwa vifaa na wao hawana fedha.

Kwa upande wa Lovette Mwansasu, alisema wana changamoto kubwa sana ya ufanyaji kazi zao hasa pale mabadiliko ya tabianchi yanapotokea wanashindwa kwa sababu ya kukosa baadhi ya vifaa.

# Wazazi wasusia tamasha la mama na mwana Dar

**Na Romana Mallya**

ASILIMIA 90 ya waliojitokeza kusherehekea Siku ya Makumbusho Duniani ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, huku mwitikio wa wazazi ukiwa mdogo licha ya sherehe hizo kubebwa na tamasha la mama na mwana.

Siku ya Makumbusho Duniani iliazimishwa Jumamosi, huku kauli mbiu ikiwa ni "Makumbusho kitovu cha utamaduni: Hatima ya mila na desturi".

Nipashe ilishuhudia idadi kubwa ya wanafunzi kutoka shule za msingi na sekondari za Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani wakishiriki maadhimisho hayo yaliyofanyika kitaifa kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama jijini Dar es Salaam ambapo washiriki walianza kwa maandamano na baadaye kutembelea nyumba za makabila tofauti zilizopo eneo hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama, Agnes Robert, alisema washiriki wamepata fursa ya kujionea utamaduni wa makabila mbalimbali uliopo kwenye nyumba hizo. "Kila nyumba iliyopo hapa imejengwa kwa asili ya kabila husika, nyumba za asili ya Wachaga, Wazaramo, Wahaya, Wasukuma, Wahehe na makabila mengi zipo hapa na watu wamejifunza namna asili zao zilivyo, namna nyumba zao zinavyojengwa, wengine zinamazizi ya ng'ombe ndani, vitanda vya miti, ngozi. Yapo mengi ya kujikumbusha bila kusahau vyakula vya asili tulivyopika leo," alisema.

Mwanafunzi wa darasa la nne, Irene Ernest, katika Shule ya Msingi Mikocheni A, alisema hiyo ni mara yake ya kwanza kwenda Makumbusho kujionea mambo ya kale.

"Tuliambia maadhimisho haya yatakuwa na tamasha la mama na mwana, wazazi wamekuwa wachache sana, sijui ni kwa nini, nawaomba wazazi wakati mwingine wajitokeze kwa wingi ili kujifunza mila na desturi," alisema.

Irene alisema katika makumbusho hayo ameona nyumba za Wahehe, ngoma za asili na amekula chakula cha asili ikiwamo chai ya mashona nguo ambayo inaongeza damu mwilini.

"Kuna vitu vingi vya kujifunza na kikubwa nimejifunza makabila tumetofautiana kidogo, nyumba za makabila zilizopo hapa karibu zote zimejengwa kwa nyasi tofauti ni muundo tu wengine walijenga kwa kuweka paa ndefu wengine mviringo na makabila mengine nyumba zao ni za kuta za pembe nne," alisema. Irene aliwashauri wanafunzi na wazazi kwenda kwenye vijiji vya makumbusho ili wajionee namna asili yao ilikotoka kwa sababu ndio njia pekee ya kurudisha maadili ya Mwafrika.

Mwanafunzi wa darasa la tatu, Erick Godfrey, katika Shule ya Msingi Makumbusho, alisema baada ya kutembelea nyumba za asili amejionea vitu mbalimbali ikiwamo mikuki, vyombo vya asili vya kuhifadhia maziwa, maji na kamba za kufungia ng'ombe.

"Nimeona mkuki ambao babu zetu waliutumia kama silaha yao ya kujikinga na wanyama wakali, vipo vitanda vya aina mbalimbali kulingana na makabila ambavyo karibu vyote vilitengenezwa kwa miti na kutandikwa ngozi," alisema.

Katika sherehe hizo watoto walipata fursa ya kuona tofauti ya ngoma za asili na nyimbo za kizazi kipya 'bongo fleva' ambapo zile za mababu na bibi zililenga zaidi maadili ya Mwafrika.

## HABARI KIMATAIFA

# Salva Kiir awafukuza kazi mabalozi 40

**JUBA, Sudan Kusini**

SERIKALI ya Sudan Kusini imesema imewatimua wawakilishi wake wa kibalozi 40 waliopo katika nchi za nje.

Sababu za kuwafuta kazi wanadiplomasia hao ni hawakuonekana kazini kwa miaka mingi, hivyo wameondoshwa kwenye mfumo rasmi wa malipo.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Sudan Kusini, Mawien Makol, alieleza kuwa serikali ilijaribu kuwasiliana na maofisa hao bila ya mafanikio, ikiwa pamoja na wale waliokuwa wanaiwakilisha nchi yao Marekani na Uingereza.

"Hakuna ofisa hata mmoja aliyejibu au aliyerejea nchini Sudan Kusini. Kwa bahati mbaya wizara hiyo haikuwa na njia nyingine ila kuwatimua mabalozi hao baada ya juhudi kubwa kushindikana ya kuwataka warejee nyumbani na kufanya kazi nchini," alisema Makol.

Alisema hatua ya kuwafukuza kazi viongozi hao imetokana na wao kutorejerea nyumbani baada ya mihula yao kumalizika.

Makol alisema kuwa mabalozi hao hawajulikani waliko na majina yao yamechapishwa hadharani na kwamba wote waliorodheshwa hawatalipwa tena mishahara yao na wameachishwa kazi, wameamriwa kurejesha pasi zao za kusafiria pamoja na zile za familia zao.

Pia wametakiwa kukabidhi hati hizo kwenye balozi za Sudan Kusini zilizopo karibu nao.

Makol alisema tamko la kuwafukuza kazi inatokana na sheria inayohusu masuala ya kibalozi ya mwaka 2011.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, yeyote ambaye haendi kazini kwa muda wa zaidi ya siku 45 bila ya kutoa maelezo atahesabika kuwa ameacha kazi.

*DW*

# Rais mstaafu Kenya apigwa faini kwa kumdhulumu mjane

**NAIROBI, Kenya**

MAHAKAMA nchini Kenya imemuamuru Rais wa zamani wa Kenya, Daniel Arap Moi, kulipa fidia ya Dola za Marekani milioni 1.06 kwa mjane ambaye alimnyang'anya ardhi yake kinyume cha sheria.

Imeelezwa kuwa Moi alinyakuwa ardhi ya heka 53 iliyokuwa mali ya mjane Susan Cheburet Chelugui.

Moi alichukua ardhi hiyo kinyume cha sheria miaka 36 iliyopita, lakini ilisajiliwa kwa jina la Moi mwaka 2007.

Mume wa mjane huyo Chelugui Noah Chelugui alikuwa chifu wakati wa utawala wa Rais Moi.

Rais huyo wa zamani ambaye ndiye rais aliyekuwa madarakani kwa muda mrefu zaidi, alishutumiwa na Chelugui na mtoto wake wa kiume David Chelugui kwa kusajili ardhi ya familia yao kwa jina lake miaka miwili baada ya mume wake, Chelugui kufariki dunia.

Inasemekana baadaye Moi aliiuza ardhi hiyo kwa kampuni ya utengenezaji wa mbao Plywood Limited.

Kampuni ya Rai Plywood Limited iliwaeleza majaji kuwa ilinunua ardhi hiyo kutoka kwa Moi mnamo mwaka 2007 baada ya kufanya uchunguzi wa kina wa kisheria kuhusu ardhi hiyo.

Hata hivyo, Moi hakuweza kuipatia mahakama ushahidi wowote juu ya namna alivyoipata ardhi hiyo.


Jaji aliyeendesha kesi hiyo, Anthony Ombwayo alisema Moi alikuwa na mienendo ya isiyo ya kawaida, ukiukaji katiba, kutofuata utaratibu na yenye dosari.

Moi alikuwa Rais wa pili wa Kenya mwaka 1978, ambapo alihudumu hadi mwaka 2002. Alilitawala taifa hilo kwa mkono wa chuma na alishutumiwa kwa ukiukwaji wa haki za binadamu. Kutokana na shinikizo la kimataifa, aliruhusu uchaguzi wa vyama vingi mnamo mwaka1992 uliotawaliwa na ghasia kwa madai ya kuwapo kwa wizi wa kura.

Kumekuwa na kesi nyingi za unyakuzi wa ardhi Kenya unaodaiwa kufanywa na viongozi wa ngazi ya juu ya serikali na wafanyabiashara matajiri kwa miaka mingi, lakini waathiriwa hawana utashi wala pesa za kukabiliana na watu hao.

Ufisadi katika mfumo wa mahakama nchini Kenye ni tatizo kubwa. Wakati mzozo unapopelekwa mahakamani, kesi huzoroteshwa kwa miaka mingi. Wengi wanamatumaini kuwa hukumu iliyotolewa dhidi ya Moi itaonekana kama jaribio na kwamba itatuma ujumbe kwa watu kwamba hawawezi tena kunyang'anya ardhi za watu maskini.

*BBC*



Kiongozi wa Upinzani wa Sudan Kusini, Riek Machar (kushoto), na Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir walipokuwa kwenye mazungumzo ya amani nchini Uganda. Katikati ni Rais wa Uganda, Yoweri Museveni. **PICHA: REUTERS**

# Tshisekedi kumtaja Waziri Mkuu wiki ijayo

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, amesema kuwa Waziri Mkuu mpya atafahamika wiki ijayo.

Rais Tshisekedi ametoa kauli hiyo wakati alipokutana na mabalozi wa umoja wa Ulaya, pamoja na mmoja kutoka Canada jijini Kinshasa siku ya Jumamosi.

Hilo pia limethibitishwa na msemaji wa Rais Tshisekedi, Kasongo Mwema Yamba Y'amba, kupitia ukurasa wake wa Twitter, ambaye ameandika kuwa 'Rais Tshisekedi amewaambia mabalozi hao kuwa, waziri mkuu amepatikana.

Wananchi wa DRC wanasubiri kwa hamu kuona ni nani atakuwa waziri mkuu kwa sababu kwa mujibu wa katiba ya Congo anastahili kutokea kwenye chama chenye wabunge wengi, kwa sasa muungano wa kisiasa wa Rais wa zamani, Joseph Kabila ndio ulio na wabunge wengi.

Tangu alipoingia madarakani mapema mwaka huu Rais Tshisekedi hajafanikiwa kuunda serikali yake.

*RFI*

# Mazungumzo ya mwafaka wa Brexit yavunjika

**LONDON, Uingereza**

CHAMA cha upinzani nchini Uingereza cha Labour kimevunja mazungumzo ya Brexit ya kupata mwafaka na Waziri Mkuu, Theresa May na kulalamika kuwa mamlaka yake yanafikia ukingoni.

Kiongozi wa chama cha Labour, Jeremy Corbyn, alisema mpasuko kati yao hauwezi kumalizika na kwamba hali ya kujihami kwa Theresa May haipo tena kwa sababu muda wake wa utawala unakaribia mwisho.

Corbyn alisema chama cha Labour kitaendelea kupinga makubaliano yaliyofikia na serikali kama yalivyo hivi sasa. Wabunge wa chama hicho waliyakataa makubaliano yaliyofikiwa na May na Umoja wa Ulaya (EU) mara tatu na kumlazimisha kuchelewesha tarehe ya Uingereza kujitoa katika jumuiya hiyo, muda wa mwisho ni Oktoba 31.

Bunge la Uingereza linatarajia kupiga kura kwa mara ya nne mwanzoni mwa mwezi Juni kuhusiana na masharti ya Uingereza kujitoa kutoka EU.

Akizungumza katika kampeni kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa bunge la EU, May alisema wabunge watakabiliwa na uamuzi mgumu wa kupiga kura kukubalina na Brexit ama kukataa tena.

Uingereza haikutaka kushiriki katika uchaguzi huo, lakini itafanya hivyo kwa sababu ya kuahirishwa kwa Brexit.

Kuvunjika kwa mazungumzo hayo kumetokana ikiwa imepita siku moja baada ya May kukubali kuweka muda maalum kwa ajili ya kuachia wadhifa wa uwaziri mkuu kufuatia kura ya kujitoa kutoka EU.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika mkutano wa faragha pamoja na wanachama na viongozi wa wabunge wa chama cha Conservative.

Inaelezwa kuwa May atazindua mpambano wa kuwania nafasi ya uongozi mara muswada wa makubaliano ya kujitoa ama ukishindwa.

*DW*

## HABARI KITAIFA

# Jaji Mkuu awafunda viongozi wa dini

INATOKA UK. 4

ambayo wamekuwa wakiyatoa kwa jamii na kuwa msingi bora katika kuboresha nchi yetu, hivyo ili kuwa na nchi yenye amani na mshikamano tunawategemea wao kama muhimili muhimu sana," alisema Prof. Juma.

Prof. Ibrahim, aliongeza kwa kuwataka viongozi hao wa dini kuendelea kulivalia njuga suala la migogoro ya mirathi kwa sababu limekuwa sugu na kutoleta maelewano katika jamii hasa kwa wajane na yatima.

"Viongozi wa dini ni kioo cha jamii kwa kuwa mna ushawishi mkubwa kama mkiamua kujenga au kubomoa, hamshindwi kitu chochote hivyo ni vyema kuona ushirikiano wenu unazidi kuimarika ili kuzidi kuifanya nchi yetu kuwa na maadili," alisema Prof. Juma.

Alisema mataifa mengine yamekuwa yakikosa ushirikiano baina ya taasisi za dini jambo ambalo limekuwa likichochea kuwapo kwa vurugu kila kukicha.

Naye Mufti Mkuu wa Tanzanzia, Sheikh Abubakary Zuber, alisema wao kama viongozi wa kidini ni jukumu lao kulinda maadili ya nchi.

Alisema kupitia hafla hizo ambazo zimekuwa zikiwakutanisha viongozi wa dini tofauti ni chachu ya kuongeza mshikamano baina yao na kuzidi kuomba amani nchini.

"Kuja kwetu hapa sio kuja kula, kama chakula kila mtu amekiacha nyumbani kwake ila tupo hapa kwa dhumuni la kuzidi kuimarisha ushirikiano baina yetu na kuzidi kuifanya nchi kuwa na amani," alisema Sheikh Zuber.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya Khoja Shia, Alhaj Azim Dewji, alisema wameamua kuandaa hafla iyo ili kuwakutanisha viongozi wa dini na jamii ili kuzidi kuimarisha amani nchi. Alisema taasisi hiyo kila mwaka imekuwa ikichunguza watu wenye matatizo ya macho na tayari watu 500 wamefikiwa na kupatiwa matibabu.

"Tumekuwa tukifanya uchunguzi kila mwaka kwa watu wenye matatizo ya macho nchini kwa kuweza kuleta wataalamu ambao wamekuwa wakiwafanyia vipimo na matibabu watu wenye matatizo hayo," alisema Dewji.

Pia alisema wameshachimba visima 400, lengo likiwa ni kusaidia jamii na kuzidi kuiletea nchi maendeleo.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alisema pia ni vyema pia taasisi za dini kuimarisha shughuli mbalimbali za kijamii kama ujenzi wa shule.

"Niwaombe viongozi wangu tuzidi kuimarisha pia shughuli za maendeleo pamoja na kujenga shule, vituo vya afya na kuzidi kusaidia jamii," alisema Polepole.

# JPM apongeza taasisi mashindano ya Qur'aan

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ameipongeza taasisi ya Al-Hikma kwa kuandaa mashindano ya Qur'aan Tukufu yaliyojumuisha nchi mbalimbali za Afrika, kwa kushirikiana na serikali katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

Rais Magufuli alitoa pongezi hizo jana wakati akihutubia katika Mashindano Maalum ya 20 ya Qur'aan Tukufu Afrika yaliyohusisha washiriki kutoka nchi 18 za Afrika na kufanyika katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Rais Magufuli alisema pamoja na kujenga misikiti 50 nchini, serikali inatambua kuwa Taasisi ya Al-Hikma imesaidia jamii kwa kuchimba visima vya maji 110, imejenga shule 1 ya msingi na shule 2 za sekondari na inawasomesha watoto yatima 400.

Kutokana na mchango huo, Rais Magufuli aliishukuru taasisi hiyo pamoja na taasisi zingine mbalimbali zinazomilikiwa na madhehebu ya dini ambazo zimekuwa zikitoa mchango mkubwa katika kuhudumia jamii kwenye sekta za elimu, afya na kutoa misaada ya kibinadamu.

Kufuatia maombi yaliyotolewa na Taasisi ya Al-Hikma, Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, kuhakikisha taasisi hiyo inapatiwa hati ya umiliki wa eneoililoomba libadilishiwe matumizi kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya kitakachotoa huduma kwa wananchi wote ifikapo Ijumaa.

Aidha, Rais Magufuli aliwapongeza washiriki wote wa mashindano hayo ya Qur'aan Tukufu, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Serikali ya Saudi Arabia na wadau mbalimbali kwa kufanikisha mashindano hayo ambayo licha ya kuimarisha misingi ya kumcha Mwenyezi Mungu, yanaimarisha uhusiano baina ya Tanzania na Saudia Arabia pamoja na mataifa yote yanayoshiriki.

Alimtaka Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa Saudi Arabia, Dk. Swalehe Al-Sheikh (ambaye alihudhuria katika mashindano hayo) kufikisha salamu zake kwa Mfalme wa Saudi Arabia, ambapo pamoja na shukrani kwa uhusiano mzuri wa Tanzania na Saudia Arabia aliomba nchi hiyo ijenge msikiti mkubwa nchini kwa ajili ya Waislamu kufanya ibada zao. Rais Magufuli aliwatakia kheri Waislamu wote katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na amezitaka mamlaka za serikali kuchukua hatua dhidi ya wafanyabiashara wenye tabia ya kupandisha bei za vyakula wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuungana na Waislamu katika mashindano hayo na amewataka Watanzania kuendelea kumwombea kutokana na kazi nzuri anazozifanya za kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwa kasi kubwa na kudumisha umoja wa Watanzania.

Naye Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alisema uwapo wa Rais Magufuli katika mashindano hayo na hotuba aliyoitoa imedhihirisha dhamira yake ya kuimarisha umoja na mshikamano wa Watanzania wote na kwamba Waislamu wote wamefarijika sana. Rais Magufuli alikabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano hayo ambapo aliyeibuka mshindi wa kwanza ni Mouhamed Diallo (Senegal), wa pili ni Faruq Kabiru Yakubu (Nigeria), wa tatu ni Shamsuddin Hussein Ally (Zanzibar), wa nne ni Idrissa Ousmane (Niger) na wa tano ni Sumaiya Juma Abdallah (Pwani, Tanzania).

Pamoja na viongozi hao, mashindano hayo yalihudhuriwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa; Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma; Makamu wa Rais mstaafu Dk. Mohamed Gharib Bilal; mawaziri, mabalozi wa nchi mbalimbali na viongozi mbalimbali wa madhehebu ya dini na vyama vya siasa.

# Lugola amtaka RCO kuonyesha jalada kesi TLTC

INATOKA UK. 4

nyeshe jalada haji, basi jalada liletwe tuone nini kimetokea, sikuridhishwa kwa kweli, sababu haiwezekani suala ambalo linaweza kutatuliwa na mimi hadi asubiriwe Rais aje alitatue...haiwezekani," alisema Lugola.

Alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, kuhakikisha RCO anakuwa mbele yake ifikapo saa nane mchana jana ili wapate kuzungumzia suala hilo.

Awali Waziri Lugola alitembelea ofisi za kiwanda cha TLTC na kupata malalamiko hayo na kuahidi kuyashughulikia na kuhakikisha anajua mwisho wake kabla hajaondoka mkoani Morogoro.

Akizungumza mbele ya Waziri Lugola Mkurugenzi wa kiwanda TLTC, Richard Sinamtwa, alisema wamepata usumbufu kwa muda wa saa nane toka asubuhi mwezi Septemba mwaka 2018 wakati askari walipofika kwenye ofisi zao wakitaka kuwakamata na kuwafikisha polisi kuwa wanakesi inawakabili.

Alisema, waliwauliza kuwa wanawakamata kwa kosa lipi walikosa jibu na kudai waende faili watalikuta polisi jambo ambalo liliwafanya washindwe kutii amri hiyo na ndipo walipokumbuka kumpigia simu RCO na kuwaambia waende jioni na baadaye akawaambia waende asubuhi.



Sinamtwa alisema, walipofika kituoni wakaomba faili lao ili wajue wanaanzia wapi wakaambiwa hakuna na baadaye walikwenda ofisini kwa RCO naye aliwaambia waende wakafanye kazi zao wakihitajika wataambiwa jambo ambalo hawajajua hatima yake mpaka leo licha ya kuandika barua kuomba maelezo ya shauri lile.

Hata hivyo, Sinamtwa alisema, kampuni ilimsimamisha kazi mmoja wa wafanyakazi wake na shauri bado lilikuwa ndani ya kiwanda halijamalizika na kama ndiye yeye muhusika hakuona haja ya kwenda polisi wakati kwao walikuwa hawajamaliza mashauriano.

# Mufti Mkuu aitabiria mema NMB kwa kujali jamii

INATOKA UK. 5

Aliitaka benki hiyo kutoacha tamaduni ya kufungamanisha makundi kwa kufuturisha waumini wa Kiislamu na kuutaka uongozi kuufanya utamaduni huo kuwa wa kudumu ili pindi awamu moja ya uongozi inapomaliza muda wake, iache alama kwa jamii.

Awali akimkaribisha Mufti Zubeir, Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Albert Jonkergouw, alisema benki yake inajisikia furaha kuungana na Waislamu katika kutimiza moja ya nguzo muhimu za dini yao, huku akiahidi kuwa NMB itaendelea kusapoti na kushirikiana na jamii.

Alisema tukio hilo ni la pili tangu kuanza kwa mfungo wa Ramadhani mwaka huu, baada ya kukutanisha, kufuturisha na kujadiliana kwa ufupi na Waislamu wa Jiji la Tanga na kwamba wamepanga kufuturisha katika miji kadhaa Tanzania Bara na Visiwani.

"Tukio kama hili leo linafanyika mjini Iringa, awali lilifanyika Tanga na sasa tunaelekea Zanzibar (Unguja na Pemba), na pia mikoa ya Mtwara, Mwanza na kwingineko kulingana na ratiba itakavyoturuhusu," alisema Jonkergouw.

Akijibu wito wa Mufti Zubeir, aliyeomba mwendelezo wa hafla za kufuturisha, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd, alisema benki hiyo itaendelea na utaratibu wa kufuturisha waumini wa Kiislamu na kwamba wamefanya hivyo mara nyingi na wataendelea.

# Serikali kupanga maeneo itakayopita reli ya kisasa

INATOKA UK. 5

na fursa za kiuchumi za mradi wa reli hiyo.

Alisema lengo la serikali ni kutaka mpango mzima wa uendelezaji ukanda wa kiuchumi katika maeneo hayo ufahamike kitaifa na kimataifa ili kuvutia wawekezaji watakaotaka kuja kuwekeza na kubainisha kuwa fedha kwa ajili ya mpango huo zimeshatengwa.

Aliwatahadharisha wananchi wa vijiji hivyo kutokubali kuuza maeneo yao kwa kuwa baada ya kupangwa kwa maeneo thamani ya ardhi itapanda na tayari baadhi ya watu wajanja kutoka nje ya vijiji hivyo wameanza kutafuta maeneo kwa ajili ya fursa hiyo.

Alisema, si vyema kila wilaya kikawa na mpango wake wa uendelezaji wa maeneo itakapopita reli hiyo bali serikali inachotaka ni kuwa na mpango wa kitaifa utakaotoa mwongozo kwa wilaya zote kusisitiza kuwa ardhi katika maeneo hayo itasimamiwa na wilaya husika.

"Tukiacha maeneo ya kandokando ya reli bila kupanga na kupima kutafanyika vitu vya ajabu, reli hii ina faida kubwa hivyo lazima kupanga maeneo inakopita ili kwenda sambamba na shughuli za kiuchumi za maeneo hayo," alisema Lukuvi.

Kwa mijibu wa Lukuvi, kuna timu imeundwa kwa ajili ya Mpango wa Uendelezaji Ukanda wa kiuchumi katika eneo inakopita reli ya SGR na timu hiyo inashirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali kama vile za nishati, uchukuzi, reli na mawasiliano, lengo likiwa kuwa na mpango utakaokidhi mahitaji ya uendelezaji ukanda kiuchumi katika eneo linakopita reli ya SGR.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.

### MCHANGANYIKO

**KIWANJA KINAUZWA,** KIWANJA KUNAUZWA PLOT NO. 97 BLOCK M, MEDIUM SIZE KILWA MASOKO MTAA MIINA OPOSITE UWANJA WA NDEGE BEI MAELEWANO. TEL. 0712 566677, 0753 907281.

**MONKAL I INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu kwa waliogua muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,vidonda vya tumbo kuunguruma na kujaa gesi n.k kama umehangaika huku na kule bila mafanikio njoo nikusaidie acha kuteseka:0713293988/0758078288

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

### CHETI KIMEPOTEA



**ADAM KIBOLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Sita chenye **index namba S0342-0556** kilichotolewa na SHAABAN ROBERT SEKONDARI mwaka 2000. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/241/2019.**

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# CAVANI ATAKA KUBAKI PSG

**PARIS, Ufaransa**

EDINSON Cavani amesisitiza kwamba anataka kubaki kwenye Klabu ya Paris Saint-Germain kumaliza mkataba wake.

Umekuwa mwisho mgumu kwa PSG, lakini kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel kiliibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Dijon ukiwa mchezo wao wa mwisho nyumbani msimu huu.

Cavani alifunga bao la pili dakika nne baada ya Angel Di Maria kufunga la kwanza na akafikisha mabao 23 msimu huu kwenye mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na amekuwa akihuishwa na mpango wa kuondoka hapo Parc des Princes, huku klabu yake ya zamani ya Napoli ikitajwa kwamba inamtaka.

Na Cavani sasa amebainisha wazi kwamba hana mpango wa kuondoka Paris na anataka kumaliza mkataba wake hapo.

"Ni raha kuwa na mabingwa wa Ligue 1, mambo kama haya yanakufanya uwe kwenye historia," alisema Cavani akiiambia Canal+.

"Mashabiki walituonyesha upendo. Ni vizuri nawashukuru. Kuhusu kuondoka? Kitu cha kwanza naheshimu mkataba.

"Naipenda klabu hii, nina furaha na familia hii. Soka hainitegemei mimi tu, lakini ningependa kubaki hapa na kumaliza mkataba wangu.

"Kurudi Napoli? Hapana. Siwezi kusema chochote. Bila shaka nitakuwa hapa msimu ujao."





# PSG YAWANYATIA AUBAMEYANG, FIRMINO

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, amewataja nyota wake anaowataka kuwanasa kwenye dirisha hili la usajili na habari mbaya kwa Liverpool na Arsenal ni kwamba Roberto Firmino na Pierre-Emerick Aubameyang wapo kwenye mpango wake.

PSG ina kundi kubwa la wachezaji wenye vipaji vikubwa kama vile Neymar, Kylian Mbappe na Edinson Cavani, lakini wanataka kuwaongeza Firmino na Aubameyang kwenye orodha hiyo ili kuwanyoosha wapinzani wao msimu ujao.

Wameanza pia mazungumzo na Mbappe kwa ajili ya kumpa mkataba mpya, lakini ripoti zinadai Neymar na Cavani wanaweza kufungasha virago vyao na kuondoka kwenye timu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Hakuna ubishi Arsenal na Liverpool hazitakuwa tayari kuwaachia washambuliaji wake hao.

Firmino alitua Liverpool akitokea Hoffenheim mwaka 2015 na Aprili mwaka jana alisaini dili jipya la miaka mitano kudumu hapo Anfield, wakati Aubameyang ndiyo kwanza hata mwaka mmoja na nusu hajafikisha kwenye kikosi cha Arsenal.

Kocha huyo anataka kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

# Rashford aiwekea ngumu Man United

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 21, amewagomea mabosi hao kuanza mazungumzo mapema kwa ajili ya kusaini mkataba mpya kwa ajili ya msimu ujao akiwa chini ya Meneja Ole Gunnar Solskjaer.

Rashford kwa sasa anajukumu la kufanya maamuzi kuhusu kujiunga na kikosi hicho msimu ujao ama kuangalia maisha mengine akiwa nje ya Manchester United.

Klabu ya Man United inahitaji huduma ya mshambuliaji huyo ambaye anachezea timu yake ya Taifa ya England, wamejipanga kumpa dili kwa ajili ya misimu miwili ijayo.

Kwa mujibu wa The Sun, Rashford ameuambia uongozi wa klabu hiyo kwamba hana mahitaji ya kuongea na klabu hiyo kutokana na matamanio yake aliyonayo hapo baadaye.

Imeripotiwa kwamba Rashford amekuwa akilalamika juu ya imani yake kwa meneja Solskjaer akiamini kwamba uwezo wake umeshuka ghafla hali iliyofanya washindwe kutinga nne bora kwenye Ligi Kuu England na kukosa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kitu alichokuwa akikipigia hesabu muda mrefu.



## HABARI MICHEZO



# RONALDO AMSHUKURU ALLEGRI AKISEPA JUVE

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo amemshukuru Massimiliano Allegri baada ya kocha huyo kutangaza kwamba ataondoka Juventus mwishoni mwa msimu huu.

Majaliwa ya Allegri yalikuwa shakani tangu Juve ilipotolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ajax Aprili mwaka huu, huku 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kikiwa na matarajio ya kubeba ndoo hiyo kwa kumsajili Ronaldo.

Lakini Ijumaa, Juve ilitangaza kwamba Allegri hataendelea kuwapo hapo msimu ujao, licha ya kushinda taji la Serie A na kubakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Allegri alishindwa kuzuia machozi yake wakati wa mkutano na waandishi wa habari pamoja na rais wa klabu hiyo, Andrea Agnelli akizungumza kwa mara ya kwanza baada ya tangazo hilo.

Agnelli alizungumzia kuhusu kazi nzuri aliyoifanya Allegri pamoja na ushirikiano wake mzuri na mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo pia alisema anatarajia timu itakuwa imara zaidi msimu ujao.

Ronaldo aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram akisema: "Asante kocha, tumekuwa pamoja kwa mwaka mmoja tu, lakini ulikuwa wakati bora zaidi kwangu kuwa pamoja na wewe. Ulikuwa wakati mzuri zaidi kwangu kufanya kazi na wewe."

# Mbappe amfukuzia Messi Kiatu cha Dhahabu

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amemkaribia Lionel Messi kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora Ulaya wakati alipofunga mara mbili kuwasaidia mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain kuibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Dijon, juzi Jumamosi.



Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, Mbappe, alirudi uwanjani kutoka kufungiwa mechi tatu baada ya kuonyeshwa kazi nyekundu kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa, alifunga mara mbili na kufikisha mabao 32, akipitwa mawili na nyota wa Barcelona, Messi mwenye mabao 34 kwenye La Liga.

PSG ilifikisha pointi 91 kwenye mchezo huo ambapo, Angel Di Maria na Edinson Cavani kila mmoja alifunga bao moja.

Halafu Mbappe akafunga mara mbili na kufikisha mabao 32 kwenye ligi hiyo ikiwa ni kwa mara ya kwanza mchezaji wa Ligue 1 kufikisha idadi hiyo ya mabao tangu Philippe Gondet alipofanya hivyo akiwa na Nantes msimu wa mwaka 1965-66.

PSG ambayo ilishatwaa ubingwa wa ligi hiyo, sasa imebakiwa na mchezo mmoja wa kufungia ligi hiyo msimu huu.

Mbappe na Messi wanafukuzia tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa kufunga mabao mengi katika ligi tano kubwa Ulaya; La Liga, Premier League, Serie A, Bundesliga na Ligue 1.

# Sancho sasa anogewa Dortmund, haondoki

**DORTMUND, Ujerumani**



JADON Sancho amesema ana matumaini ya kushinda taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Borussia Dortmund msimu ujao, huku akiwa anahusishwa na mpango wa kuhamia Ligi Kuu ya England.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye aliwasili hapo Dortmund kutoka Manchester City mwaka 2017, amekuwa akiripotiwa kwamba anawaniwa na Manchester United baada ya kuwa na msimu mzuri zaidi pale Ujerumani.

Sancho amefunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 14 katika mechi 34 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na hivyo kuvuta hisia za klabu nyingi Ulaya.

Kushindwa kwa Dortmund kuipiku Bayern Munich kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kuliongeza uwezekano wa Sancho kuondoka klabuni hapo, lakini ameonyesha ishara kwamba atabakia hapo kwenye dimba la Signal-Iduna-Park msimu wa 2019-20.

"Nina furaha kubwa jinsi nilivyocheza msimu huu," alisema Sancho akiwaambia waandishi wa habari baada ya Dortmund kushinda 2-0 dhidi ya Borussia Monchengladbach kwenye mchezo wa mwisho wa kufunga msimu huu, ambapo Bayern ilitwaa ubingwa huo kwa kuongoza kwa pointi mbili.

"Kamwe sikujua itakuwa hivi. Tangu mwanzo sikuwa nacheza mara kwa mara, lakini nikaanza kucheza mara kwa mara kwenye msimu huu. Nilifanya kazi kwa bidii kubwa.


"Timu ilinisaidia mimi na kocha alikuwa na imani na mimi na namshukuru Mungu. Msimu ujao malengo ni kushinda taji, na siyo kumaliza nafasi ya pili."

Mchezaji mmoja wa Dortmund ambaye ataondoka kwenye klabu hiyo ni Christian Pulisic, ambaye anakwenda Chelsea baada ya kukaa hapo kwa msimu mmoja kwa mkopo.

Sancho alimtakia kila la heri mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani kwa kusema: "Kwa uhakika nitakumisi Pulisic.

"Nina furaha juu yake na namtakia kila la heri pale. Nina uhakika atakwenda kufurahia maisha yake pale na nitammisi yeye."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: UBINGWA UEFA RAHISI KULIKO EPL

**LONDON, England**

PEP Guardiola anahisi kwamba, Manchester City kushinda mataji matatu nchini England ni ngumu zaidi kuliko kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini ametabiri wanaweza kurudia mafanikio hayo.

Kikosi cha Guardiola kiliifunga Watford mabao 6-0 kwenye Uwanja wa Wembley juzi Jumamosi na kutwaa taji la FA, ikiwa tayari imetwaa Kombe la EFL na la Ligi Kuu England msimu huu.

City ilianza msimu huu kwa kutwaa taji la Ngao ya Jamii dhidi ya Tottenham ambao waliwatoa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ni moja ya misimu bora zaidi niliyoishuhudia kama kocha. Siwezi kusema bora zaidi, lakini nina uhakika ulikuwa msimu bora," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Kucheza kwenye mashindano yote si jambo rahisi kwa sababu katika nchi hii kuna timu nyingi bora na hivyo naweza kusema msimu ulikuwa mzuri.

"Naipenda Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kushinda mataji ya England ni ngumu zaidi kuliko kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwa timu kama hii na mmiliki wake Sheikh Mansour pamoja na wachezaji wenyewe wamefanya jambo kubwa nawapongeza. Kwa sabau siyo rahisi kucheza kila baada ya siku tatu, ni ngumu mno.

"Leo (juzi) tulicheza bila ya kuwa na nguvu kubwa, kushinda taji la Ligi Kuu ni ngumu mno. Wiki hii hatukuweza kutulia na kuhifadhi nguvu zetu, lakini tulicheza vizuri na kutwaa taji."

Guardiola alisisitiza kwamba City inaweza kuwa bora zaidi na alidokeza ataingia kweye soko la usajili kwa ajili ya kuongeza nguvu zaidi katika kikosi chake.

"Kila mmoja alitoa mchango wake, makosa yalijirudia kwa baadhi ya wachezaji na wanatakiwa kuimarika zaidi, pengine wachache watakuja kuongeza nguvu kwenye uchezaji," aliongeza Guardiola.

"Hatuwezi kusahau tumeshinda taji la Ligi Kuu kwa pointi moja dhidi ya Liverpool, hatuko mbali.

"Nilisema jana Liverpool walituonyesha ugumu ulivyo, ubora tuliokabiliwa nao, tulijitahidi kuimarika, lakini mara zote unaweza kuimarika, lakini naweza kusema niliridhishwa."

## KWA UFUPI

### JESUS KUMPISHA RODRIGO CITY

Manchester City inapewa nafasi kuihamishia huduma ya kiungo wa Atletico Madrid, Rodrigo, 22, Ligi Kuu England - lakini kocha Pep Guardiola atapaswa kumuuza kwanza mshambuliaji wa Kimataifa wa Brazil, Gabriel Jesus, 22. ***(Sun on Sunday)***

### PSG KUMNASA DE GEA BURE

Paris St-Germain ipo tayari kumshawishi kipa wa Manchester United, David de Gea, 28, kuhitimisha kipindi chake cha mkataba kilichobaki na klabu hiyo na kisha kutua kwao akiwa mchezaji huru. ***(Sunday Express)***

### ARSENAL YAMTAKA ZAHA

Arsenal inamtaka mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 26, lakini inataka kulipa pauni milioni 40 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, ikiwa ni nusu ya thamani Palace iliyopanga kwake. ***(Sun on Sunday)***

### KANTE ATAVUTIWA PUMZI PSG

Paris St-Germain inataka kumsajili kiungo wa kimataifa wa Ufaransa na Chelsea, N'Golo Kante, 28, majira haya ya joto. ***(Sunday Mirror)***

### ALLEGRI, POCHETTINO KUPISHANA

Tottenham inaweza kumgeukia kocha aliyeachana na Juventus, Massimiliano kama Mauricio Pochettino ataondoka na kujiunga na klabu hiyo ya Italia baada ya mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sunday Express)***

### LLORENTE, BALE, NAVAS KUSEPA

WINGA wa Wales, Gareth Bale, 29, kiungo Mhispania Dani Ceballos, 22, kipa Mcosta Rica Keylor Navas, 32, na kiungo raia wa Hispania, Marcos Llorente, 24, wote wanajiandaa kuondoka Real Madrid majira haya ya joto. ***(Marca)***

### HUDSON-ODOI UZI WA HAZARD

Chelsea itampa ofa winga wa kimataifa wa England, Callum Hudson-Odoi, 18, jezi namba 10 itakayoachwa na Eden Hazard majira haya ya joto lengo likiwa ni kumshawishi kusaini mkataba mpya na klabu hiyo mwezi huu. (Mail on Sunday)

### WAN-BISSAKA BEI JUU

Crystal Palace imetaja dau la pauni milioni 60 kama bei sahihi kwa beki wao wa kulia Aaron Wan-Bissaka, 21, lengo likiwa ni kuizuia Manchester United kumpigia kasi. (Mail on Sunday)

### RASHFORD KUSHAWISHIWA KWA MSHAHARA

Manchester United inaamini straika wa kimataifa wa England, Marcus Rashford, 21, atasaini mkataba mpya, kwa ofa ya mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki ikiwa ni zaidi ya mara tatu ya mkataba wake wa sasa. ***(Star on Sunday)***

### POGBA KUJITOSA MADRID

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 26, anajiandaa kukatwa malipo yake ili kufanikisha uhamisho wake wa kujiunga na Real Madrid. ***(Manchester Evening News)***

### ARSENAL KWA CLAUDE-MAURICE

Arsenal ipo tayari kumfuata mshambuliaji wa Lorient na Ufaransa U-20, Alexis Claude-Maurice, ambaye anathaminishwa na pauni milioni tisa ambaye pia ameivutia wapanda daraja msimu huu, Norwich. ***(Sunday Express)***

### LOOKMAN ATANGAZIWA BEI

Everton inataka pauni milioni 20 kwa winga wa England U-21, Ademola Lookman, 21, wakati huu ikitazama kuuza takriban wachezaji 15 wa kikosi chake majira haya ya joto. ***(Mail on Sunday)***

### CHELSEA KUWAREJESHA ABRAHAM, ZOUMA

Chelsea itawarejesha Tammy Abraham, 21, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Aston Villa, na Kurt Zouma, 24, ambaye ameutumia msimu huu kwa mkopo Everton - kama tu kifungo chao cha kusajili kutoka Fifa kitaendelea kama kilivyotangazwa. (Sun on Sunday)

# SERIKALI, TFF SASA KUMTUZA SAMATTA

**Na Somoe Ng'itu**

SERIKALI pamoja na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanatarajia kumpa pongezi maalumu mshambuliaji wa timu ya KRC Genk, Mtanzania Mbwana Samatta kwa mafanikio ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ubelgiji msimu huu.

Kutokana na kutwaa ubingwa huo, Samatta msimu ujao atashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa ni mara ya kwanza kwa Mtanzania huyo kushiriki michuano hiyo mikubwa duniani kwa ngazi ya klabu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema hatua ambayo Samatta amefikia ni kubwa na anastahili kupongezwa kwa sababu ya kupeperusha vema bendera ya Tanzania.

Waziri Mwakyembe alitaka mafanikio ya Samatta kuchukuliwa kama changamoto kwa wachezaji wengine kupambana na kutokata tamaa kwa lengo la kufikia hatua kama hiyo. "Kama serikali tutampongeza, amefanya vizuri yeye pamoja na klabu yake, kila atakapopita jina la Tanzania litaendelea kutajwa," alisema waziri huyo.

Naye Rais wa TFF, Wallace Karia, aliliambia Nipashe kuwa wanampa pongezi za dhati mshambuliaji huyo na nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) kutokana na mafanikio ambayo amefikia msimu huu.

"Tumefurahi sana, kama shirikisho tunaahidi tutampa pongezi rasmi kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ubelgiji sio jambo dogo, ameweka historia nyingine nzuri kwa nchi yetu," alisema rais huyo.

Karia aliongeza kuwa Samatta alisema kuwa yeye sasa hivi si nahodha wa Taifa Stars bali ni nahodha wa Watanzania na kauli yake hiyo imeanza kuonekana kwa vitendo tangu alipoongoza vita ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Afrika (Afcon 2019).

Samatta mshambuliaji wa zamani wa African Lyon na Simba za jijini Dar es Salaam, alijiunga na KRC Genk mwaka 2016 akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (wa tatu kushoto), akikabidhi vifaa vya michezo kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Tabora Girls, (waliovaa nguo za rangi ya njano) wakiwa pamoja na mwalimu wao Jacob Kavageme (kulia) wakati wa hafla ya uzinduzi wa michuano ya Copa Coca-Cola UMISSETA kwa Mkoa wa Tabora uliofanyika jana mkoani humo. Wengine katika picha ni Meneja Chapa mwandamizi wa Kampuni ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (kushoto) na Meneja Mauzo na Masoko wa Nyanza Bottling Company, Samwel Makenge (wa tatu kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Coca-Cola yazindua rasmi Copa UMISSETA Tabora

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

Kampuni ya Coca-Cola, Tanzania imezindua mashindano ya Copa UMISSETA 2019 katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, ikiwa ni baada ya mafanikio makubwa ya uzinduzi kama huo kufanyika hivi karibuni mkoani Manyara na Dodoma.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema michezo ni sehemu muhimu katika malezi ya vijana na kwamba humtengeneza mtu kufanya kazi kwa bidii, hujenga timu ya pamoja, uvumilivu na ubora zaidi uwanjani.

Alisema: "Nitoe shukurani na pongezi za dhati kwa Kampuni ya Coca-Cola kwa kuwa jicho kwenye soka la vijana nchini Tanzania. Uwekezaji wenu katika soka kwa zaidi ya miaka mitatu sasa umekuwa kichocheo cha maendeleo ya vipaji kwa klabu zetu za ndani na pia kwa timu yetu ya Taifa Stars."

Mashindano ya mwaka huu yamebuniwa mahususi kuwezesha ukusanyaji wa chupa za plastiki kwa shule shiriki kwenye michezo ya Copa Coca-Cola UMISSETA 2019.

Kupitia kampeni hiyo, wanafunzi. walimu na jamii wanapata fursa ya kujifunza zaidi juu ya faida za utunzaji mazingira kupitia dhana ya urejeshaji wa chupa hizo na kuwashawishi wengine kuchukua hatua kama hizo kuanzia kwa wanafunzi, walimu na jamii nzima kwa ujumla.

Meneja Mauzo na Masoko wa Nyanza Bottling Company Ltd, Samwel Makenge alisema: "Ikiwa ni sehemu ya kampeni, wanafunzi wa shule za sekondari wataelimishwa na kupewa mafunzo ya namna ya kuileta jamii karibu ili itambue umuhimu wa kuhifadhi mazingira yetu kupitia dhana ya urejeshaji. Ili kuwapa motisha washiriki wa kampeni hii, Coca-Cola imedhamiria kutoa tuzo na zawadi mbalimbali ikiwamo maboresho ya uwanja wa mpira wa miguu kwa shule ambayo itaibuka mshindi wa jumla wa kampeni hii," aliongeza Makenge.

Zawadi nyingine ni pamoja na mashine moja ya kudurufu, projekta mbili, kompyuta mpakato 108, kompyuta 11, vishikwambi (Tablets) 108, saa 12, jezi 1176 na mipira 360 kwa washindi wa kila kipengele katika kampeni hiyo.

Mashindano ya Copa Coca-Cola yameendelea kuongoza Tanzania kwa kuibua na kuwaunga mkono wachezaji mbalimbali ambao wameendelea kufanya vizuri ndani na nje ya nchi akiwamo Thomas Ulimwengu, Simon Msuva, Aishi Manula, Shomari Kapombe, Hassan Kessy, Yusuph Soka pamoja na timu ya Taifa, Taifa Stars.

## Rais wa zamani ZFA afariki dunia, azikwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ALIYEKUWA Rais wa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) kwa sasa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Fereji Tamimu amefariki dunia.

Fereji ambaye anakumbukwa kwa kuiongoza ZFA kwa miaka mingi mpaka alipojiuzulu mwaka 2012, alifariki katika Hospitali ya Mnazimmoja alfajiri ya kuamkia jana.

**Marehemu Fereji ambaye alitoa mchango mkubwa katika soka la Zanzibar alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa saratani kwa muda mrefu ambapo aliwahi kusafirishwa hadi India kwa matibabu zaidi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa familia ya Fereji, Lageet Khalid Tamim, alisema msiba wake ni pengo kwa familia ingawa hakuna makosa kwa mwenyezi Mungu.

Alisema marehemu alilazwa katika Hospitali ya Mnazimmoja wodi ya saratani kabla ya kufariki alfajiri kuamkia jana.

Fereji ambaye alizikwa jana, atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika soka ambapo mbali ya kuwa Rais wa ZFA, lakini pia aliwahi kuwa kiongozi katika Klabu Kongwe ya soka Zanzibar ya Malindi.

Marehemu ameacha mjane na watoto wawili na alizikwa katika makaburi ya Mwanakwerekwe mjini Unguja jana baada ya kusaliwa katika msikiti mkuu wa Malindi. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.SIMBA | 35 | 28 | 4 | 3 | 74 | 14 | 88 |
| 2.YANGA | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 3.AZAM | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4.KINONDONI MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5.MTIBWA SUGAR | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6.LIPULI | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7.MBEYA CITY | 36 | 13 | 8 | 15 | 38 | 38 | 47 |
| 8.NDANDA | 36 | 12 | 11 | 13 | 23 | 33 | 47 |
| 9.SINGIDA UNITED | 36 | 11 | 12 | 13 | 30 | 37 | 45 |
| 10.STAND UNITED | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 11.ALLIANCE | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 12.COASTAL UNION | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13.MBAO | 36 | 11 | 11 | 14 | 26 | 38 | 44 |
| 14.TZ PRISONS | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15.KAGERA SUGAR | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 16.RUVU SHOOTING | 36 | 10 | 12 | 14 | 33 | 41 | 42 |
| 17.KT TANZANIA | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 18.BIASHARA UNITED | 35 | 10 | 10 | 15 | 27 | 33 | 40 |
| 19.MWADUI | 36 | 10 | 8 | 18 | 41 | 51 | 38 |
| 20.AFRICAN LYON | 36 | 4 | 11 | 21 | 23 | 49 | 23 |

# Michezo

Jumatatu Mei 20, 2019

Nipashe




## Guardiola: Ubingwa Uefa rahisi kuliko EPL

HABARI UK 30

NDOO...




Nahodha wa Manchester City, Vincent Company, akinyanyua Kombe la FA juu na kusherehekea na wachezaji wenzake baada ya kukabidhiwa 'ndoo' hiyo kufuatia kuichapa Watford kwa mabao 6-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi. **HABARI UK. 30**

# KAGERE AMPIKU OKWI, SIMBA UBINGWA BADO 2

●●● Sasa kutangazia ubingwa kwa Singida United kesho, hesabu zagoma Yanga...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya tano wakati akitupia mawili dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Uhuru jana, lilimwezesha mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere kuvunja rekodi ya mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara msimu uliopita, Emmanuel Okwi.

Kwa bao hilo, limemwezesha kufikisha mabao 21 na kuyapiku 20 aliyofunga mshambuliaji mwenza wa Simba, Okwi msimu uliopita ambayo yalimwezesha kutwaa Kiatu cha Dhahabu.

Hata hivyo, Kagere aliongeza bao la pili katika mechi hiyo waliyoshinda 2-0, hivyo kufikisha mabao 22 hadi sasa msimu huu, wakati huu akiwaacha Heritier Makambo wa Yanga na Salim Aiyee wa Mwadui FC wenye mabao 16 kila mmoja huku washambuliaji wenza wa Simba, Okwi na John Bocco wakifuata kila mmoja akiwa amecheka na nyavu mara 15 msimu huu.

Aidha, kwa ushindi huo, Simba ipo kileleni na pointi 88 baada ya kushuka dimbani mara 34, ikiwa ni alama tano mbele ya Yanga iliyocheza mechi 36. Hivyo inahitaji alama mbili tu ili kutetea ubingwa wao msimu huu.

Na kama Simba itaibuka na ushindi ugenini dhidi ya Singida United kesho Jumanne, itatawazwa rasmi kuwa mabingwa wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2018/19 kabla hata ya kuivaa Biashara United na kisha kufunga msimu Mei 28, mwaka huu dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Pointi mbili zitaifanya timu hiyo kufikisha alama 90 ambazo hazitofikiwa na timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu, huku pointi moja inaweza kuifanya Simba kuwa bingwa kwani itafikisha pointi 89 ambazo Yanga inaweza kufikisha kama ikishinda mechi zake mbili zilizobaki, lakini Simba ina uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa, hivyo itailazimu Yanga kushinda zaidi ya mabao 30 kwa mechi mbili.

Simba imefunga mabao 74 na kufungwa 14, hivyo tofauti ya mabao yake ya kufungwa na kufungwa ni mabao 60, wakati Yanga yenye mabao 55, ikiwa imefungwa 25, ina tofauti yake ni mabao 30.

Simba ilianza mechi hiyo ya jana kwa kasi na iliwachukua dakika tano tu kuweza kupata bao lililofungwa na Mnyarwanda Kagere kwa shuti kali, baada ya kupata pasi kutoka kwa Bocco na kumwacha kipa Deal Makonga akishangaa.

Dakika sita baadaye Kagere alifunga bao la pili baada ya kuwazidi mbio mabeki wa Ndanda, kabla ya kumvisha kanzu kipa Makonga na mpira ukajaa wavuni.

Kipindi cha pili Ndanda ilibadilika na kuwapa wakati mgumu Simba ambayo nayo ilipata nafasi kadhaa kupitia kwa Kagere, Bocco na Chama, lakini hawakuzitumia vema.

Kutoka kwa Kiggi Makasi na kuingia kwa mchezaji wa zamani wa Yanga, Yusuph Mhilu kuliisaidia sana Ndanda, lakini umaliziaji wao wakiongozwa na Vitalis Mayanga, haukuwa mzuri.

Kwenye mechi hiyo pia kulikuwa na kurejea kwa beki Paschal Wawa ambaye alikuwa majeruhi tangu kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya TP Mazembe iliyochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kutoka sare ya bila kufungana.

## Sevilla kutua Dar kesho

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa kihistoria wa michuano ya Europa League, waliomaliza nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu huu, Sevilla FC wanatarajiwa kuwasili nchini kesho kwa ajili ya mechi ya kirafiki dhidi ya Simba ikiwa ni mara ya kwanza katika historia kwa timu kutoka nchini humo kucheza soka Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam, timu hiyo inatarajiwa kuwasili kesho jioni katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

Kulingana na taarifa hiyo, mechi hiyo itakuwa ni maalum kwa vinara hao wa 'La Liga ambao wanadhaminiwa na SportPesa' na kwamba ziara itahusisha matukio kadhaa ya jamii na michezo ikiwamo kliniki na mafunzo mbalimbali.

"Kama ushindani wa kimataifa unakutana na dhamira ya La Liga kuwa karibu na mashabiki wake. Kwa kweli mashabiki wetu wa Tanzania wataweza kupata fursa ya kuangalia karibu klabu kubwa kama Sevilla FC inamaanisha kuwa ni fursa kubwa kwa kila mtu," alisema Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kimataifa wa Ligi ya La Liga, Oscar Mayo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usimamizi wa Utawala na Utekelezaji wa SportPesa, Tarimba Abbas, alisema kampuni yao imeshirikiana na baadhi ya taasisi za soka kubwa ulimwenguni baada ya kuona kuna haja ya kuleta uzoefu huu mkubwa Tanzania.

"Ili kufurahia kuona moja ya klabu kubwa za mpira wa miguu Ulaya, Sevilla FC kwa makubaliano yetu na La Liga ambayo ni ligi bora duniani, tutaweza kuonyesha vipaji vyetu na kuboresha kiwango cha soka nchini," alisema Talimba.

Alisema mechi hiyo ni sehemu ya mradi wa 'La Liga duniani ambao unalenga kueneza soka la Hispania kimataifa na kueneza pia sera ya 'Marca Espana', kuleta karibu mashabiki wa La Liga na kukuza klabu nje ya nchi.

Hii itakuwa ni klabu ya pili Ulaya kufanya ziara Afrika Mashariki, baada ya mwaka 2017 Everton FC kucheza na Gor Mahia ya Kenya katika Uwanja wa Taifa, ingawa si mara ya kwanza kwa Sevilla kutua barani Afrika kwa kuwa mwaka 2015 ilikuwa nchini Morocco ambapo ilicheza mechi ya kuajindaa na msimu wa La Liga dhidi ya timu ya Hassania Union Sport d'Agadir.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >